

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA ISHIRINI**

**Kikao cha Nne – Tarehe 10 Juni, 2005**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

**Na. 31**

**Uchaguzi Mkuu**

**MHE. ALI SAID SALIM** aliuliza:-

Kwa kuwa Uchaguzi Mkuu unakaribia; na kwa kuwa, katika chaguzi mbili zilizopita kwa upande wa Tanzania Zanzibar zililalamikiwa sana ndani na nje ya nchi yetu hali iliyosababisha machafuko na watu kadhaa kupoteza maisha yao, na kwa kuwa hali hiyo iliitia nchi yetu aibu kubwa katika uso wa Kimataifa:-

- (a) Je, Serikali inajiandaa vipi kuhakikisha kuwa matukio kama hayo hayatokei tena hapa nchini kwetu katika uchaguzi ujao wa 2005?
- (b) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa iko haja ya kuwaalika waangalizi wa uchaguzi (*observers*) kutoka nje waje kuangalia uchaguzi kuanzia hatua za kampeni hadi wakati wa kutangaza matokeo ya uchaguzi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Said Salum, Mbunge wa Ziwani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1995 na 2000 kwa upande wa Tanzania Bara hakuna vurugu zozote zilizowahi kutokea na kusababisha roho za

watu kupotea na hivyo kuliaibisha Taifa kama anavyodai Mheshimiwa Mbunge. Kinyume chake, uchaguzi zote hizo zilisifiwa na kupongezwa na Vyama vya Siasa na waangalizi wa nje na ndani. Serikali imejiandaa kufanya uchaguzi ujao kwa kufuata Katiba na Sheria za uchaguzi ili uwe huru na haki na kuendeshwa kwa salama na amani.

(b) Mheshimiwa Spika, katika uchaguzi zilizopita, Serikali na Tume ya Taifa ya Uchaguzi yaani *NEC* imekuwa ikiruhusu waangalizi wa Uchaguzi (*Election Observers*) kutoka ndani na nje ya nchi kuangalia zoezi la uchaguzi linavyoendeshwa, na hivyo ndivyo itakavyokuwa kwa Uchaguzi wa mwaka huu 2005.

Katika uchaguzi mkuu wa mwaka 1995, Asasi za nje zipatazo tano zikiwemo Jumuiya za Kikanda, mfano *OAU*, *EEC* na *the Commonwealth* pamoja na nchi zipatazo kumi na nne za Ulaya, Marekani, Mashariki ya Mbali na Afrika zilialikwa kuleta waangalizi wao. Aidha, kwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2000, Asasi zipatazo 12 za nje na ndani na hali kadhalika nchi 24 kwa makundi kama nilivyoainisha hapo juu zilialikwa.

Mheshimiwa Spika, aidha kama Mheshimiwa Mbunge swali lake anakusudia kuongelea kuhusu uchaguzi wa Zanzibar namshauri amwombe mwakilishi wake aulize swali hilo katika Baraza la Wawakilishi ili apate majibu ya fasaha na ya kina kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya *ZEC* huko Zanzibar. (*Makofi*)

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, swali ndogo la nyongeza. Kwa kuwa shughuli za siasa ni suala la Muungano Mheshimiwa Waziri haoni kutokujibu swali hilo amekwepa wajibu wake wa Kikatiba? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB):** Mheshimiwa Spika, kuna swali la siasa la ujumla na swali la uchaguzi *particularly*. Yeye alikuwa anazungumza kuhusu uchaguzi wa Zanzibar. (*Makofi*)

**SPIKA:** Sahihi.

**WABUNGE FULANI:** (*Kicheko*)

Na. 32

### **Mpango wa EPZ na SMEs**

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika msingi sera na malengo ya Bajeti ya mwaka 2004/2005 moja ya mambo muhimu ya uchumi ni kuwa na kiwango cha ukuaji wa uchumi cha asilimia 6.3 katika mwaka 2004 na asilimia 6.5 katika mwaka 2005 msisitizo ukiwa ni kukuza kilimo, uzalishaji viwandani na mauzo ya nje hasa kupitia mpango wa *Export Processing Zones (EPZ)* na *Small and Medium Enterprises (SMES)*; na kwa kuwa

msimamizi wa mpango huu ni Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia mashirika yake ya *NDC* na *SIDO*:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza bajeti ya *NDC* ambayo ina majukumu muhimu na makubwa kama *EPZ*, *Mtwara Corridor* na uendelezaji Chuma cha Liganga na Makaa ya Mawe ya Mchuchuma badala ya *T.shs.50,000,000/=* wanazopewa kila mwaka ambazo hazilingani na kazi waliyopewa?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mbunge wa Manyoni, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba *NDC* ndio wakala (*agent*) katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa katika maeneo maalumu ya uzalishaji kwa ajili ya mauzo ya nje (*Export Processing Zones*) na miradi ya Ukanda wa Maendeleo ya Mtwara (*Mtwara Development Corridor*). Aidha, ni kweli kwamba *NDC* haipati fedha za kutosha kulinganisha na majukumu muhimu yanayotakiwa kutekelezwa na Shirika hili.

Mheshimiwa Spika, sababu kubwa ya kupewa fedha zisizotosha zinatokana na ufinyu wa bajeti. Haya hivyo, baada ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuingizwa kwenye Mpango wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini Tanzania (MKUKUTA), awamu ya pili, tunategemea kuwa kiwango cha bajeti ya Wizara kitaongezeka na moja ya maeneo yatakayopewa kipaumbele kwenye MKUKUTA chini ya Wizara ni shughuli za maendeleo na uendeshaji wa maeneo maalum ya uzalishaji kwa ajili ya mauzo nje (*Export Processing Zones*).

Mheshimiwa Spika, nje ya fedha zinazotolewa na Serikali, Miradi mingine inafadhiliwa na Mashirika ya nchi za nje. Kwa mfano, Uendelezaji wa Kanda za Maendeleo (*Development Corridors*) za *SADC* unahisaniwa na Afrika ya Kusini kupitia *SADC Spatial Development Initiatives (SDIs)* na *unit* ya Benki ya Maendeleo ya Afrika Kusini (*Development Bank of Southern Africa (DBSAI)*).

Kupitia utaratibu huo, zimetengwa fedha kiasi cha *Rand (ZAR)* 14,000,000 sawa na Dola za Marekani milioni 2.2 kwa ajili ya *Mtwara Development Corridor (MDC)* ambayo inahusisha pamoja na kuendeleza mradi wa Makaa ya Mawe ya Mchuchuma, Mradi wa Chuma Liganga na miradi mengine ya *corridor* hizo na zikiwepo *Central Development Corridor (CDC)*. Kila *Corridor* imetengewa *Rand* 7 milioni ambazo zinatumiwa kuwalipa Mameneja wa Miradi (*Project Managers*) pamoja na gharama nyingine za Ofisi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara, inatekeleza Sera ya Maendeleo ya Viwanda vidogo na Biashara ndogo ndogo ambayo inalenga kuondoa umaskini na hatimaye sekta hii kuchangia katika maendeleo ya uchumi wa Tanzania. Mikakati ya utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo (*SMEs Development Policy*) inalenga maeneo

makuu 3 ambayo ni (1) uboreshaji wa mazingira yanayohusika katika kuendeleza Sekta, (2) kuendeleza huduma za kifedha na zisizo za kifedha na (3) kujenga uwezo wa asasi husika.

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipatia nafasi hii ili niulize swali la nyongeza. Lakini pia naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa majibu mazuri. Lakini kama nilivyouliza katika swali la msingi ni kwamba Shirika la *NDC* kwa ukubwa wake na shughuli zake zilivyo kubwa na nyingi inakuwa na stahili kama vile Wizara na kwa maana hiyo hili shirika linahitaji fedha nyingi. Lakini vilevile naomba niishukuru Serikali kwamba mwaka huu imeweza kuiongeza *NDC* fedha badala ya milioni 50 wameweza kuwapa fedha nyingi kidogo. Lakini tukizingatia ukubwa na umuhimu wa kazi ambayo *NDC* inafanya na Wizara yenyewe.

**SPIKA:** Uliza swali.

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Je, Wizara itakuwa tayari kuangalia uwezekano wa kuongezea fedha Shirika hili ili liweze kutekeleza majukumu yake sawasawa badala ya kutegemea fedha za wahisani ambazo huwezi ukazichagua wala huwezi ukalazimisha kwamba uongezewe?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali imeona umuhimu wa kuongezea fedha Shirika la Maendeleo la *NDC* na ndiyo sababu katika jibu langu la msingi nimesema kwamba katika mpango wa *MKUKUTA* fedha nyingi tutazipeleka katika Shirika hili.

Mheshimiwa Spika, lakini ningependa pia kuongezea kuwa hatuwezi kutegemea fedha za Serikali katika miradi mikubwa kama ya Mchuchuma ama ya Liganga. Utafiti wa miradi hii ya *Mtwara Corridor* ni wa gharama kubwa na utekelezaji wa miradi hii pia ni mkubwa. Kwa hiyo, ndiyo sababu tunategemea nchi tatu ambazo zinahusika katika *Corridor* hii na vilevile misaada kutoka kwa wahisani.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali ndogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali kwamba Mwanza sasa tuna mipango hii ya kuinua uwekezaji na kuendeleza uchumi katika eneo letu juhudi ambazo zinafanywa katika *corridor* hizi ambazo zimetamkwa na nguvu za *NDC*. Je, pamoja na uwezo ilionao *NDC* itatusaidiaje sisi watu wa Mwanza ili tuweze pia kuwa na nafasi ya kufaidika na hilo jukumu la *EPZ*? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba Serikali haina uwezo wa kuendeleza maeneo *EPZ* kwa pamoja. Kwanza, tumeanza kuendeleza katika Mkoa wa Dar es Salaam ambapo Serikali ina mpango wa kununua maeneo mbalimbali ya *EPZ* na hatimaye tutakwenda Mkoa hadi Mkoa. Namwomba Mheshimiwa Mbunge awe

mvumilivu. Tutajitahidi vilevile Mkoa unaofuata baada ya kumaliza Dar es Salaam twende Mwanza. (Makofi)

### Na.33

#### Umeme Mbinga

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mji wa Mbinga umeingia katika Karne ya 21 ya Sayansi na Teknolojia na pia Millenium ya tatu ukiwa na giza:-

(a) Je, ni lini Mji wa Mbinga utapatiwa umeme?

(b) Je, wananchi wa Mji wa Mbinga hawana haki ya kuwa na huduma hiyo muhimu kwa ajili ya maendeleo yao?

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU (k.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati wa Madini naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Thadeus M. Luoga, Mbunge wa Mbinga Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mji wa Mbinga, kama walivyo wananchi wa maeneo mengine nchini ni wachapakazi na katika karne hii ya 21 ya Sayansi na Teknolojia wanayo haki ya kupata huduma muhimu ya umeme kwa ajili ya maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa haki ya huduma ya umeme hata hivyo unategemea sana uwezo wa fedha wa Serikali yetu. Ndio maana, pamoja na umuhimu wa umeme katika kuleta maendeleo, Serikali imelazimika kuifanya kazi ya kusambaza umeme nchini, kwa awamu, kuanzia Makao Makuu ya Mikoa, Wilaya, Majimbo maeneo ya uzalishaji na yaliyo kando kando ya njia za umeme. Aidha, Serikali limeandaa mpango kabambe wa umeme vijijini, ambao sheria yake imepitishwa na Bunge mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na jiografia ya nchi yetu, umeme wa Mji wa Mbinga unahusika sana na umeme wa Mkoa mzima wa Ruvuma, hasa Songea. Kama nilivyowahi kusema hapo awali katika Bunge hili, suluhisho la kudumu la kuupatia umeme wa uhakika Mji wa Mbinga, ni mpango wa kupeleka umeme wa gridi ya Taifa Mjini Songea kutoka Makambako. Kazi kubwa ya awali inayotakiwa kufanywa ni kujenga kituo cha kupozea umeme (*substation*) pale Makambako kutoka msongo wa 220 hadi wa 132 na baadae kutumia kituo hiki kusafirishia umeme kwenda Songea. Tayari mkandarasi wa kujenga kituo hicho cha kupozea umeme ameshapatikana na kazi ya ujenzi imeanza.

Aidha, Serikali ya Sweden imeshatoa fedha kugharimia upenguzi yakinifu. Tathmini ya mshauri itakamilika mwishoni mwa mwaka huu, 2005. Hatua itakayofuata ni kutumia taarifa ya mshauri kujenga njia ya kusafirisha umeme kutoka Makambako hadi Songea na usambazaji wa umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya, zikiwemo Mbinga na Namtumbo.

Mheshimiwa Spika, naomba kupitia Bunge lako Tukufu, kuwaarifu wananchi wa Mkoa wa Ruvuma kwa jumla na hususan Mji wa Mbinga kuwa Serikali ina nia thabiti ya kuwafikisha haraka umeme wa kuaminika kwenye Mkoa na Mji wa Mbinga.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Mpango alioutaja Mheshimiwa Waziri wa kupunguza nguvu za umeme na kuupeleka Mkoa wa Ruvuma utakamilika lini?

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU (k.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu la msingi ni kwamba upenguzi yakinifu wa mradi huu tayari umekamilika na Mkandarasi tayari ametangaza *tender* zake. Kwa hiyo, pindi taratibu hizi zitakapokamilika na mradi huu utakuwa umekamilika.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kuniruhusu niulize swali la nyongeza. Matatizo ya Mbinga yanafanana sana na matatizo yaliyo katika Jimbo la Busanda Geita na katika jibu la msingi Mheshimiwa Waziri amesema kwamba Serikali ina mpango wa kabambe wa kupeleka umeme vijijini.

Sasa napenda kufahamu katika mpango huo kabambe Serikali imezingatia ahadi ambayo imekuwa ikiieleza kwamba itapeleka umeme katika vijijini vya Rwamgasa, Katoro, Nyakagwe na maeneo ya Butundu ambayo yanatoa dhahabu nyingi na ili kuzalisha zaidi inahitaji umeme?

**SPIKA:** Kwa kweli ni swali jipya na liletwe katika njia za kawaida.

Na. 34

### **Umeme wa Makaa ya Mawe**

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi yetu imekumbwa na ukame hali iliyosababisha upungufu wa umeme na kusababisha kupanda kwa bei ya umeme; na kwa kuwa Serikali inatumia mabilioni ya fedha kulipia umeme wa *IPTL* kila mwezi na tuna umeme wa Makaa wa Mawe pale Mchuchuma:-

(a) Je, ni lini Serikali itaanza mradi wa umeme wa Mkaa wa Mawe wa Mchuchuma?

(b) Je, ni mambo gani yanayokwamisha kutotekelezwa kwa mradi huo hadi sasa?

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU (k.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini ninapenda kujibu swali namba 34 la Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mbunge wa Ole, lenye sehemu mbili kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mchuchuma ni mradi mkubwa unaohitaji kiasi cha Dola za Marekani 612 milioni kwa makadirio tuliyonayo sasa. Fedha hizo zitatumika kujenga kituo cha umeme, mgodi, kijiji ambapo wafanyakazi watakaa, barabara, njia kuu ya umeme kuunganisha Mchuchuma na gridi ya Taifa, pamoja na usambazaji ili umeme utakaozalishwa uweze kuwafikia watumiaji nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kushirikiana na wawekezaji binafsi katika kufanya tathmini za kiufundi, kiuchumi na kibiashara ili kuhakikisha gharama za mradi zinabakia chini kwa ajili ya kunusuru uchumi wa nchi yetu usiathirike, mtumiaji asishindwe kumudu gharama za umeme na kulinda Shirika letu la *TANESCO* lisifilisike kutokana na mikataba ambayo inategemewa kuingiwa kati ya wawekezaji na *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu kuhusu:- (1) ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme (*400MV*) cha Mchuchuma na (2) ujenzi wa njia ya umeme ya msongo kilovolti 330 kutoka Mchuchuma hadi Mufindi umekamilika.

Kwa hivi sasa Serikali imewaruhusu *NDC* pamoja na jopo la wawekezaji (likiongozwa na kampuni ya *Siemens* ya Afrika Kusini) kutafuta soko la umeme utakaozalishwa kwa Mkaa ya Mawe ya Mchuchuma nje na ndani ya nchi. Ujenzi wa mradi utanza baada ya wawekezaji kuridhika na soko la umeme watakalopata na kukubaliana na Serikali kuhusu uendelezaji wa mradi huo.

**MHE. STANLEY H. KOLIMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa mradi huu Kampuni ya *Siemens* na Serikali ya Tanzania waliingia mkataba ule wa *MOU* mwaka 2001 na hadi sasa hivi hatujaona matokeo yoyote. Je, Serikali inaweza kusema nini kuhusu jambo hili? (*Makofi*)

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU (k.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Spika, mradi mkubwa kama huu kama nilivyoeleza katika majibu ya swali la msingi na vilevile kama alivyojibu Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara leo hii unachukua muda. Kwa sababu lile jopo

la wawekezaji linahitaji liwekwe sawa. Pili, uzoefu wetu mikataba yenyewe ambayo tunaingia na wawekezaji lazima tuwe makini zaidi kuliko kukimbia kuingia katika Mikataba ambayo sisi tunakuwa mfilisi badala ya kupata manufaa. Kwa hiyo, namwomba tu Mheshimiwa Stanley Kolimba awe na subira na imani na Serikali yake kwamba katika mradi huu mambo yanawekwa sawa vizuri zaidi na vilevile kwa kuunganisha mambo yanatokea. Kwa mfano, jana hapa tulizindua Taarifa ya *Africa Commission* pale ambapo tutapata umakini wa ushirikiano, tutapata *Partners in Development* ambao wako makini zaidi, pale nina uhakika kabisa kwamba mradi huu utakuwa na mwanya mzuri zaidi wa kufanikiwa.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa watu wameonyesha mshangao mkubwa kwamba Serikali yetu inalipa bilioni 4 kila mwezi kuipa IPTL, lakini bado umeme ni huu wa kukatikakatika. Je, Serikali iko tayari kuleta hapa Bungeni katika kipindi hiki mkataba wa IPTL ili tuone sisi Waheshimiwa Wabunge? (*Makofi*)

**SPIKA:** Swali la msingi lilihusu Mradi wa Umeme wa Mchuchuma. Sasa hili swali la IPTL lije kwa njia za kawaida. (*Kicheko*)

Na. 35

### **Vibali vya Kuagiza Sukari toka nje**

**MHE. BENSON M. MPESYA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeamua kutoa vibali vya watu kuagiza sukari toka nchi jirani za Malawi na Zambia katika Mkoa wa Mbeya ili kupunguza tatizo la upatikanaji wa bidhaa hiyo katika maeneo hayo:-

(a) Je, ni Watanzania wangapi wa Mji wa Mbeya wamepewa vibali hivyo hadi sasa?

(b) Je, ni wafanyabiashara gani wamepewa jukumu hilo?

(c) Je, ni utaratibu gani unaofuatwa na *TRA* katika kufuatilia kodi za Serikali katika biashara hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mwilugla Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, sukari inayoingizwa nchini kutoka nchi za nje iko katika maeneo mawili: Eneo la kwanza, linahusu sukari inayoingizwa nchini na wafanyabiashara wenye viwanda na hutumiwa kama malighafi (*Industrial Raw Sugar*)



kwa ajili ya kutengeneza vinywaji na vyakula (*beverages and confectioneries*). Vibali hutolewa na Bodi ya Sukari Tanzania katika matangazo ya Serikali (*Government Notices*) na vinaonyesha majina yote ya waagizaji na kiasi walichoruhusiwa kuagiza. Inatarajiwa kwamba kiasi kinachoagizwa kitapungua kufuatia kuanza kwa uzalishaji wa sukari ya aina hii (*Industrial Raw Sugar*) na Kampuni ya Sukari ya Kilombero kuanzia Julai mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, linahusu sukari inayoingizwa kwa matumizi ya kawaida (*domestic sugar*). Uagizaji wa aina hii ya sukari hufanywa na wafanyabiashara wa jumla na reja reja ambao hupewa vibali kuingiza kiasi maalum cha sukari katika kipindi husika. Sukari hii huingizwa ili kuziba pengo ambalo hutokana na viwanda vya ndani kushindwa kukidhi mahitaji halisi ya sukari Kitaifa katika kipindi husika. Vibali vya uingizaji wa sukari ya kuziba pengo hutolewa na Bodi ya Sukari kwa kuhusisha wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na wenye viwanda vya sukari, TRA, Hazina na Chama cha Wakulima wa Miwa. Kama ilivyo katika uagizaji wa sukari ya viwandani, Bodi ya Sukari hutoa Tangazo la Serikali (*Government Notice*) ikiwataka wafanyabiashara wanaotaka kuagiza sukari kuomba vibali.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Katika kipindi cha Aprili hadi 30 Juni, 2004 vibali vilitolewa katika awamu mbili ili kuingiza jumla ya tani 39,500. Watanzania wawili kutoka Mkoa wa Mbeya walipewa vibali vya kuingiza nchini yenye jumla ya tani 4,000 za sukari kwa ajili ya matumizi ya kawaida kuziba pengo la matumizi ya sukari ya Mkoa ya Mbeya, Rukwa na Ruvuma. Waagizaji hawa ni:-

(i) *Tripple P. Investment, S.L.P 2534 Mbeya* - (tani 1,000) awamu ya kwanza

(ii) *Tecler Southern General Supplies Ltd* – tani 3,000 katika awamu ya pili.

Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2004, *Tecler Southern General Supplies Ltd*, ilikuwa imeingizwa tani 500 tu za sukari badala ya tani 3,000. Aidha, kwa mwaka 2004/2005 kampuni hizo hizo zimepewa vibali vya kuingiza jumla ya tani 1,000 za sukari kama ifuatavyo:-

*Tripple P. Investment* tani 400

*Tecler Southern Supplies Ltd* tani 600.

Hata hivyo, kama ilivyokuwa kwa mwaka 2003/2004, hadi tarehe 13/4/2005 *Tecler Southern General Supplies* ilikukwa imeingiza tani 150 tu za sukari.

(b) Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara waliopewa jukumu la kuagiza sukari kwa matumizi ya kawaida kwa mwaka 2003/2004 na mwaka 2004/2005 ni wale wanaouza bidhaa kwa jumla, reja reja na taasisi za dini. Mwaka 2003/2004 walikuwa 17 na mwaka 2004/2005 ni 18.

(c) Mheshimiwa Spika, utaratibu unaotumiwa na *TRA* katika kufuatilia kodi za Serikali katika biashara hii hauna tofauti na ufuatiliaji wa kodi katika biashara zingine. Tofauti iliyopo ni kwamba sukari huingizwa nchini na wenye vibali tu wakati bidhaa zingine huingizwa bila vibali. Muingizaji wa sukari anatakiwa atimize masharti yote ya uingizaji bidhaa nchini ikiwa ni pamoja na kulipa kodi zifuatazo:-

- Ushuru wa Forodha (*Import Duty* – 25%)
- Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) – 20%
- Kodi ya Zuio (*Suspended duty*) - 10%

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza kuhusiana na swali langu la msingi.

(a) Kwa kuwa kufanya biashara kwa kutumia vibali kunaashiria uchumi hodhi na enzi za RTC. Je, Serikali ipo tayari kulegeza masharti ili hata wafanyabiashara wadogo wadogo wapate fursa ya kuweza kuagiza sukari bila matatizo?

(b) Kwa kuwa Serikali inaruhusu wafanyabiashara kuagiza sukari ya kiasi cha shilingi 500,000/= bila malipo. Je, sasa hivi Serikali ipo tayari kuongeza angalau badala ya 500,000/= iwe 1,000,000 kama sehemu ya MKUKUTA kwa sababu biashara hii ya sukari imeajiri makundi mengi ya vijana kwa sehemu za Mwanjelwa, Mbalizi, Kiwira na kwingineko? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Benson Mpesya kwa juhudi anayofanya katika Jimbo lake la Mbeya Mjini. (*Makofi*)

Pili, Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu ambao nimeutaja katika jibu la msingi kwamba anayehusika na sekta ya sukari ni Bodi ya Sukari Tanzania.

*Tanzania Sugar Board* na hawa huwa hawatoi vibali peke yao kama nilivyosema wanashirikiana na wadau wengine kwa ajili ya kuziba pengo ambalo huwa linatokea kwa kawaida kati ya mwezi Aprili na mwezi Juni, kipindi ambacho viwanda vya sukari huwa havizalishi. Kwa sababu uamuzi huwa haufanywi na Bodi ya Sukari peke yake.

Kwa hiyo tunaamini kwamba kiasi cha sukari kinachokubalika kuingizwa hapa nchini hakivurugi soko la sukari nchini. Kwa hiyo ukiruhusu watu wote waagize sukari kama wanavyotaka basi kutakuwa na matatizo, na inaweza ikasababisha viwanda nchini vya sukari visiweze kuuza badhaa zake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wafanyabiashara kuingiza sukari 500,000 bila malipo, hilo tutaliangalia na kama kutakuwa na haja hiyo basi tutafanya hivyo. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza. Matatizo ya Mkoa wa Mbeya kuhusu uhaba wa sukari yanafanana na yale ya Mkoa wa Kagera. Sukari ni bidhaa muhimu na sasa hivi inaanza kuwa bidhaa adimu katika nchi yetu. Je kwa kuwa kiko kiwanda cha Kagera *Sugar* ambacho sasa kinazalisha sukari ya kutosha, na imekuwa kwamba kinauza sukari hii katika nchi za Kenya, Uganda na Rwanda badala ya kuisambaza nchini kama inavyoonekana kwamba nchi ina upungufu wa sukari, na kwa kuwa bei ya sukari katika Mkoa wa Kagera imekuwa ni kubwa, kiasi cha kufikia karibu shilingi 800 mpaka 1,000 kule Wilayani Ngara. Je, Serikali ina utaratibu gani wa kukifanya Kiwanda hiki kisambaze sukari nchini na hasa hasa Mkoa wa Kagera ili kutoshereza mahitaji yetu kabla ya kuuza katika nchi za nje.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, Kagera *Sugar* kuuza sukari nje ya nchi nafikiri sio kitu kibaya kwa sababu inatuingizia fedha za kigeni. Lakini pia, Kagera *Sugar* kama Wafanyabiasha ni budi na kwa kweli naamini wanafanya hivyo, wanaangalia mahitaji ya sukari yako wapi kwa jaili ya kuuza. Sidhani kama wanaacha kuuza sukari Mkoa wa Kagera kwa sababu tu wanataka wapeleke nchi jirani. Naamini kwamba kama hilo tatizo lipo basi Serikali inawaagiza wahakikishe kwamba sukari Mkoa wa Kagera inapatikana kwa wingi

Mheshimiwa Spika, tatizo kama hili linafanana na lile la Mbeya, kwa sababu hawa waagizaji ambao nimewataja katika jibu la Msingi walipewa kibali maalum kwa ajili ya kuleta sukari katika Mikoa ya Mbeya, Ruvuma na Rukwa. Kampuni zinazozalisha sukari kama Kilombelo na Mtibwa zimeshindwa kwasababu moja ama nyingine kupeleka sukari katika Mikoa ile, ndiyo maana tuliagiza walipewa vibali vya kuingiza sukari. Kwa hiyo naamini baada ya muda sio mrefu baada ya uwezo mkubwa wa Kagera *Sugar* na viwanda vingine hapa nchini tatizo hili litatatuliwa na sukari inayozalishwa hapa itaenea nchi nzima, lakini pia itaauzwa nchi za nje kwa ajili ya kuipatia nchi fedha za kigeni. *(Makofi)*.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuongezea yafuatayo:-

Katika msimu uliopita Kiwanda cha Kagera kilizalisha tani 18,000 za sukari. Makubaliano ni kwamba watauza sukari humu nchini kwanza na kiasi cha ziada ndicho watakachouza nchi za jirani. Kwa bahati nzuri nafikiri, nchi za jirani zinazotuzunguka Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi, wanaupungufu wa sukari. Kwa hiyo kuna soko zuri sana la sukari katika nchi hizo. Katika msimu unaokuja mwaka huu wanatarajia kuzalisha tani 35,000, kwa hiyo huu upungufu wa sukari unaonekana Ngara katika kipindi hiki ni upungufu wa muda mfupi san na tunatarajia kwamba utamalizika na eneo lile litakuwa na mafuriko ya sukari. Asante sana. *(Makofi)*

**WAZIWA WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, niongezee kwamba sio sawa kusema kwamba soko la sukari la Mikoa ya kusini linafanana na soko la sukari la Mikoa ya kaskazini hususani Kagera. Kiwanda cha Kagera kinalenga soko la Afrika ya Mashariki. Serikali kwa ujumla inataka kulinda viwanda vyote vya sukari vya ndani ili visiathiriwe na sukari kutoka nje. Kwa hiyo kiwanda cha kagera kinauza sukari kwa mujibu wa makubaliano yetu ya Forodha ndani ya Afrika ya Mashariki. Kiwanda cha Kilombelo ambacho ndicho kinachotakiwa kuuza sukari Mikoa ya kusini hususani kusini magharibi, kimeshindwa kufanya hivyo, kimeshindwa kabisa kufanya hivyo; na ndiyo maana kwa muda mrefu kupitia njia za panya na za halali, Mikoa ya Rukwa, Iringa kwa kiasi fulani na hasa Mbeya, wamekuwa wakitegemea sukari kutoka Zambia na Malawi.

Zambia na Malawi ni nchi za COMESA, hatuna makubaliano nazo kama tulivyo na makubaliano ya pamoja ndani ya Afrika ya Mashariki yaani Uganda na Kenya. Kwa hiyo kwa sababu hiyo biashara ya magendo ilishamili na iliendelea kushamili. Kwa hiyo ningependa kuchukuwa fulsa hii kumpongeza Mkuu wa Mkoa wa Rukwa ambaye alichukua hatua za kiutawala kuhakikisha kwamba Serikali yetu kwa sababu alijua kwamba hawezi kupambana na njia za panya, akaweka utaratibu wa wakubwa wachache kuingiza sukari na kuiuza ndani ya Mkoa wake kwa bei ya jumla. Kwa hiyo nilipokuwa Mbeya mwezi Aprili nilitoa maagizo kwamba Mkoa wa Mbeya nao uige Mkoa wa Rukwa kwa kuteuwa watu wachache wakubwa watakaouza suakri kwa jumla ili hao wadogo badala ya kupitia njia za panya waweze kununua huko na kusambaza vijijini; na kwamba hawa wakubwa wa Rukwa na Mbeya watalipa Ushuru wa Forodha ili sukari yenyewe isije ikaingiliwa. Lakini cha kufurahisha pamoja na kulipa Ushuru wa Forodha bado sukari ile ni nafuu kuliko sukari ya Kilombelo ingeuzwa Mbeya na Rukwa.

**MHE. SEMINDU PAWA:** Mheshimiwa Spika asante kwa kunipa nafasi ya muda mfupi kuuliza swali dogo tu. Tatizo sio utaratibu wa usimamizi wa sukari, tatizo ni kwa wale wanaoomba vibali. Takwimu zilizotolewa hapa inaonyesha kabisa mtu kapewa kibali tani 1,000 analeta tani 150. Sasa hii huyu amesababisha matatizo ya mapungufu ya sukari kule Mbeya, anachukuliwa hatua gani mtu kama huyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DK. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu na kama alivyosema Mheshimiwa Pawa, waliopewa vibali hawakutimiza kile kiasi walichopewa kuagiza; na tunajaribu kuwafuatilia kujuwa walikuwa na matatizo gani hasa, na kama tukiona kwamba kulikuwa na taratibu zilikosewa ama wamefanya maksudi basi aidha tutaacha kuendelea kuwapa vibali na tutawapa watu wengine ambao wanaweza kukidhi mahitaji hayo.

Na. 36

### **Kuangamiza Mazalia ya Mbu Sehemu Zinazotuama Maji Kikwajuni**

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN** aliuliza:-

Kwa kuwa, nyakati za mvua, maeneo kadhaa katika Jimbo la Kikwajuni hujaa maji hasa maeneo ya Kilimani, Gongoni, Mnazi Mmoja, Nyumba za Ujerumani,

Kikwajuni Bondeni, na Kasimajongoo; na kwa kuwa hali hiyo husababisha mazalio makubwa ya mbu ambao wanasababisha homa kali na malaria sugu:-

Je, Serikali kwa kushirikiana na Wizara husika huko Zanzibar ina mpango gani wa kumwagilia dawa kwenye maeneo hayo ili wananchi waondokane na tatizo la kuugua malaria mara kwa mara?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan Mbunge wa Kikwajuni napenda kutoa maelezo yafuatavyo:

Ni kweli nyakati za mvua, maeneo kadhaa ya Visiwa vya Unguja na Pemba ikiwemo mitaa kadhaa katika Jimbo la Kikwajuni hujaa maji na hali hiyo husababisha mazalio mengi ya mbu.

Kutokana na hali halisi ya uchumi, mazingira na hata jiografia inayoizunguka Zanzibar ni dhahiri kutokomeza maradhi haya kunahitaji fedha na mikakati madhubuti ya kisayansi na ya kijamii ikiwemo kumwagilia dawa za kuulia viluilui vya mbu, matibabu sahihi na bora, elimu ya afya na usafi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo napenda kumjibu Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan Mbunge wa Kikwajuni kama ifuatavyo:

Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Zanzibar imeelekeza nguvu zaidi za kudhibiti mbu wa malaria kwa kutumia mikakati mikubwa mitatu kama ilivyoainishwa na Shirika la Afya Ulimwenguni kama ifuatavyo:-

- Kutoa tiba sahihi kwa wagonjwa wa malaria na pia kuhamasisha jamii kuwahi kupata tiba kila wajisikiapo kuwa na dalili za ugonjwa wa malaria.
- Kujikinga na mbu wa malaria kwa kutumia vyandarua vilivyotiwa viuatilifu yaani *insecticides* na kuhamasisha jamii hasa mama wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mitano kutumia vyandarua.
- Kutoa tiba ya tahadhari yaani *Intermittent Preventive Treatment* kwa mama wajawazito ili kuzuia vifo na athari dhidi ya ugonjwa wa malaria wakati wa ujauzito.

Mheshimiwa Spika, namshauri Mheshimiwa Mbunge awasiliane na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Zanzibar kufahamu mpango uliopo wa kuangamiza mazalio ya mbu kwa kunyunyizia dawa sehemu maji yaliyotuama.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina suali moja la nyongeza. Kwa kuwa hawa mbu wako wa aina nyingi, lakini miongoni mwao ni mbu ambao wanasababisha malaria na mbu

wengine wanasababisha matende na mabusha. Sasa je, mwananchi wa kawaida atawaelewaje hao mbu ambao wanasababisha mabusha na matende? (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna mbu ambao wanaambukiza matende na mabusha wanaitwa *Qulex* na wale ambao wanaambukiza malaria wanaitwa *Anopheles*, si rahisi kwa mtu wa kawaida kutambua kwamba mbu aliyoko mbele yake ni wa aina ipi. Sasa hivi kuna hizi dawa wanazotumia katika vyandarua vilivyowekwa dawa inayoitwa NGAO, dawa hiyo inaweza kuwauwa wale *Anopheles* lakini *Qulex* wanaweza kuona kwenye dawa ile. Hiyo ni njia rahisi ya kuwatambua lakini kwa ufupi hakuna sababu ya msingi ya kumfanya mtu lazima awatambuwe kwa ufupi inatakiwa tu, wazuiliwe wote kwa ujumla.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kuniona. Suala la maji kujaa kwenye Mitaa ya Miji yetu imekuwa ni jambo la kawaida, Dar es Salaam panajaa maji, Mwanza kila mahali panajaa maji na yale maji ni machafu. Serikali haiwezi kusema tu utakuwa unangojea maji yaje ukapulizie dawa. Hiyo sio utatuzi; utatuzi ni kuhakikisha kwamba maji hayatuami katika Miji, maji yanakwenda sehemu inayotakiwa. Je, Serikali inasemaje juu ya kuweka *Sewerage System* katika miji yetu ili kuondokana na maji? (*Makofi*)

**SPIKA:** Sijui kama hilo ni la Wizara ya Afya kweli, lakini kama unamajibu yatowe Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba system nzuri ya kupitisha maji ya mvua na maji machafu itaweza kwa kiwango kikubwa kuzuia mazalia ya mbu na hivyo kupunguza ugonja wa malaria. Lakini jukumu la kuhakikisha kwamba *Sewerage System* ni nzuri ni la kila Halmashauri ya Wilaya. Kwa hivyo tunatoa wito kwa Halmashauri zote kuahakikisha kwamba wanaweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba mtiririko wa maji katika *systems* zao za kutoa maji ya mvua na maji machafu ni mzuri, na vile vile huu utaratibu mzima wa kunyunyuzia dawa katika maji, kwa kweli utaratibu huo sasa hivi haufanyiki kutokana na athari za kimazingira zilizooneka kwa kutumia *DDT* katika maeneo kama hayo. Hivi sasa dawa za kunyunyuzia zinatumiwa katika nyumba tu, tunaita *spraying* ambayo inafanyika *in-door* kwa sababu ya athari za kimazingira. Hivyo ni vyema tukahakikisha kwamba kila Halmashauri ya Wilaya inaweka vyema *Sewerage System* zao ili kuepusha maji kutuama. (*Makofi*)

Na. 37

### **Ujenzi wa Sekondari Katika Jimbo la Kondoza Kusini**

**MHE. PASCAL C. DEGERA** aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wa kata mbalimbali katika Jimbo la Kondoza Kusini hususani, Kata za Ovada, Farkwa na Mrijo wameonyesha jitihada kubwa sana katika ujenzi wa shule za Sekondari katika Kata hizo:-

- a) Je, Serikali ina habari na jitihada zilizofanywa wa wananchi hao?
- b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuunga mkono jitihada hizo?
- c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzifungua shule hizo ili nguvu za wananchi husika zisipotee bure?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MHE. ARCADEO D. NTAGAZWA) (K.n.y.WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paschal Degera, Mbunge wa Kondoza Kusini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua jitihada zinazofanywa na wananchi wote nchini wakiwemo Wananchi wa Jimbo la Kondoza Kusini katika jitihada za kujenga majengo ya shule za Msingi na Sekondari.

Aidha Serikali inawapongeza wananchi wa Kata za Ovada, Farkwa na Mrijo kwa kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge wao, kwa jitihada zao katika ujenzi wa shule za Sekondari za Kata.

- (b) Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali katika kuunga mkono jitihada hizo ni kutoa Ruzuku ya Maendeleo ya shilingi milioni 7 kwa darasa na shilingi milioni 9 kwa ujenzi wa nyumba ya Mwalimu kupitia Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES) (2004-2009).

Lengo la Kitaifa, Kimkoa na Kiwilaya ni kupeleka Sekondari asilimia 35 ya watahiniwa wa Darasa la .VII wa mwaka 2004 ikiwa ni utekelezaji wa MMES mwaka wa kwanza.

Ili kufikisha lengo hilo katika Wilaya ya Kondoza, Serikali imechangia shilingi milioni 378 ili kukamilisha ujenzi mpya wa madarasa 54 na shilingi milioni 72 myumba 8 za Walimu. Kwa hiyo jumla ya shilingi milioni 450 zimepelekwa Wilaya ya Kondoza, kati ya hizo shilingi milioni 42 ni kwa ajili ya kukamilisha madarasa 6 katika shule za Farkwa, Ovada na Mrijo.

- (c) Mheshimiwa Spika, napenda kumuarifu Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kuwa; Serikali, mwaka huu wa 2005 imefungua shule za Sekondari 6 katika Wilaya ya Kondoza ambazo ni Farkwa, Mrijo, Msakwalo, Busi, Bukulu na Ula, baada ya shule hizo kufikia vigezo muhimu vya kuwezesha shule kufunguliwa, na tunampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa mchango wake.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Napenda kwa kuanzia niipongeze sana Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa jitihada kubwa na msaada mkubwa ambao

wametupa kukamilisha majengo ya shule ambazo nimezitaja hapo. Pamoja na pongezi hizo naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

- (a) Kwa kuwa katika jibu lake, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba Wilaya ya Kondo iliahidiwa kupewa pesa za kukamilisha vyumba 54 vya madarasa; na kwa kuwa hiyo pesa hatujapata kikamilifu mpaka leo lakini katika majibu yake amesema pesa imetumwa, Je, atahakikisha kwamba atakaporudi Wizarani ahakikishe kwamba pesa zote zimefika Wilayani kwa wakati unaotakiwa ili madarasa hayo 54 yakamilike?
- (b) Kwa kuwa shule hizo nilizozitaja katika swali la msingi, zimekwisha funguliwa lakini hazina walimu na vifaa vya kufundishia; Serikali ama Wizarani ina mpango gani wa kwenda kuhakikisha kwamba walimu wanapatikana na pesa za uendeshaji wa shule hizo zinapatikana ili vifaa hasa vitabu viweze vinapatikana ili Elimu iweze kutolewa kikamilifu?

**MHE. ARCADE D. NTAGAZWA (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI):** Kuhusu swali la kwanza kwamba fedha zilizotamkwa anahisi hazijafika zote kule Wilayani Kondo na kwenye shule zinazohusika, ninakubaliana naye kwamba mara Mheshimiwa Waziri atakaporudi Wizarani na hata Wataalam wake wako hapa asubuhi hii, hili litakuwa ni jambo la kufuatiliwa ili litakiwalo litekelezwe.

Kuhusu swali la pili, kwamba ni kweli shule mpya za Sekondari zimefunguliwa na nina hakika Mheshimiwa Mbunge anakumbuka Mheshimiwa Waziri mwenyewe Waziri wa Elimu na Utamaduni amewahi kutukumbusha hapa kwamba kwa sababu wananchi wameitikia mpango wa kujenga shule za Kata, ni kweli kwamba kwa kipindi kifupi tutakuwa na tatizo la upungufu wa Walimu na vile vile tunaweza tukajikuta tunalo tatizo kwa muda mfupi la vifaa vya kufundishia. Lakini, kama Mheshimiwa Mbunge na mimi tunavyokumbuka, Mheshimiwa Waziri mwenyewe alisema tatizo hili ni la muda na Serikali inachukua hatua zifaazo zinazotakiwa ili kuondokana na tatizo hili muda si mrefu ujao.

N a. 38

### **Kushuka kwa Kiwango cha Elimu Nchini**

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi yetu ina upungufu mkubwa wa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari jambo linalopelekea taifa letu kuwa na kiwango kidogo cha elimu ikilinganishwa na kiwango cha elimu kinachotakiwa kutolewa:-

- (a) Je, Taifa letu linapoteza asilimia ngapi katika Shule za Msingi na Sekondari hapa nchini na limebakia na asilimia ngapi ya elimu inayotolewa?
- (b) Je, Serikali inasema nini juu ya hali hiyo na ni nini hatima yake?



**MHE. ARCADEO D. NTAGAZWA (k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jeremiah Mulyambate Mbunge wa Meatu lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, ubora wa kiwango cha Elimu inayotolewa unapimwa na kuonekana kwa kutumia vigezo mbalimbali vikiwemo vya; matokeo ya mitihani ya Kitaifa na Kimataifa, mhitimu kuweza kumudu mazingira na maisha yake na katika mchango wake kwa jamii.

Takwimu za matokeo ya mtihani wa Darasa la VII zinaonesha kuwa kiwango cha ubora wa Elimu ya Msingi kimekuwa kikiongezeka mwaka hadi mwaka kuanzia mwaka 1999 hadi mwaka jana kama ifuatavyo:-

- Mwaka 1999 waliofaulu walikuwa 82,419 sawa na 19.3%.
- Mwaka 2000 waliofaulu walikuwa 85,576 sawa na 22%.
- Mwaka 2001 waliofaulu walikuwa 110,633 sawa na 24.87%.
- Mwaka 2002 waliofaulu walikuwa 133,674 sawa na 27.14%.
- Mwaka 2003 waliofaulu walikuwa 196,273 sawa na 40.1%.
- Mwaka 2004 waliofaulu walikuwa 243,043 sawa na 48.7%.

Matokeo ya mtihani wa kidato cha IV katika Daraja la I-III wamekuwa wakiongezeka kama ifuatavyo:-

- Mwaka 2001 waliofaulu walikuwa 14,646 sawa na asilimia 18.3.
- Mwaka 2002 waliofaulu walikuwa 18,423 sawa na asilimia 24.62.
- Mwaka 2003 waliofaulu walikuwa 23,736 sawa na asilimia 38.09.
- Mwaka jana waliofaulu walikuwa 22,910 sawa na 38.77.

Kwa mujibu wa takwimu hizo kiwango cha Elimu hakipotei kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema bali kanazidi kuboreka. Nawapongeza Wakuu wa Shule, Walimu Wakuu Walimu na wanafunzi husika na kuboreka huko kwa matokeo.

- (b) Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa na inatekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu (*Education Sector Development programme*).

Lengo kuu la *ESDP* ni kuongeza nafasi na kuinua kiwango cha ubora wa elimu itolewayo katika ngazi zote za elimu ili iweze kufikia kiwango cha juu kulinganisha na jirani zetu na kimataifa.

Ili kufanikisha malengo ya programu hii, imeandaliwa Mipango ya Maendeleo ya miaka mitano kwa kila ngazi ya elimu inayozingatia mahitaji yote ya kuboresha na kupanua elimu ili tuwe na rika jipya ambalo wote wana elimu ya msingi na angalau

asilimia 50 wanayo elimu ya Sekondari. Huko ndiko MEM na MMES inakolenga kutufikisha.

Na. 39

### **Timu ya Mpira wa Miguu ya Wanawake**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa tatizo la kushuka na kudumaa kwa mpira wa miguu nchini liko wazi sasa; na kwa kuwa hapa nchini kwa muda mrefu mpira huo umekuwa ukichezwa na wanaume, lakini kwa sasa timu za mpira wa miguu zinazojumuisha wanawake zimekuwa zikifanya vizuri ndani na nje ya nchi:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuufanya mpira wa miguu nchini kuwa mchezo wa wanawake badala ya wanaume?
- (b) Je, ni juhudi gani zinafanywa na Serikali kukuza vipaji vya watoto wa kike hasa katika shule za msingi ili kukuza mchezo huo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Serikali haina mpango wa kufanya mpira wa miguu nchini uchezwe na wanawake badala ya wanaume kwani nia ya Serikali ni kusimamia maendeleo ya michezo kwa jinsia zote mbili kwa ufanisi kama sera ya maendeleo ya michezo nchini inavyoeleza.
- (b) Mheshimiwa Spika, katika kukuza vipaji vya watoto wa kike, Serikali inajitahidi kuhamasisha kuundwa timu ya wanawake kwa vilabu vilivyopo nchini.

Mheshimiwa Spika, vipaji vya watoto wakike katika shule za msingi vitakuzwa na Wizara husika kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri maswali madogo mawili ya nyongeza:-

Kwa kuwa, michezo si burudani tu, michezo vile vile ni ajira na kwa kuwa katika maeneo mengi ya vijijini sasa hivi, vijana wameanzisha *clubs* zao za michezo kwa vijana wa kiume na wakike ili kuweza kujiondolea tabia ya kubaki katika vijawe na kupoteza muda mwingi; Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kuweka mpango maalum wa

kutumia vilabu hivyo vya michezo kuvigeuza kuwa vikundi vya kiuchumi kwa vijana ili kuwaondolea tabia ya kukaa katika vijiwe na kuwapunguzia adha ya umaskini?

Kama Serikali iko tayari kuanza mpango huo, Je, Mheshimiwa Waziri anakubali kwamba mpango huo uanzishwe katika Majimbo yote nchini na hasa Jimbo la Bukene na Jimbo la Peramiho? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mhagama kwamba, michezo ni ajira, siyo burudani peke yake, siyo afya peke yake ni ajira. Hilo ndilo tunalolikusudia kulifanya kupitia utaratibu huu wa MKUKUTA, kwamba wale watu wenye vilabu basi wasijziuke tu na kusubiri jioni kwenda kufanya mazoezi.

Majimboni ambamo ametaja Mheshimiwa Mhagama, kutwa nzima wawe mashambani wanazalisha, kama ni wavuvi wawe wanavua, lakini inapofika jioni wanakwenda... kwa namna hiyo utakuta vilabu vinageuka kuwa vikundi vya kiuchumi. Tumeanza hivyo kwa vijiwe vya Wilaya za Temeke, Ilala na Kinondoni kama majaribio. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mhagama kwamba, Mpango huu utaendelea kwenye Majimbo yote lakini wadau wakubwa ni sisi wenyewe pamoja na Halmashauri zetu na kwa sababu Mheshimiwa Mhagama yeye mwenyewe ni mwanamichezo wa Timu ya Bunge, bila shaka jambo hili atalikazania kwa nguvu zote huko Peramiho anakosema. *(Makofi)*

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Kwa kuwa Sheria yetu ya michezo bado haijarekebishwa na kuwa michezo ni ajira; na kwa kuwa Serikali yetu ijayo itatilia mkazo ajira kwa vijana, Je, Wizara yako itakuwa tayari kufanya marekebisho ya Sheria ili michezo iwe ni kazi na ajira?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, hivi sasa katika nchi yetu hakuna anayezuiwa kuwaajiri wanamichezo. Kwa hivyo klabu ambayo iko tayari, iwe ya mpira, iwe ya ngumi, kuhama kwenye ridhaa kwenda kwenye ajira, iko huru kufanya hivyo. Lakini nataka nimhakikishie kwamba michezo katika nchi yetu itabadilika kutokana na mambo mengi, mazingira ya wadau wenyewe, lakini hata hiyo uliyozungumza kwamba Serikali ijayo itaweka mkazo kwenye suala la vijana, bila sana itasaidia vile vile kuleta mabadiliko makubwa katika michezo.

Na. 40

### **Tatizo la Wazee - Kahama**

**MHESHIMIWA RAPHAEL N. MLOLWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imekuwa ikiwahamasisha wananchi kujiunga katika vikundi maalum ili waweze kutambuliwa na kusaidia vizuri na kwamba kumekuwa na mwitikio mzuri juu ya jambo hilo; na kwa kuwa katika miaka ya 1990 ilianzishwa Taasisi isiyo ya

Kiserikali iliyojulikana kwa jina la *COEL* kwa lengo la kuwasaidia wazee wastaafu wakiwemo wale wa Jimbo la Kahama na wazee hao wamechangishwa kiasi cha shilingi 10,000/= kwa kila mmoja kwa ahadi kwamba *COEL* ingeshughulikia matatizo ya wastaafu hao lakini hakuna kilichofanyika:

Je, Serikali inawasaidiaje wazee hao kuhusiana na tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mlolwa Mbunge wa Kahama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali imekuwa ikihamasisha wananchi kujiunga katika vikundi maalum ili waweze kutambuliwa na kuhudumiwa kwa urahisi.

Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa jitihada za kulifuatilia suala hili. Wizara yangu haina taarifa za kuwepo kwa Taasisi inayojiita *COEL* kwa ajili ya kushughulikia matatizo ya wastaafu. Tunawasiliana na uongozi wa Mkoa kuhusu wahusika na *COEL* ili hatua zifaazo ziweze kuchukuliwa dhidi yao kwani tunaamini kuwa kilichofanyika ni utapeli.

**MHESHIMIWA RAPHAEL N. MLOLWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu ya kutia matumaini. Napenda kuuliza swali dogo la nyongeza.

Tunaipongeza Serikali kwa ujumla kwa kuwarudisha wazee kwenye mtandao wa Pensheni, lakini bado kuna wazee wengine ambao hawako katika mtandao huo. Je, Serikali ina mkakati gani wenye kuleta matumaini ili na wenyewe waweze kuendelea na faida katika huu uchumi unaoendelea kukua kwa kushamiri?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwa wale ambao walikuwa ni Watumishi wa Serikali, Wizara ya Fedha imejitahidi kuwarejesha katika malipo kwa wale ambao walichukua mkupuo mzima. Lakini kwa wazee wengine ambao anawazungumzia kwamba siyo waajiri lakini umri wa kuweza kujituma umekwisha, hawa wanashughulikiwa katika sera ya wazee ambayo imekamilika na sasa unaandaliwa mkakati wa kutekeleza hiyo sera. Napenda nikumbushe tena ambalo lilishazungumzwa na Waziri wa kazi hapa, kwamba sera hii hailengi tu kuhudumia ambao wameishakuwa wazee. Lakini, inatuandaa hata sisi wazee wa kesho ili uzee usituvamie. Kwa hiyo sera itakapo kuwa imeanza kutekelezwa, na tayari imeanza kutekelezwa katika baadhi ya Wizara, nia kubwa; kwanza ni kutuandaa sisi vijana tusivamiwe na uzee lakini la pili, kuona ni namna gani tunaweza kuwashughulikia ambao tayari wameisha kuwa wazee na hawakuwepo katika mpango wa Pensheni za Serikali.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha, sasa matangazo mawili; moja ni kwamba Jumamosi ya kesho haikupangiwa Semina. Haikupangiwa Semina, kwa hiyo Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi anataka kuwaarifu wajumbe wake kwamba watakwenda, kwa mwariko wa Mheshimiwa Lowassa, Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Wajumbe wote wa Kamati ya Kilimo na Ardhi watakwenda Mpwapwa hiyo kesho na gari la kuwapeleka Mpwapwa litaondoka hapa saa 1.30 asubuhi kutoka kwenye lango kuu la majengo yetu ya Bunge. Mwisho wa Matangazo.

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2004, Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2005/2006 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2005/2006**

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge orodha ya walioomba kuchangia imeshawekwa kwenye kibao chetu si lazima kwamba wataitwa katika mpangilio huo lakini angalau kutakuwa na hakika kwamba aliyeleta karatasi jina lake limewekwa kwenye orodha.

Sasa wanaokwenda kunywa chai waende kabla sijamwita mtoa hoja. Aah !!! Maana yake Mwenyekiti. Mmm!!!!!!

Sasa namwita Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi iliyochambua bajeti hii atoe maoni ya Kamati yake.

**MHE. NJELU E. M. KASAKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2005/06 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka wa 2005/06.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 43(5) (b) ya Kanuni za Bunge letu maoni haya yanatolewa. Awali ya yote napenda kumpongeza Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafisishaji Mhe. Dk. Abdallah Kigoda, (Mb) na Waziri wa Fedha Mheshimiwa Basil P. Mramba, (Mb) kwa hoja zao nzuri walizoziwasilisha mbele ya Bunge hili Tukufu, siku ya tarehe 8 Juni, 2005

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea kutoa maoni ya Kamati yangu ningependa kutumia nafasi hii kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya Wajumbe wote wa Kamati yangu kutoa pole na rambirambi kwa familia na wananchi wote wa Jimbo la Kilombero kwa msiba wa kuondokewa na Mbunge wao Mheshimiwa Abu Towegale Kiwanga.

Tunamwomba Mwenyezi Mungu ailaze mahali pema roho ya Marehemu. *(Amin)*  
Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia nafasi hii kumpongeza Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuteuliwa na CCM kuwa kugombea

Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Namtakia mafanikio katika Uchanguzi Mkuu mwezi Oktoba 2005. Ni matumaini yangu kwamba atashinda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilikutana Mjini Dar es Salaam kuanzia tarehe 23/05/2005 hadi tarehe 03/06/2005 kwa shughuli zake za kawaida. Pamoja na shughuli nyingine Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2004 na Mapendekezo ya Mpango wa Muda wa Kati na Mfumo wa Matumizi ya Serikali kwa kipindi cha 2005/06 – 2007/08; na kuhusu Sera na malengo ya bajeti kwa mwaka 2005/2006.

Katika kupitia Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa na Bajeti ilijitokeza wazi kuwa:-

- .. Uchumi umeendelea kupata mafanikio kwa *GDP* kufikia asilimia 6.7 katika mwaka 2004. Makadirio yalikuwa asilimia 6.3%.
- .. Makusanyo ya kodi kufikia wastani wa Shilingi 146 bilioni kwa mwezi.
- .. Mfumuko wa bei umeendelea kuwa chini ya asilimia 5.
- .. Kuwa na fedha za kigeni zinazokidhi mahitaji ya miezi zaidi ya saba.
- .. Mikopo ya mabanki kwa sekta binafsi imeongezeka kufikia Tsh.1,151 bilioni kulinganisha na *Tsh.965* bilioni kwa mwaka 2003/2004. Mikopo kwa sekta binafsi imepanda kutoka asilimia 85 hadi asilimia 92.
- .. Matumizi ya Serikali yamezingatia bajeti ingawa matumizi ya bajeti ya maendeleo yameongezeka.
- .. Katika kipindi hiki Serikali imeandaa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA).
- .. Kilimo kilikua kwa asilimia 6.0 mwaka 2004 kutoka asilimia 4.0 mwaka 2003.
- .. Elimu ya Msingi na Sekondari imepanuka sana.

Mheshimiwa Spika kwa mafanikio haya na mengine mengi ambayo mmeyasikia na kuyasoma katika Hotuba za Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji na Waziri wa Fedha, Kamati yangu inapongeza sana Serikali. Mafanikio kama haya hayawezi kupatikana bila ya mipango thabiti na utekelezaji imara. Kamati inashauri mipango iliyoleta mafanikio haya iimarishwe na kuboreshwa ili uchumi ukue zaidi na huduma kwa wananchi ziongezeke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inaipongeza Serikali kwa kupata mafanikio makubwa katika sekta ya ujenzi hasa barabara na mawasiliano ya simu. Aidha, marekebisho katika sekta ya fedha yamekuwa na mafanikio makubwa na ya kuridhisha.

Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa kazi iliyoanza nayo katika ujenzi wa barabara iendelee ili kujenga mazingira mazuri ya uchumi na biashara. Mtandao mzuri wa barabara ni kichocheo kikubwa kwa kuvutia wawekezaji na kukua kwa uchumi.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana yanaweza yakafanya mtu asitambue kwamba bado kuna maeneo mengi yenye matatizo na ambayo yanahitaji kuwekewa mkakati ili kupata ufumbuzi. Serikali inahitaji kuyatupia macho maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Fedha alieleza Kamati kuwa Serikali inakamilisha utaratibu wa kupeleka fedha ngazi ya Serikali za Mitaa ili zisimamiwe na Halmashauri za Vijiji, Wilaya, Manispaa na Jiji. Mpango huu ni mzuri lakini ni jambo lililo wazi kuwa Halmashauri nyingi hazina uwezo wa kumudu majukumu hayo mapya. Uwezo wa Kiutawala na Kihisibu ni mdogo. Kwa hiyo fedha zitakazopelekwa kuna uwezekano mkubwa wa ama kupotea au kutumika vibaya na hivyo kushindwa kutimiza lengo linalokusudiwa. Kamati inashauri Serikali mpango huu utekelezwe tu baada ya maandalizi ya kutosha katika maeneo ya Watumishi, Vitendea kazi na elimu ya mpango wenyewe. Aidha njia za kusimamia na kufuatia ziwe zimeandaliwa na kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, ilijitokeza wakati wa majadiliano ndani ya Kamati kuwa kumezuka wizi wa Mtandao ambao unahusisha Watumishi wa Wizara wasio waaminifu na baadhi ya Halmashauri zinazoendesha wizi huo. Katika Mtandao huo fedha kutoka Wizara kwenda kwenye Halmashauri kwa ajili ya Miradi, lakini fedha hizo hurudishwa Wizarani na Watumishi wa Halmashauri baada ya kuchukuwa sehemu yao.

Mheshimiwa Spika, Wizi huu ama huzorotesha utekelezaji wa miradi au miradi haitekelezwi kabisa na kufanya ongenzeko la mapato ya Serikali lisiwe na manufaa kwa Wananchi. Kamati inashauri kuwe na ukaguzi wa miradi ili kubaini na kuzuia mbinu hizi za wizi. Aidha, hatua kali za kiutawala na kisheria zichukuliwe kwa wahusika wanapobainika.

Mheshimiwa Spika, rushwa bado ni tatizo kubwa katika nchi yetu. Jitihada zinazofanywa na Serikali zimeongeza idadi ya Wafanyakazi wa PCB, kuingeza bajeti na kuwa na Kitengo cha Kuzuia Rushwa katika Wizara mbalimbali. Katika Mkutano wa Bunge wa mwezi Aprili 2005, Kamati ya Fedha iliombwa kuidhinisha uhamishaji wa Fedha toka Wizara ya Fedha kwenda kwenye Vitengo vya Kuzuia Rushwa vya Wizara mbalimbali. Na katika bajeti hii kuna fedha ambazo zimetengwa kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua zote hizo rushwa inazidi kushamiri hapa nchini na hasa rushwa ya kisiasa. Wananchi wengi wanaosumbuliwa na tatizo hili wanajua kuwa rushwa ipo na inaongezeka. Serikali isidanganyike kuwa tatizo limepungua, bado lipo.

Hivi karibuni kulikuwa na Semina kuhusu rushwa. Moja wa Maofisa Waandamizi wa PCB alisema rushwa iliyo ngumu kupambana nayo ni rushwa ya kisiasa kwa sababu wahusika ni vigogo na ndiyo wanaotunga na kusimamia sheria.

Kisha akapendekeza kuwa kupambana na rushwa ya aina hii kunahitajika uamuzi wa dharti wa kuwachukulia hatua wale wote wanaobainika au ambao ushahidi wa kimazingira unawahusisha. Kamati inashauri vita dhidi ya rushwa haina budi kuangaliwa upya ili kuwa na mkakati unaozingatia utawala wa sheria, uwazi na uwajibikaji mahali pa kazi. Aidha, sheria ya PCB irekebishwe ili kuipa PCB uwezo wa kumchunguza mtu yeyote na kumfikisha Mahakamani. Vinginevyo wananchi watakuwa wanagharamia taasisi ambayo haina manufaa makubwa kwao.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasoma taarifa ya maendeleo ya Benki ya Dunia ya mwaka 2005 ambayo imejielekeza katika suala la Uwekezaji. Katika eneo hilo walipoulizwa Wawekezaji kama ni vikwazo gani vinazuia Uwekezaji katika nchi mbalimbali katika eneo la rushwa Tanzania ilipata asilimia 52. Kwa hiyo inaonyesha kwamba bado tatizo ni kubwa na lipo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza Serikali kwa kuandaa makakati wa kukuza uchumi na kupunguza umasikini ambao ukitekelezwa vizuri utakuwa na matokeo mazuri pia. Aidha, Kamati inapongeza Serikali kwa kuanzisha programu kama *TASAF*, Mfuko wa Umoja, mfuko wa Udhamini wa mikopo ya Benki, na kadhalika. Hata hivyo Watanzania walio wengi ni maskini na wengi wa hao wanaishi vijijini na wanategemea hasa kilimo. Kwa mujibu wa hotuba ya Waziri wa Nchi, Mipango na Ubinafsihsaji ukurasa 25 asilimia 70 ya Watanzania wanategemea kilimo na mchango wa sekta hiyo kwa Pato la Taifa ni asilimia 48.8

Kamati inashauri kuwa njia ya haraka ya kupunguza umaskini ni kuboresha kilimo. Mapato yatokanayo na kilimo yakiongezeka yatawezesha Serikali kupanua sekta zingine na zote kwa pamoja zitasukuma mbele uchumi wa Taifa. Umaskini wa kipato utaondolewa katika muda mfupi kwa kuboresha kilimo. Sekta za madini zimeshajulikana hata Benki ya Dunia inajua hazina manufaa ya moja kwa moja na mwananchi wa kawaida na wala haiwezi kubadili maisha ya wananchi wa kawaida hata wale wanaokaa karibu na migodi yenyewe.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Fedha alipofika mbele ya Kamati ilimtaka aeleze msimamo wa Serikali kuhusu kuibadili Benki ya Rasilimali (*TIB*) na kuifanya Benki ya Maendeleo. Mtazamo wa Kamati ni kwamba Sekta za Uzalishaji katika uchumi wa Tanzania hazitapanuka kwa haraka bila ya kuwepo chombo cha kutoa mikopo ya muda wa kati na muda mrefu kwa masharti tofauti na yale yanayowekwa na Benki za Kibiashara. Na kwamba Serikali isisubiri wawekezaji binafsi kuanzisha Benki ya aina hiyo. Badala yake Serikali ndiyo iwe chimbuko la mpango huo.

Kamati inafurahi kuona kwamba Serikali imekubali kuibadili *TIB* na kuwa Benki ya Maendeleo. Waziri aliieleza Kamati kuwa maandalizi yamefikia hatua ya kuridhisha na Benki hiyo inaweza ikaanza hata kabla ya mwisho wa mwaka huu. Kamati inashauri utekelezaji wa suala hili ufanywe haraka na lisipigwe danadana. Ni vigumu sana kwa sekta za kilimo na viwanda kufanikiwa na kupanuka bila ya Mikopo ya Muda wa Kati na Muda mrefu. Aidha, si rahisi kwa Watanzania wengi hasa Wazalendo kuingia katika sekta hizo bila ya Mikopo ya aina hii. Kilimo cha mashamba



makubwa na uanzishaji viwanda kunahitaji mikopo toka Benki zilizotofauti na Benki za Kibiashara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu marekebisho ya *TIB* Kamati imepata wasiwasi kuona kuwa ingawa hotuba ya Waziri wa Fedha imetaja jambo hili katika Ibara ya 18(h), hotuba ya Waziri wa Nchi (Mipango na Ubinafsishaji) haikutaja kabisa jambo hili. Tunafikiri jambo hili ni kubwa na Waziri wa Nchi hakupaswa kulisahau. Au anataka tuamini kuwa jambo hili halijaingia katika Mipango ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, pengo kati ya riba anayolipwa mtu anayeweka fedha zake Benki yaani amana na riba anayolipa mtu anayekopa Benki, ni kubwa sana. Kwa mujibu wa takwimu za Benki Kuu (*BOT*), mtu anaeweka amana Benki hulipwa asilimia 2.5 na ile ambayo wanatia *weighed average* ni asilimia 4 na anaekopa Benki hutozwa na riba ya asilimia 15.21, tafauti ni asilimia 12.71.

Mheshimiwa Spika, ukizingatia kuwa mfumko wa bei ni asilimia 4.1. basi Mtanzania anaeweka amana Benki hakuna faida anayopata na Mabenki yaliyopo yanakopa fedha za wananchi na kuzifanyia biashara kwa gharama ndogo kabisa. Ingawa Waziri wa Fedha amesifu mafanikio ya mabadiliko katika Sekta ya Fedha, ambayo tuliyokubaliana nayo Watanzania ndiyo wanaoumia kwa mazingira ya sasa.

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ni kwamba Mabenki haya hayakopeshi kwa kiwango cha kuridhisha na ili yasipate hasara yameanzisha gharama (*charges*) nyingi kwa mtu anaeweka fedha benki na hivyo kujipatia faida kubwa bila ya jasho. Kamati inashauri Serikali ilishughulikie jambo hili ili hali hii ibadilike. Aidha, Kamati inashauri *BOT* imarishwe ili iweze kusimamia masuala haya vizuri zaidi. Benki Kuu yenyewe katika kitabu ilichokitoa juzi hapa *Monetary statement* inasema kabisa tofauti kati ya riba inayolipa kwa anayeweka amana na anayekopa kwao wamejihesabu kama ni *challenge* kubwa kwa Benki Kuu. Kweli ningependa na Serikali ilichukulie pia ni *challenge* ili liweze kurekebisha haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, katika ibara za 69 hadi 72 katika hotuba ya Waziri wa Nchi Mipango na Ubinafsishaji anazungumzia mafanikio na faida zilizotokana na ubinafsishaji, na azma ya Serikali kuendelea kubinafsisha Mashirika yaliyo salia. Kamati haina kipingamizi na mchakato wa Serikali wa kubinafsisha Mashirika na Makampuni, bali inatahadharisha kuwa kubinafsisha bandari, reli, *TANESCO*, na Maji ni suala nyeti (*sensitive*) kunahitaji uangalifu na umakini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Mashirika haya yanagusa maisha ya watu moja kwa moja na yanagusa uhai wa uchumi wa Taifa moja kwa moja. Shirika lolote katika haya haliwezi kufa peke yake, likifa na sekta nyingine nyingi tu nazo zitakufa pamoja nalo umeme, unaguza viwanda, maji yanaguza viwanda na kadhalika. Aidha usalama na ustawi wa wananchi unakuwa mashakani. Kutokana na umuhimu huo Kamati inashauri Serikali isiharakishe kubinafsisha Mashirika haya mpaka ijiridhishe kuwa mambo yatakwenda vizuri. Pia Serikali isijitoe kabisa katika umiliki wa Mashirika haya na ikibidi iingie ubia na wawekezaji wa nje. Ni vizuri Serikali ikawa na sauti

katika Mashirika ya aina hii. Yaliyotokea kwa utoaji wa huduma ya maji Dar es Salaam na Pwani yaani kwa *City Water* yatakuwa ni funzo katika kubinafsisha Mashirika yaliyobaki. *(Makofi)*

Kamati imefurahishwa na uamuzi wa Serikali kukubali ushauri wa kutojitoa kabisa katika Mashirika na Makampuni yaliyobinafsishwa na ambayo yanapata faida. Hakuna sababu ya kufanya hivyo, kwa hiyo Serikali iendelee kuwa na hisa zake na muda utakapofika wakati hali ya uchumi itakapokuwa nzuri basi hisa hizo zinaweza zikauzwa kwa Watanzania wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji ilitamka mbele ya Kamati hii kwamba azma ya Serikali ni Uchumi wa Tanzania kuwa Mikononi mwa Watanzania ifikapo mwaka 2025. Kamati imekaribisha azma hiyo ya Serikali. lakini kwa kuwa bado miaka 20 tu kuanzia sasa kufikia mwaka 2025, Kamati inaitaka Serikali iandae ramani ya utekelezaji *(Road Map)* ya azma hiyo itakayoonyesha Watanzania watapita katika njia gani hadi kufikia lengo hilo. Ramani hiyo itaonyesha vikwazo vinavyotakiwa kuondolewa na mapungufu yanayotakiwa kushughulikiwa ili lengo hilo lifikiwe bila ya hivyo itakuwa ni maneno tu.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilibaini kwamba Bajeti yetu ina utegemezi kwa misaada ya nje kwa asilimia zaidi ya 40. Na hii haijabadilika sana kutoka Bajeti ya mwaka jana na mwaka juzi. Kwa hiyo Kamati kwa kweli ina wasi wasi na hali hiyo hairidhiki na hali hiyo kuendelea kuwa katika na utegemezi huo. Tunashauri Serikali ijitahidi kubana matumizi yake na kuongeza mapato ili pengo kati ya mapato ya ndani na kutegemea misaada liendelee kupungua kwa haraka zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumalizia kwa kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri walioifanya na kwa ushirikiano wao walionipa. Kamati ililifanya kazi kwa masaa mengi na wakati mwingine nje ya saa za kawaida za kazi. Ni kutokana na moyo huo wa kujituma kwa Wajumbe, Kamati iliweza kukamilisha kazi zake.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Lephy Gembe, (Mb), Makamu Mwenyekiti kwa kunisaidia kuongoza Kamati pale nilipokuwa na udhuru. Aidha, namshukuru Bwana James Warburg, Katibu wa Kamati kwa kuihudumia Kamati vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kukushukuru wewe mwenyewe kutuongoza vizuri na kutoa fursa kwetu sisi kutekeleza majukumu yetu vizuri. Napenda pia kuwatakiwa Waheshimiwa Wabunge wote uchaguzi mwema na wenye mafanikio ili tukutane tena hapa mwezi Novemba, 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Baada ya kusema hayo napenda kutamka kuwa Kamati inaunga mkono hoja na kuliomba Bunge liipitishie.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD R. MOHAMED – MSEMAJI WA UPINZANI OFISI YA RAIS MIPANGO NA UBINAFSISHAJI NA WIZARA YA FEDHA:**

Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba upokee shukrani zetu za dhati kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Hotuba ya Bajeti, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Ubinafsishaji) na Wizara ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2005/2006 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43(5)(b)(c) toleo la 2004;

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Ubinafsishaji) Mheshimiwa Abdallah Kigoda (Mb.) na Mhe. Basil Pesambili Mramba, (Mb.), Manaibu Mawaziri na Makatibu Wakuu, na Manaibu wao pamoja na Wakuu wa Vitengo na asasi zilizo chini yao, wote tunawapongeza kwa kuratibu mipango na mwenendo wa uchumi pamoja na ukusanyaji wa mapato hadi nchi yetu kuweza kujijengea sifa ya kuwa pahala pazuri pa kuwekeza (na uvunaji) wa rasilimali mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia hadi leo hii. Pia naomba nitoe pole kwa watu waliofiwa na Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu peponi wale wenzetu waliopata na maafa.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaliia hadi leo hii tukakutana katika mkutano wetu wa mwisho wa mwaka huu na miaka mitano 2000-2005. Mwenyezi Mungu atujaalie tukutane tena katika muhula wa 2005-2010 tukiwa na Serikali zitakazoongozwa na Kambi ya Upinzani na kuwa na idadi kubwa ya Wabunge kutoka Kambi ya Upinzani. *(Makofi)(Amin)*.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nikushukuru wewe binafsi na wafanyakazi wa ofisi yako kwa mashirikiano mazuri waliyotupa Kambi ya Upinzani katika kufanikisha majukumu yetu, Mola akipenda tutakuwa pamoja tena kipindi kijacho, tukiwa upande wa Serikali kutoka Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika naomba pia niwashukuru Wabunge wote na hasa wajumbe wa Kambi ya Upinzani na wa Kamati yangu ya PAC kwa kufanya kazi kwa mashirikiano, maelewano makubwa kwa kutanguliza utaiifa wetu mbele badala ya itikadi zetuza kisiasa. *(Makofi)*

Aidha, naomba nizishukuru Serikali zote ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania na ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuipa Kamati ya PAC kila msaada katika kufanikisha mikutano miwili ya SADCOPAC ule uliofanyikia Bagamoyo (2004) na uliofanyika Zanzibar Mei, 2005 ambapo mimi nilichaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa SADCOPAC (kwa niaba ya Tanzania) kwa kipindi cha miaka mitatu (3). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shukrani za pekee zimwendee kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa kufanikisha vilivyo kazi za PAC na mkutano ndani ya SADCOPAC na hasa kwa kukubali kwake kuilea Sekretariati ya SADCOPAC. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika mwaka huu ni mwaka wa mkupuo wa tatu tokea nchi yetu iingie katika mfumo wa siasa wa vyama vingi. Chaguzi mbili zilizopita, tumeshuhudia migogoro, ambayo hatimae ilitea Taifa letu aibu kubwa, ambayo ilibadilisha historia ya nchi kuwa wapokeaji wa Wakimbizi, ikawa mzalilishaji wa Wakimbizi nchi iliokuwa ikikemea migogoro na kusuluhisha, inayosababisha vifo, Wakimbizi, vizuka na yatima. Yenye ikaua raia wake wasiopungua 35, na kuacha vizuka, mayatima na vilema ambao hadi leo hata kifuta machozi walicho ahidiwa na Rais wetu tunae muaga Benjamin William Mkapu hawajalipwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ilitegemea kuwa matokeo hayo matatu yaliyosababishwa na kutokuwa na uchaguzi ulio huru na haki, kuzalisha Wakimbizi na kuuawa kwa raia hakuto rudiwa tena, hasa pale Rais wetu alipo sema wakati akihutubia Bunge lako Tukufu kuwa yaliyotokea si mazuri ni aibu kwa Taifa letu na ni historia, “si vyema kuyarudia”.

Lakini hatuoni kuwa Rais, kama Amir Jeshi Mkuu anatembea kwenye maneno yake.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa namna raia, (mwanafunzi) alivyouawa bila hata ya hatua za kisheria kuchukuliwa.

Aidha, tumeshuhudia wakati wa uandikishaji wa daftari la kudumu huko Zanzibar watu walivyouawa, akiwemo askari wa KVZ na sio MKKM, vikosi vya Serikali visivyo na jukumu la kisheria kusimamia shughuli za uchaguzi wakisaidiwa na Jeshi la Polisi wakati mwingine (hasa Mkoa wa Mjini Magharibi) wakiwazuia raia kutumia haki yao ya kuchagua. Aidha, tumeshuhudia raia wakipigwa kunajisiwa na kupachikwa mashtaka ya bandia.

Mheshimiwa Spika, jinsi hali hii ilivyo kithiri ya uvunjwaji wa haki za binadamu ikiwa ni msingi muhimu katika kupima ubora wa utawala Naibu Mwanasheria Mkuu na Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Kiongozi Katiba Sheria na Utawala Bora Mheshimiwa Makungu alipingwa na kudhalilishwa.

Mheshimiwa Spika Waswahili wanasema: “Tumbili akimaliza miti huja mwilini”.

Mheshimiwa Spika, ikiwa Msumbiji tulioisaidia kuondoa utawala wa Wareno, raia wao hata walioko nje ya nchi wanahaki ya kupiga kura, yawaje nchi iliyokuwa na amani, utulivu wa muda mrefu nchi yetu raia wake wengine wasipate haki ya kupiga kura wakiwa ndani ya nchi yao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani haishangai na matukio haya, hasa pale Amiri Jeshi Mkuu aliposema kuwa “atahakikisha CCM inashinda hata ikilazimu kutumia vyombo vya Dola”.

Kambi ya Upinzani inaamini kuwa yanayotendwa na vikosi vya SMZ na kusimamiwa na Jeshi la Polisi ni sehemu ya utekelezaji wa tamko la Amiri Jeshi Mkuu,

hivyo Kambi ya Upinzani haioni mwanga wa kuwa na uchaguzi ulio kuwa huru na haki mwaka huu wa 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa bado ipo nafasi kwa Amiri Jeshi Mkuu, kuweka mazingira mazuri ya ushindani wa kisiasa kwa kutekeleza kikamilifu muafaka wa CCM na CUF kwamba vyombo vya ulinzi na usalama vitekeleze kazi zao bila ya kuelemea upande wowote wa kisiasa, bali wafuate sheria na taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani bado inaamini kuwa bado kuna mapungufu makubwa katika katiba yetu hasa pale inapo mpa haki raia ya kuchagua na kuchaguliwa lakini wakati huo huo imembana raia huyo huyo, kwamba ili achaguliwe lazima awe na chama cha siasa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na upungufu huo tumeshuhudia vyama vya siasa vikiwanyima raia haki ya kugombea nafasi za uongozi wa Taifa letu kwa sababu ya umri wao, (kuwa mdogo au mkubwa) rangi zao (kana kwamba waliomba wazaliwe na rangi hizo) ukubwa wa kabila anakotaka mgombea – kuwa ni tishio. Uwezo wa mgombea au jinsia anayotoka, au kuambiwa muachie mwenzio amalize muda wake.

Mheshimiwa Spika, kasoro hii inaweza kuvigawa vyama na kuviingiza katika migogoro na hatimae kuwa kichocheo cha kuvurugika amani na utilivu uliopo nchini.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ikipata ridhaa ya Watanzania kuunda Serikali itahakikisha kuwa na Katiba iliyoshirikishi na endelevu ikiruhusu kila raia kuwa na haki ya kuchagua na kuchaguliwa hata kama si mwanachama wa chama cha siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mapungufu hayo nilioyaelezea naomba kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kuwapongeza wote waliopitishwa na vyama vyao (kama hatua ya awali) kugombea nafasi mbalimbali za uongozi. Nampongeza Prof. Ibrahim Haruna Lipumba wa CUF na Maalim Seif Sharif Hamad kuwa wagombea wa urais wa Jamhuri na Serikali ya Zanzibar. Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Mheshimiwa Amani Abeid Karume wa CCM. Mheshimiwa Agostino Lyatonga Mrema na Mheshimiwa Halima Kiota wa TLP, Mheshimiwa John M.Cheyo wa UDP na wengine wote watakaopitishwa na vyama vyao kugombea nafasi hizo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya upinzani tunaomba ushindani huu usiingize nchi yetu katika vurugu, tuheshimu sheria na kanuni za uchaguzi. Vyombo vya dola, vyombo vya habari vitoe haki sawa kwa wagombea wote na Tume za yaani Wagombea wote tujue kuwa tunakokwenda sio mbali sote tutakwenda na tutaaulizwa juu ya uadhilifu wetu. Mungu Ibariki Tanzania !!!!!

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa na kigugumizi juu ya kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi, pamoja na ahadi nyingi kutolewa.

Mheshimiwa Spika, baba yangu Marehemu Rashid Mohammed Khamis(Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahala pema peponi.(Amin) mara baada ya Mapinduzi, John Okello alikuja Pemba, alimteua baba yangu kuwa Kadhi Pemba, kazi ambayo aliifanya hadi alipostaafu mwaka 1986.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka alipokuwa akifanya kazi kwa karibu na Mheshimiwa Jaji Mkuu wakati ule Mheshimiwa Ali Haji Pandu, hatimae Mheshimiwa Agustino Ramadhani, Majaji wengine akina Jaji Lipiki, Jaji Mapigano, Jaji Mfalila na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hakuna ugumu wowote hasa kutokana na uzoefu ulioko Zanzibar ambayo ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuanzisha mahakama hii. Kambi ya Upinzani, ikipata ridhaa ya Watanzania itahakikisha kuwa hili ni moja kati ya mambo yatakayokuwemo ndani ya Katiba ambayo itahakikisha kuwa utawala wa kutumia sheria zinazopitishwa na Bunge hili, ndio msingi wa utawala na wakati huo huo kulinda kanuni za utawala wa makundi mbalimbali katika jamii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, rushwa. Nimetangulia maelezo hayo, kwa sababu, Mipango yote, Bajeti yetu, msingi wake mkubwa ni amani na utulivu. Hakuna nchi yoyote duniani iliyopata nafasi ya kujenga uchumi endelevu na shirikishi kama ndani ya nchi hiyo hakuna amani, ambayo msingi wake mkuu ni tabia nzuri za raia wake na demokrasia isiyo na mizengwe. Watanzania wanayo sifa na tabia nzuri wanachohitaji ni demokrasia isiyo na mizengwe. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, wanafalsafa wote wa uchumi wanakubaliana kuwa rushwa ni kikwazo kimoja kikubwa kwa maendeleo ya nchi ambazo chumi zake ni changa kama wa kwetu. Rushwa ina makundi mawili makubwa. La kwanza, ni Rushwa ya kisiasa na ya pili ni ya mali, au tendo. Kama uongozi wa kisiasa umeingia madarakani kwa kutumia nguvu ya dola au fedha uongozi huo hauwezi kwa namna yoyote ile kupambana na rushwa, ambayo ni hii ya pili ya mali au tendo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, moja katika mambo muhimu aliyoahidi Rais Mkapa kuyashughulikia wakati alipokuwa akiomba ridhaa ya Watanzania ni vita dhidi ya rushwa. Rais Mkapa hawezi kulaumiwa kwa kushindwa na vita hivi kwani alisema mapema kuwa Ilani ya Chama chake haitekelezeki na ndio maana tunaikuta rushwa imeota mizizi ndani ya chaguzi na ndani ya Serikali hizi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi wa Serikali, taarifa za Kamati zako za Bunge ni uthibitisho tosha wa hayo niliyoelezea. Kwa mfano, kutokana na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu juu ya ununuzi wa nyumba ya Ubalozzi wetu Rome kwamba taratibu za manunuzi hazikufuatwa na baya zaidi Serikali imeshirikiana na muuza nyumba hiyo kwa kuikosesha kodi halali Serikali ya Italia pale ilipokubali kuandikiana na muuza nyumba bei ya USD 1.5 million badala ya bei halisi ya USD 3. milioni.

Mheshimiwa Spika, ushahidi mwingine, ni pale Serikali ilipoisamehe kodi *Williamson Diamond* 1994/1996 na baada ya muda huo kuisha ikashindwa kudai kodi hiyo hadi leo hii. Aidha Serikali ikauza hisa zake kwa 25% kwa *Williamson Diamond* kwa *USD 185,000*, fedha ambazo hazikulipwa *PSRC* na badala yake *PSRC* iliilipa *Williamson USD 180,000*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ushahidi mwingine ni uuzwaji wa Kiwanda cha Mgololo Iringa kwa *USD 3* million na kulipwa *USD 1* million hadi leo. Wakati Serikali imeshindwa kuonyesha kwenye Bajeti ya mwaka huu mapato yatokanayo na ubinafsishaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa *computer* 400 kwa ajili ya shule za Sekondari, bila ya kufuata utaratibu, matokeo yake zikaletwa *computer* ndani ya *ma-box* ya sabuni ambazo hadi leo hazikutumika na wanafunzi wameendelea kukosa huduma hiyo na wahusika hawakuchukuliwa hatua yeyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ushahidi mwingine ni mkataba wa TVT wa *USD 4.5* Million ambapo mzabuni, alipewa *tender* kienyeji bila hata Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kuhusishwa, akaruhusiwa kutengeneza mkataba mwenyewe ambao ulimlinda yeye tu, hadi leo ameshindwa hata kusajiliwa hapa Tanzania na hivyo ameikosesha Serikali kodi na hadi leo hajakabidhi kazi alizokabidhiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine ni ununuzi wa *Compressor Pumps* ya maji kutoka Kampuni *M/s Soft Trade Inco*. ya Canada kwa *USD 975,000*, muuzaji mbali na malipo ya *Compressor* hizo pia alilipwa gharama ya *air ticket*, *hotels* na kadhalika, Serikali ikapata hasara ya *US\$ 1,289,191.37*.

Mheshimiwa Spika, mifano ni mingi, tunachojaribu kusema Kambi ya Upinzani ni kwamba; vita dhidi ya Rushwa imeshindikana, hivyo tunawaomba Watanzania waipie Kambi ya Upinzani ridhaa yao kwa kuwapa kura kwani wao hawatakuwa viongozi waliopatikana kwa rushwa ya Kisiasa kwani Amiri Jeshi Mkuu hajawahakikishia wao kushinda kwa kutumia nguvu za dola. Pili Kambi ya Upinzani haina fedha, wala njia za siri za kupata fedha hivyo wanawategemea wapiga kura tu na wanachama wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika ninayaeleza haya kwani Kambi ya Upinzani, inaamini kuwa bila ya kupambana kwa dhati na tatizo la rushwa, hatuwezi kujenga uchumi endelevu na jamii inayoishi kwa misingi ya haki na usawa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na takwimu za ukuaji wa uchumi za asilimia 6.9 mwaka 2005 mpaka asilimia 7.9 mwaka 2007 zilizotolewa na Mawaziri wote wawili na msisitizo alioutoa Waziri wa Fedha, kuwa kwa mwenendo huu itachukua si chini ya miaka 20 kuongeza maradufu pato la wastani la wananchi kutokana na ongezeko la watu la asilimia 3%. Ni dhahiri kuwa matumaini ya Mtanzania ya kutokana na umasikini wa kipato utakuwa ndoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukweli wa kauli hii, lakini pia inadhihirisha ukomo wa uwezo wa Serikali wa kubuni njia na mbinu za kujikwama kutoka hapo, ushahidi wa hilo ni viwango vilivyobuniwa vya kupanda kwa uchumi.

Mheshimiwa, bado kilimo ndio kinachochangia asilimia kubwa katika Pato la Taifa wastani wa asilimia 49 na asilimia 66 ya mapato ya fedha za kigeni na kutoa ajira asilimia 70 ya Watanzania, ambao kiwango chao cha umasikini kimefikia asilimia 75 2004 kutoka asilimia 48, mwaka 1992 kwa lugha nyepesi kila Watanzania 100 Watanzania 75 ni masikini wa kutupwa.

Mheshimiwa Spika, naomba ikumbukwe kuwa wakati Serikali ya awamu ya tatu inaingia madarakani thamani ya Shilingi ya Tanzania ilikuwa 570 kwa Dolla leo ni 1070 na kwa kuwa urari wa biashara una naksi ya *US\$ 948.2* mwaka 2004, ni wazi kuwa uchumi wetu utaendelea kuwa ghali na umasikini kukithiri kama kilimo cha umwagiliaji maji hakikushughulikiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na tafiti zizizofanywa na asasi mbalimbali zikiwemo za Serikali na baadae Serikali ikatayarisha *National Irrigation Master Plan* inaonyesha kuwa Tanzania ina hazina ya hekta zipatazo 29.4 million zifaazo kwa kilimo cha umwagiliaji katika ngazi tofauti, ngazi hizo ni kama ifuatavyo:-

Hekta 2.3 million kwenye *High Development Potential*, hekta 4.8 million kwenye *Medium Development Potential*, hekta 22.3 million kwenye *Low Development Potential*. Mpaka sasa, Serikali inahubiri kuwa kilimo ndio uti wa mgongo kwa maendeleo ya Taifa letu, wakati inakadiriwa kutumia hekta 227,486 tu kati ya 29.4million. Kambi ya Upinzani, inaona huku nikutokuwa na mipango endelevu na kupewa kipaumbele kwa sekta hii muhimu kwa nchi yetu. Tunaamini kabisa kuwa Watanzania kwa ujumla sio maskini kama ambavyo tunalazimishwa kuamini hivyo ila kinachowafanya wawe maskini ni kushindwa kwa Serikali kuwawekea mipango endelevu.

Kwa mfano, Mpango Kamambe wa Taifa wa Kilimo cha Umwagiliaji (*National Irrigation Master Plan*), unaonyesha kuwa hekta 405,000 tu kama zikilimwa chini ya kilimo cha umwagiliaji zinaweza kuifanya nchi yetu ikajitosheleza mchele kwa ngazi ya Taifa. Kumbuka kuwa Tanzania karibu mikoa yote inalima mpunga, tafiti zinashauri kama kilimo cha umwagiliaji kikifanyika katika mikoa ya Pwani, Lindi, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Rukwa na Ruvuma basi Tanzania badala ya kuagiza mchele toka nje tutaweza kusafirisha kwenda nje.

Mheshimiwa Spika, njia za kujiondoa hapa zipo nyingi, za muda mfupi na muda mrefu, za muda mfupi ni kukubali kula nyasi, kama vile tulivyokula nyasi wakati Serikali ilipotaka kununua Ndege ya Rais. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, korosho, Tanzania tuna viwanda vya kubangua korosho visivyopungua 10, ambavyo kama Serikali ikipania sawasawa vinaweza kusafirisha korosho zilizo banguliwa, wastani wa tani 50,000, kati ya wastani wa tani 120,000



zinazozalishwa hivi sasa. Hivi sasa ni wastani wa asilimia 5% ndio inayobanguliwa na kusafirishwa.

Mheshimiwa Spika, wastani wa bei ya korosho iliyobanguliwa ni *US\$ 4200* wakati isiyobanguliwa ni *US\$ 850*. India kila mfanyabiashara anayeagiza korosho isiyobanguliwa anapewa *bonus* na Serikali kwa kuweza kuingizia Serikali mapato zaidi kwa kuviwezesha viwanda vyao kupata malighafi na tunaamini *bonus* hiyo pia hupata wale wanaozuia viwanda vyetu visifanye kazi.

Mheshimiwa Spika, hatua hii ingewaongezea kipato wakulima wa korosho, soko la uhakika na tungefaidika na kupungua kwa thamani ya shilingi yetu ambapo sasa hatufaidiki kwani urari wa kibiashara una naksi kubwa, wastani wa *US\$946.3 (17.5%)* kwa 2004 ikilinganishwa na *US\$ 880.2* mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, kama tutaweza kusafirisha wastani wa tani 50,000 zilizobanguliwa zitaweza kutuingizia wastani wa *US\$ 225* million wakati kiwango hicho hicho tukiuzua ambazo hazijabanguliwa zitaingiza *US\$ 42.5* million.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, ikipata ridhaa ya wananchi itarahisisha upatikanaji wa mikopo kwa kuwezesha viwanda na mashamba ya korosho ili:

- Katika kipindi cha miaka mitatu tuweze kusafirisha wastani wa tani 50,000 badala ya tani 5000 zinazosafirishwa sasa. Kuendelea kuwapatia mbegu za muda mfupi wakulima ili tuongeze uzalishaji kutoka tani 120,000 za sasa hadi tani 200,000 mwaka 2009.
- Kuendelea kupanua viwanda vya kutumia mazao yanayotokana na korosho ili kuongeza thamani ya mauzo kwa wakulima pale ambapo mwekezaji hakutokea, Serikali itaajiri *management* ya wazalendo wenye uwezo wa kuendesha kwa masharti karibu sawa na wanayopewa wageni.

Mheshimiwa Spika, karafuu, hivyo hivyo kwa zao la karafuu, ambapo Serikali inawakamua wananchi kwa kununua karafuu kwa nusu ya bei ya soko la dunia (*\$1500 - \$3000*).

Mheshimiwa Spika, tutahakikisha viwanda vya karafuu, makony'o vinaendelezwa na ikibidi kupanuliwa. Aidha kuruhusu karafuu kuuzwa na wananchi wenyewe kutapunguza umasikini na gharama za uendeleshaji kwa Shirika la Karafuu *ZSTC*. Aidha kutaongeza motisha kwa wakulima wa karafuu kwa kulima na kupanda mikarafuu mipya.

Mheshimiwa Spika, zao la pamba bado halijasimamiwa vya kutosha na hasa bidhaa zinazotokana na pamba kama nyuzi, mbegu na kadhalika. Kambi ya Upinzani, kwa kushirikiana na wazalishaji, wanunuzi itafanya kila liwezalo ili:-

- Kuwaongezea bei wakulima kwa kupunguza mapato yanayokwenda kwenye mamlaka ya Pamba.
- Kukaa na wenye viwanda vya nguo na nyuzi kujua matatizo yao ili yapate ufumbuzi wa kudumu kwa madhumuni ya kuongeza thamani ya mauzo.
- Pembejeo na mikopo kwa wakulima wanaolima wastani wa hekta mbili itatolewa kwa kupitia *Agricultural Bank*.(Makofi)

Mheshimiwa Spika, uvuvi na mifugo ni eneo jingine linalowapa ajira Watanzani wengi hasa wa mikoa ya kusini kati na Ukanda wa Ziwa. Hii ni idadi kubwa ya Watanzania, kama tungekuwa na mipango madhubuti endelevu, umaskini ungekuwa ndoto.

Mheshimiwa Spika, wakati watanzania wanaishi kwa wastani wa Dola moja kwa siku, bei ya samaki, kuku ni wastani wa dola mbili kwa kilo, wakati nyama ni wastani wa dola moja na nusu kwa kilo. Uhai wa Mtanzania ulikuwa mkubwa wakati nchi yetu ilikuwa na mfumuko mkubwa wa bei 32% hadi leo tuko 4% na riba kutoka 35% mpaka leo 18% hadi 22%. Sikusudii kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kusema hakuna mafanikio ila kwa Mtanzania wa kawaida, ambaye wakati mfumuko wa bei ulikuwa mkubwa anaweza kujikimu zaidi angalau milo miwili alikuwa akipata elimu kwa gharama ndogo zaidi, alikuwa na uwezekano wa kuishi angalau miaka 50, bado hata Kambi ya Upinzani iliamini kwamba mipango yetu ni endelevu na shirikishi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hivi sasa sekta ya uvuvi inaingiza pato la wastani wa *US \$9.8* million sawa na asilimia 2.5 ya Pato la Taifa, wakati Namibia wanaingiza wastani wa *USD 52* million.

Mheshimiwa Spika, Namibia wanazo (*Fish Ports na Fish Processing Plants*). Bandari za samaki na viwanda vya Kusindika samaki ambavyo vimeajiri si chini ya watu 14,000. Tanzania tuna viwanda kwenye ziwa tu wakati ukanda mzima wa bahari hakuna bandari ya samaki jambo ambalo litatukosesha, ajira kwa vijana wetu, huduma ya kuuza mafuta kwa meli zinazovua, mrahaba kwa samaki wanaovuliwa na kusafirishwa ambapo kuna wastani wa meli 140. Kila moja inavua samaki wasiopungua tani 500 kwa mwezi, sawa na MT 70,000 ambazo ni sawa na kilo 70,000,000 kwa mwezi, wanauza samaki kwa wastani wa *USD 5* kwa kilo, sawa na *USD 350* milioni kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, meli hizi zina uwezo wa kutumia *diesel* wastani wa lita 1000 meli kwa siku, 140,000 kwa meli zote kwa siku sawa na *USD 140,000,000* kwa siku. Mafuta haya kwa sababu hakuna bandari ya samaki wananunua huko huko nje (*high seas*).

Mheshimiwa Spika, samaki wanaotupwa baharini ni wastani wa asilimia 20 mpaka 30% ya samaki wanaovuliwa, kuwa wangaliweza kabisa kuteremsha bei ya samaki katika miji yetu na kupunguza ughali wa maisha, cha kushangaza zaidi ni kwamba wamiliki wa meli hizi hulipia leseni ya *USD 18,000* tu kwa mwaka hivyo kati ya

mapato wanayopata wenye meli hizi yaani dola 350 milioni na 2,520,000/= tu ndiyo Serikali inayo mipango imara, endelevu na yenye nia na kupunguza kasi ya umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pindi raia wa Tanzania wakiipa ridhaa yao Kambi ya Upinzani, itaanzisha mara moja bandari za samaki, Mtwara, Dar es Salaam, Tanga, Zanzibar (Unguja na Pemba na eneo lolote patakapokuwa na bandari inayoweza kutoa huduma hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, Kambi ya Upinzani, itaongeza kiwango cha leseni kutoka *USD 18,000* hadi laki moja kwa kuanzia kwani Somalia ambako hakuna Serikali wanatoza *USD 300,000*.

- Kambi ya Upinzani, itawalazimisha wenye meli kuwaajiri Watanzania wasiopungua asilimia 75% ya wafanyakazi wote. *(Makofi)*
- Kambi ya Upinzani, itahakikisha meli zote zinanunua mafuta, maji na huduma nyingine kwenye bandari ya samaki. *(Makofi)*
- Kambi ya Upinzani, itamuwezesha Mtanzania kuanzisha viwanda vya kusindika samaki na pia kuingia kwenye uvuvi wa bahari kuu. *(Makofi)*
- Kambi ya Upinzani, kwa kupitia *Bank* ya Kilimo itawaongezea wavuvi wadogo wadogo kupata ujuzi, ushauri juu ya masoko na mikopo.

Mheshimiwa Spika, fedha za mipango hii itatokana na Mfuko Mkuu wa Serikali, misaada mbali mbali na sehemu ya mrahaba unaotokana na samaki ambao utakuwa wastani wa asilimia 10% mpaka 15%. Mfuko maalum utanzishwa chini ya usimamizi wa Benki ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mifugo, kama nilivyotangulia kusema juu ya idadi kubwa ya mifugo iliyopo Tanzania, Kambi ya Upinzani ikipata ridhaa ya Watanzania inakusudia kufanya yafuatayo:

- Mashamba yote ya mifugo yaliyokuwa ya Serikali, kwanza watapewa wafugaji wadogo wadogo walio kubali kufuga kisasa.
- Wanafunzi wanaohitimu elimu ya mifugo watawezesha kuanzisha ufugaji wa kisasa na kuyatumia mashamba yao kueneza elimu kwa wafugaji wadogo wadogo.
- Kuendelea kuwaelimisha wafugaji wadogo wadogo umuhimu wa kubadili ufugaji wao wa kijadi kwa kuwapatia utaalamu, majosho ya kutosha na kutengwa maeneo kwa ajili ya ufugaji.

- Kupanua soko la nje la wanyama hai, hasa kondoo na mbuzi nchi za Uarabuni ambao huingiza wastani wa wanyama hawa milioni 60 kwa mwaka.
- Kurahisisha njia ya usafirishaji mifugo ili kupunguza gharama za nyama katika miji.
- Kwa kupitia Benki ya Kilimo, Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo utaanzishwa kwa madhumuni yaliotajwa hapo juu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, madini, Tanzania inawastani wa tani 20 milioni za madini ya dhahabu, hivi sasa kwa mwaka inasafirisha wastani wa 50,000 Kg yaani tani 5. Kiwango hiki ni cha migodi mitano tu mikubwa. Kwa kiwango hicho cha chini madini yanategemea kumalizika mnamo miaka ya 40 ijayo na kama migodi hiyo haitaongezea uzalishaji na mingine itafunguliwa. Lakini muda wa uhakika hautozidi miaka 25 hasa kutokana na takrima inayotolewa nchini yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kati ya makampuni matano ambayo hupitishia fedha zake Benki Kuu huonyesha kwenye vitabu vyao kuwa thamani yake ni *USD 593.2 million* Tanzania hupata mrahaba wa asilimia 3% sawa na *US\$17,790,000* na ajira ya watu 4,000 wanaolipwa wastani wa *US\$ 300* mpaka *US\$400* na hulipia umeme, maji na kutoa mchango usiozidi *US\$ 1 million* kwa huduma za jamii kama shule na vituo vya afya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupewa *Tax holiday*, pia husamehewa kodi ya mafuta ya kuendelea mitambo yao ambayo inakisiwa wastani wa lita 50,000,000 kwa mwezi. Kodi katika mafuta ni asilimia 60% ya bei ya mafuta hivyo ukichukua wastani wa bei ya *TShs.900* ni sawa na *TShs.540*. Sasa kuwasamehe lita 50,000,000 maana yake unasamehe shilingi 27 bilioni shillings.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia fedha tunayoisamehe kwenye kodi itokanayo na mafuta na mrahaba tunaokusanya maana yake sio tunatoa takrima bali tunatoa zaka maana zaka ni haki ya mpewaji na lazima utoe kama ni muumini wa kweli. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nimetangulia kusema kuwa mkulima ndiye mtu anayeonewa. Yeye hapunguziwi bei ya aina yoyote, mafuta ananunua kwa bei kubwa kuliko hata mtu wa mjini n.k. hatuna hakika kama mafuta yote haya yanakwenda kwenye mitambo, lakini cha kushangaza, ni kuwa hakuna hata mgodi mmoja aliosema unapata faida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yapo masuala ya msingi Kambi ya Upinzani haijapata majibu, pengine Serikali wanayo.

- (i) Hivi ni benki gani itakubali kutoa mkopo kwa biashara ambayo haina faida?

- (ii) Ni mwekezaji gani atawekeza kwenye miradi ambao haina faida?
- (iii) Migodi hii baada ya miaka minne mingine imeza hisa zake. Je, ni mnunujaji wa hisa gani ambaye hununua hisa kwenye biadhara isiyo na faida?
- (iv) Ikiwa mwekezaji kwenye migodi hakuna faida, kwa nini wawekezaji wanaendelea kuwekeza? (*Makofi*)

Kama Kambi ya Upinzani, itapata ridhaa ya Watanzania itasimamisha mara moja takrima na zaka inayotoa kwenye migodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kambi ya Upinzani inaamini kuwa katika *Cooperate plan* ya wawekezaji wote hawa hakuna mahali walipoonyesha kuwa watasamehewa kodi ya mafuta. Kambi ya Upinzani itapitia upya mikataba yote ya msamaha wa kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa uendelezaji wa huduma za jamii hufanywa kwa ridhaa ya wawekezaji,

- Kambi ya Upinzani itahakikisha kuwa miradi ya kijamii jirani na migodi imo ndani ya mipango ya uwekezaji ambayo itawiana na mipango ya Wilaya husika.
- Kambi ya Upinzani itahakikisha mfuko maalum wa kuendeleza wachimbaji wadogo wadogo unaanzishwa kwa kutenga sehemu ya mrahaba ambao viwango vyake vitatu na si chini ya 10% kutegemea mgodi na mgodi.
- Mamlaka ya *STAMICO* yatapewa jukumu kwa kushirikikana na *SIDO*, *VETA* kuhakikisha kunaanzishwa rika la wachimbaji wa kati ili kuwarithisha watanzania raslimali yao. (*Makofi*)
- Mheshimiwa Spika, Watanzania watawezesha kuanzisha viwanda vya kutengeneza vito badala ya kusafirisha madini ghafi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika hivi sasa *Tanzanite* baadhi ya mawe yake yanakaribia bei ya almasi au kuipita. *Tanzanite* hivi sasa inakuwa *stocked* wenzetu wanai-*stock* na siku moja itakapomalizika Tanzania ziko nchi zitatengeneza fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Spika wakati umefika kuharakisha uanzishaji wa viwanda vya vito vya almasi na *Tanzanite* ili ile amri iliyotolewa ya kuzuia usafirishaji wa *Tanzanite* ghafi uweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika maswali ni yale yale, kama Williamson hawapati faida toka 1994 ni kitu gani kinachowafanya waendeleo kuwekeza? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ikipata ridhaa ya watanania walio na uchungu na raslimali zao, itafanya uchunguzi wa kina juu ya ukwepaji wa kodi na kukoseshwa mgao Serikali pamoja na kuangalia uwezekano wa kuchukua hatua za kisheria kwa wawakezaji wa mgodi wa almasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo ambalo Tanzania lazima iliangukie ni la Elimu. Ikiwa nchi jirani zinatoa wastani wa wahitimu wa Chuo Kikuu 60,000, wakati Tanzania ni 23,000 na hao wanaomaliza bado hawana hakika ya ajira, ni dhahiri kuwa Tanzania itaifaidika kidogo mno katika ushirikiano wetu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, ikipata ridhaa ya wananchi itakahakikisha watoto wanaomaliza darasa la saba waliofaulu wataingia Kidato cha Kwanza hadi cha Nne. Aidha, itakikisha kuwa vijana wote wanaomaliza Kidato cha Sita na kufaulu wanaingia Vyuho Vikuu ama vya Serikali au hata vya binafsi kwa kushirikiana na wazazi wasiokuwa na uwezo wa kulipia watoto wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, itahakikisha kuwa nafasi zote zinazotolewa na Serikali mbalimbali (*scholarships*) zinatumiwa kikamilifu. Kwa kutumia *pre fabricated* kutaharakishwa kujenga madarasa ya shule za msingi na ya sekondari pamoja na nyumba za waalimu na maabara. Usambazaji wa *Computer* utaharakishwa ili kuhakikisha kuwa elimu kwa mtandao inaenea nchini. Usambazaji wa vitabu na vifaa vyengine utasimamiwa vya kutosha ili kuhakikisha kuwa unakwenda sambamba na ongezeko la walimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili gharama za mawasiliano ziwe rahisi, Kambi ya Upinzani itahakikisha utandikaji wa *Fiber optic* kwa kuvishirikisha vyombo mbalimbali vya mawasiliano. Aidha itataka kufahamu juu ya usambazaji wa *line* za simu zisizopungua 300,000 zilizo ahidiwa ndani ya Bunge hili. Nakumbuka Bunge liliahidiwa kwamba tutapata laini 300,000 za simu lakini badala yake Serikali ikaingia kwenye mradi wa *celtel* ya simu za mkononi ambazo ni gharama kubwa kulinganisha na simu hizi za *wire*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, itakuwa makini katika utimiaji wa rasilimali za nchi hivyo ikipata ridhaa ya wananchi, itachukuwa hatua zifuatazo:-

- Kupunguza ukubwa wa Serikali.
- Kupunguza gharama ya umeme kwa kuangalia upya mkataba wa Kampuni ya *Net Group Solution* na kuondoa kabisa ruzuku wanayopata ambayo imekwisha fikia bilioni 70, wakati bei ya Umeme inazidi kupanda. (*Makofi*)
- Kujenga asasi ya fedha kwa kushirikiana na Benki Kuu itakayotoa mikopo kwa makampuni makubwa ya madini kwa sababu Makampuni makubwa ya madini yanakopa huko nje wala hatuhakiki fedha zao na hatimaye tunaendelea kulipa deni na wao wanaondoka na mali na hatuna chochote tunachopata. Lakini

tunasema ili kudhibiti lazima tuwe na Benki ambayo ina uwezo na *TIB* nafikiri nafikiri inaweza kufanya kazi hiyo, vizuri sana kwa hiyo kambi ya Upinzani ikipata ridhaa itahakikisha Benki hiyo inaundwa mara moja.

- Kuongeza viwango vya mishahara kwa watumishi wa Serikali ili kisiwe chini ya Tshs.100,000/- kwa mwezi. Hivi sasa ukiangalia *expenditure vote* zetu utakuta mishahara wa mfanyakazi ni mdogo kuliko zile *substance allowance*. Ukiangalia vitabu vyote sasa hivi. Sisi hatuoni kwa nini *substance allowance* iwe kubwa kuliko mishahara. Tutawapa mishahara mkubwa ili tutoze kodi na ili waweze kupata *pension* ya kutosha hapo watakapostaafu. (*Makofi*)
- Kumaliza shida ya nyumba za kuishi kwa wafanyakazi na vyombo vya ulinzi katika kipindi cha miaka mitano.
- Kufanya usanifu wa miradi yote ya uwekezaji ili kujua thamani halisi na michango yao kwa Pato la Taifa. Unakumbuka katika Bunge hili tumeambiwa kila wakati tutafanya tathimini ya uwekezaji lakini mpaka leo hatujapata tathimini hiyo. (*Makofi*)
- Kuangalia mikataba ya waliouziwa nyumba na kama thamani ya nyumba zilizouzwa zinalingana ili irekebishwe.
- Kuangalia mikataba ya waliouziwa viwanda na mashirika ya umma na kupata tathimini halisi bila ya kuingiza Serikali ndani ya mgogoro wa kwenda mahakamani kama ilivyotokea kwa *IPTL* ambapo tunalipa bilioni tatu kila mwezi na sasa hivi tunasubiri *CITY WATER* watakapotupeleka Mahakamani hatujui tutalipa bilioni ngapi. (*Makofi*)
- Kuangalia mapato yanayotokana na utalii, uwindaji wa wanyamapori na ugawaji wa maeneo ya uwindaji ili kuwamilikisha Watanzania zaidi kuliko wageni. (*Makofi*)
- Kupunguza gharama za uendeshaji Serikali kwa kuweka viwango maalum vya mafuta ya magari ya Serikalini. Watakaoruhusiwa kutumia magari ya Serikali ni Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Waziri Kiongozi, Mawaziri na Manaibu wao, Spika, Naibu Spika, Viongozi wa Upinzani ndani ya Bunge na Baraza la Wawakilishi, Jaji Mkuu, Viongozi wa Ulinzi na Usalama na Makatibu Wakuu. Wengine wote watauziwa magari na watapewa *package* yao wasiisumbue tena Serikali. (*Makofi*)
- Kupunguza gharama ya viongozi kutibiwa nje ya nchi kwa kuimarisha huduma za ndani na kuagizia madaktari kutoka nje (*Flying Doctors*). Kama tungeweza kwa kufanya wagonjwa wote tukawaagizie madaktari gharama zinakuwa rahisi zaidi hivi tunavyofanya sasa, pamoja na mimi mwenyewe nimepeleka nje kutibiwa. (*Makofi*)

- Kupunguza gharama za Serikali kwa kuacha kutumia vibaya vyombo vya dola hivyo kufanya *operation* za kunyanyasa raia badala ya kushughulikia wahalifu yaani hizi *operation* zinazofanywa na Serikali wakati mwingine zina gharimu kama shilingi milioni 100 hivi.
- Kupunguza gharama za Ndege za Serikali ambazo kwa wastani ikiruka tu ndege *one hour* inatumia kama US \$ 3,000 sasa ikiruka masaa 8 utajua gharama zake ni kiasi gani. (*Makofi*)
- Kupunguza safari za viongozi kwa kuwatumia mabalozi wetu walioko nje ambao nao matumizi yao yanahitaji kuangaliwa pia.
- Kuacha kabisa kuwanunulia simu za mikononi viongozi na kuwalipia tu *US\$ 150* kwa matumizi ya kawaida. Hivi sasa wanatumia wastani wa *US\$ 1,200* kwa mwezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, unapozungumzia namna utavyokavyotumia lazima uelezee namna utakavyo kusanya mapato.

Mheshimiwa Spika, nchi nyingi masikini hazitumii vizuri mapato yake na rasilimali zake, tofauti na nchi tajiri. Katika nchi masikini ukienda ofisini kwa rafiki yako atakupa simu upige kwa familia yako bure, kwa nchi tajiri atakupa kwa gharama ulipe na mimi yalikuta hayo Ujerumani, nilikwenda kwa Waziri wa Mambo ya Ndani nikamuomba simu akaniambia hii hapa lakini at cost. Akaniambia ninyi maskini mnafanya mambo ya kitajiri na sisi matajiri tunafanya mambo ya kimaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naamini pamoja na juhudi kubwa iliyochukuliwa na Serikali katika kukusanya kodi, lakini bado kuna mwanya mkubwa wa mapato. Hivyo Kambi ya Upinzani itaongeza mapato kutokana na;-

- Kutumia mtandao kwa kununua mali za Serikali (*Electronical Procurement*) huu ni utaratibu ambao ukitaka kununua unakwenda kwenye *website* na kila mtu ana *tender* kama vile unavyokwenda kwenye mnada wa samaki. Kwa hiyo, huwezi kupata tatizo la rushwa ndani yake na unapata thamani ya bidhaa unayonunua chini kuliko ambavyo ungenunua kwa utaratibu wa *tender* wa sasa. Utaratibu huu huwa unapunguza asilimia 15 mpaka 25 ya gharama za ununuzi. Hatua hii itapunguza kwa sehemu kubwa rushwa iliyokithiri hivyo itaongeza mapato.
- Kuzitumia kikamilifu kamati za kudumu za Bunge katika kufuatilia utekelezaji wa miradi na kupata matumizi halisi.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo tumejifunza kama Kamati za Bunge zinawezeshwa vizuri zinaweza kwa ukamilifu kabisa kusimamia miradi hii na Serikali



ikapunguza gharama kwa kiwango kikubwa. Lakini kwa bahati mbaya muda wa Kamati hizi kufanya kazi ni mdogo na *resources* ni ndogo sana. (*Makofi*)

- Hatua hii inakusudia kupunguza ubadhirifu na kusukuma utekelezaji wa miradi kwa wakati, kutapunguza gharama za miradi na ufanisi, pia wahusika watapewa tunzo kwa waliofanya vizuri na kuadhibiwa kwa waliovuruga.
- Kuweka mrahaba kwenye mavuno ya Samaki kwa 10 mpaka 15% wanaovuliwa bahari kuu ambao sasa haupo. Hatua hii inakusudia kupata mapato ya moja kwa moja.
- Kuongeza mrahaba wa madini ya dhahabu kutoka asilimia 3 kwenda 10 mpaka 15%.
- Kuongeza mrahaba kwenye vito vya almasi, *Tanzanite* asilimia 10 mpaka 15%.
- Kuongeza bidii ya kukusanya mapato kutokana na maeneo yanayokusanywa sasa kwa kuziba miaya yote ya misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Spika, maslahi ya wafanyakazi wa nchini, wafanyakazi wa kada ya kati na chini wamekuwa wakati mwingi wakikopwa mishahara yao au mafao yao mengine, kwa mfano walimu, wauguzi, wapiganaji wengi hukopwa haki zao za kwenda likizo au uhamisho na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, lakini haijawahi kutokea hata siku moja mtumishi wa ngazi ya juu au kiongozi kuchelewa kupata mishahara wake au posho au marupurupu yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, ikipata ridhaa ya wananchi itakuwa ni kosa kubwa kwa asasi ya Serikali kuwakosesha watumishi haki zao zote hasa ngazi za chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimalize kuwasilisha kwa kumwomba Rais wetu mpendwa anayestaafu, kuwahakikishia Watanzania kuwa hatatumia vyombo vya dola ili kuhakikisha kuwa chama chake kinashinda kwani kufanya hivyo siyo tu kuvunja Katiba ya nchi bali ni kupora haki ya raia ya kuchagua na kuchaguliwa.

Aidha, nawaomba Wagombea wote wa Rais, Ubunge, Uwakilishi, Udiwani na kadhalika tujitahidi kufanya kampeni zetu kwa kuheshimu na kuweka maslahi ya Taifa mbele ili atakayeibuka mshindi awe mwakilishi wa Watanzania wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika mwisho, rasilimali yetu kubwa ni amani na utulivu wetu ni sawa na yai jiteta, linahitaji kulindwa na kulelewa na sisi sote. Mungu ibariki Tanzania. Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Nadhani umewasilisha Ilani ya Uchaguzi ya Upinzani. Sasa tunaanza mjadala wa jumla Waheshimiwa Wabunge, msemaji wa kwanza ni Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Lucas Seleli, jiandae na Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, jiandae.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu kuhusu hotuba hizi mbili. Ya kwanza kabisa ninaunga mkono mia kwa mia kwa hotuba zote mbili zilizowasilishwa Bungeni. *(Makofi)*

Vile vile kwa sababu nakamilisha Bajeti hii na miaka ya mitano ya uongozi wetu katika Bunge hili, naomba nitumie nafasi hii kukupongeza na kukushukuru kwa kuliongoza Bunge vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umefanya kazi vizuri na wakati tunamaliza kipindi hiki chini ya uongozi wako tutakuwa jengo la heshima inayofanana na Bunge letu. Baada ya hayo ningependa vile vile kutoa pongezi kwa Waheshimiwa Mawaziri, Waziri wa Fedha na Waziri wa Mpango na Ubinafsishaji kwa hotuba zao nzuri sana. Tunawapongeza pia Wataalam wao, Makatibu Wakuu wao na Wasaidizi wao kwa kazi nzuri walioifanya katika kipindi cha miaka mitano hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha kwa kuwa sisi baadhi yetu, mimi ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati ile, tulipoanza Waziri alitoa ahadi na ahadi moja ambayo tuliweka, tulisikia sana ilikuwa ni namna ya kusimamia vizuri mapato ya Serikali *(Financial Management)* pamoja na kutazama sehemu nzima ya Fedha ikiwemo mabanki na uwezeshaji wa Watanzania. Nataka kumpongeza na kuipongeza Serikali kwamba mambo haya yametokelezwa vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, rafiki yangu Msemaji wa Upinzani tunafahamiana ni rafiki yangu sana. Nimefurahi sana alipotamka kwamba suala la amani na utulivu ndiyo jambo la kulea kama mboni ya jicho. Nafurahi sana kama amesema hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na hii ndiyo tumefanya sisi CCM. Ndiyo tumeifikisha nchi hapo. Nchi ina utulivu na amani kutokana na uongozi bora wa Serikali ya CCM na niliona ilikuwa vizuri tu, haileti aibu kupongeza. Angepongeza halafu aseme tuendelee hivyo. Maana hapo ndipo tulipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile ukitazama hotuba ya Waziri, baadhi ya mambo ambayo Mheshimiwa ameyasema sasa hivi, yamo mle. Ila kama ulivyosema Mheshimiwa Spika, ametumia muda mwingi sana kueleza ilani yao badala ya kueleza mafanikio yanayotokana na Bajeti hii ambayo yamo wazi wazi wala huhitaji kuyatafuta, yamo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme vile vile kuwa Rais Benjamin Mkapa kwa kipindi cha miaka mitano, amefanya kazi inayoonekana, huhitaji kutafuta ili ujue amefanya kazi gani

na jana wakubwa wamemsifu. Sasa wale wenye dunia, maana hapa tumegawanyika. Kuna watu wa dunia ya tatu na dunia ya kwanza. Wale wa dunia ya kwanza wanamsifu hadharani. Hivi sisi wenyewe hatuoni? Tukimsifu tutakufa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana mafanikio ya uongozi wa Rais wetu Benjamin Mkapa ni ya wazi wazi kabisa na leo Rais wetu ni miongoni mwa marais wachache wa Afrika wenye sifa ya wazi wazi.

Mheshimiwa Spika, ukiwapanga kumi bora Afrika, yumo. Ukiwapunguza wakabaki hata watatu yumo. Sasa hii si sifa ya CCM ni sifa ya Watanzania waliopiga kura. Ameongoza nchi, hakuongoza Chama, aliongoza nchi. Kwa hiyo, hii sifa ni yetu sisi wote Watanzania pamoja na vyama vyote vya nchi hii. Kwa hiyo, ningependa tutambue na kumpongeza kwa hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile ningependa niseme rasmi kwamba mimi ni Mtanzania mwenye kukua katika siasa. Hata mtu akiniuliza na ninavyoona hivi sasa mwaka wa uchaguzi huu mwezi wa kumi Chama kitakachoongoza tena hii nchi ni CCM. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Waambie!!

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, na Rais wa nchi hii atakuwa ni yule mgombea wa CCM Ndugu Jakaya Kikwete. Watu wote wanaojua siasa wangeweza kusoma tu fikra za wananchi na kuona mtazamo, watu hawajapiga kura, lakini Rais ni Kikwete. Hawezi kuwa mwingine na anao uwezo wa kuendeleza na kusimamia sera za CCM pamoja na mafanikio ya CCM na Watanzania wengi naona watafanya hivyo tu maana itawezekana Rais mzuri anatoka halafu umpeleke Rais wa kukisikia, maana Rais anayetoka CCM ndiye atatekeleza mambo haya vizuri. Hivyo ndivyo mimi naona Watanzania wanaona. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nafurahi kusema kwamba wenye sifa hiyo ni CCM. Pia si kazi yangu kujibu. Lakini nataka nisaidie kusema mambo ambayo mimi nimeyaona. Kwa mfano, ndugu yangu ameyazungumzia habari kwamba wakiingia madarakani watagawa mashamba ya mashirika ya umma. Yale mashamba yameshagawiwa tayari. Sasa yatagawiwa mara ngapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na yameshagawiwa kwa wazalendo wa Tanzania, tena wafugaji wadogo wadogo. Sasa watagawa yapi? Wameshagawa, hivi Serikali inafanya mipango ya kuwawezsha wayaendeleze. Kwa hiyo, ni vizuri Watanzania tukasema hasa viongozi kusema mambo ambayo una hakika nayo. Mimi nasema hivi kwa sababu nina hakika nayo kwamba ndivyo Serikali imekwishafanya.

Pili, kwa mara ya kwanza Serikali hii ya Tanzania imeweka utaratibu na fedha zimewekwa za uwezeshaji kwa Watanzania wazalendo. Kazi inatekelezwa hivi sasa na mimi nataka niipongeze Benki Kuu maana ndio wanaosimamia utekelezaji wa mradi huu. Benki Kuu tunawapongeza wanafanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Benki yetu ni miongoni mwa benki za sifa katika Afrika katika kusimamia *Finacial* na kuendesha *finacial management* vizuri. Pia nataka nitoe taarifa ya mambo mazuri tu ambayo tunatakiwa kujivunia katika Afrika, nchi 48 zilifanyiwa mashindano kwa kushindanisha vyombo vyao vinavyosimamia uwekezeshaji. Kwetu hapa sisi tuna *Tanzania Investment Center* katika nchi 48 za Afrika zilichujwa zikabaki tatu, Senegal, Ghana na Tanzania. Tanzania imechukua zawadi ya kwanza kwa uwekezaji mzuri. Sasa tufanye nini, kwa nini hatutambui mambo mazuri tunasema yale ya hovyoy tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo uwekezaji ndiyo sifa, *Investment Center* yetu inaongoza kwa kuheshimiwa kwa uaminifu na uadilifu na kusimamia kazi vizuri. Kwa hiyo, nilitaka niseme hayo machache ili kusaidiana tu tuelewane tuko wapi.

Baada ya hayo Mheshimiwa Spika, nilitaka nisemee mambo yanayohusiana na kukua kwa uchumi. Mimi ningependa niseme kwamba tunapongeza kukua kwa uchumi na huwezi kuanza kuzungumza habari ya kwenda kusaidia mwanakijiji wakati uchumi wa jumla wenyewe umewekwa shaghala bagala.

Leo tunapozungumza uchumi umekua kwa asilimia 6.7 mimi Mbunge wa CCM naweza kuishauri Serikali yangu namna ya kwenda kuwawezesha watu wadogo ili kukua kwa uchumi kuende kwa mtu wa kawaida. Hayo usingeyazungumza miaka 10 iliyopita. *(Makofi)*

Kwa mfano, mimi nina mawazo yafuatayo, ya kwanza ninapendekeza kwamba Bajeti hii nina hakika itatekelezwa na awamu ya Nne ya Serikali ya CCM na baadhi yetu humu ndani tutarudi kuisaidia Serikali na mimi huwa nawaombea Wabunge wengi mrudi, maana mmeshiriki vizuri katika kuisaidia Serikali yetu. Na nyiyi mnayo sifa maalum Wabunge, mimi ni Mbunge wa muda mrefu. Lakini nataka niseme na Watanzania wasikie, Bunge hili limeweka kiwango cha juu sana cha kuelewa na kuisaidia Serikali, kwa sababu Wabunge wengi wa Bunge hili wanajali sana maslahi ya wananchi waliowachagua na mimi nawaombea wengi murudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwa sababu watakoajaza fomu wengi watakuwa ni wa CCM wasipuuze kutambua kazi yenu nzuri mliyoifanya. Tusichanganye ubinafsi na kutamani kuwa Wabunge bila kuzingatia sifa na kazi nzuri ambayo Wabunge mmeifanya. Mimi naomba niwapongeze. *(Makofi)*

Baada ya hayo nataka kusema hivi, Mkoa wa Rukwa tumejitahidi kusaidia Serikali hasa katika uzalishaji wa chakula. Mwaka jana sisi ndiyo tumeongoza, tulikuwa wa kwanza, tumeiuzia tani 31 za chakula. Hii ni historia na naipongeza Serikali pia nayo imevunja rekodi ya kununua mazao mengi ya mkulima kwa ajili ya ghala la Serikali. Nao tunawapongeza. *(Makofi)*

Lakini jambo ninalotaka kulisema hapa ni kuwa mahindi ya Sumbawanga hayatoki kuja huku kwa sababu ya *infrastructure*, barabara ni mbaya. Inatakiwa iwe ya

lami na hili ndilo jambo nasema kwa niaba ya wananchi na Wabunge wenzangu tuliomo humu kwamba tunaomba safari hii Serikali itamke lini barabara itajengwa. Itamke rasmi sasa. Kwa sababu vinginevyo sisi Wabunge wote tumejiandaa ikifika Wizara ya Ujenzi tutatoa shilingi. Kwa hiyo, tunaomba Waziri wa Fedha useme mwenyewe maana ninyi ndiyo mnaosimamia matukio, lini barabara itajengwa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mchango huu sisi wa kwanza katika Tanzania, wa pili walikuwa Dodoma, wa tatu Ruvuma wa nne Iringa kwa ziada. Sasa mnatupa zawadi gani sisi wenzenu? Na sisi tunahitaji barabara, zawadi tunaomba kwenu ni barabara ya lami ili tuongeze zaidi marudufu. Nitatoa mfano mdogo tu, kwa mfano, kuna lugha inayosema kipi kianze yai au kuku?

Sasa Mkoani kwetu pamoja na matatizo yote haya kiwanda cha kusindika nyama kinajengwa. Kitachinja zaidi ya ng'ombe 34,000 na zaidi ya 17,000 mbuzi. Lakini hakuna barabara ya lami. Kwa hiyo, tunaomba Serikali ilifikirie jambo hili.

Mheshimiwa Spika, halafu vile vile ningependa nisemee kwamba mwaka huu wakulima hawa hawa walipata mahitaji ya mbolea katika Mkoa wetu ni tani 26,000 tulipata tani za mbolea 800 tu. Tani 800 za mbolea unalinganisha vipi na mahitaji ya tani 26,000 kwa hiyo, tunaomba jambo hili litazamwe. Kwa sababu linaanza kuwa kero, uamuzi wa Serikali wa kutoa ruzuku tunaukubali na tunashukuru sana imeonyesha imesaidia lakini bado.

Mheshimiwa Spika, ningependa kusesitiza kwamba fedha zinazotolewa kwenye kilimo sasa ziende kwenye miradi. Tuijue miradi yenyewe, kwa mfano tungeweza tukajenga miradi ya umwagiliaji mikubwa siyo hii midogo midogo ya hekta 200 au 300 hapana. Miradi mikubwa, mizuri ambayo mnaweza mkawagawia wananchi wadogo kulima kwa umwagiliaji maji. Kwa mfano, kama hizi bilioni 50 mpaka mwisho wa mwaka unaisha inawezekena tusione kitu chochote cha maana katika jambo hili.

Kwa hiyo, sisi tunashauri kuweko na miradi na nataka pia niipongeze Wizara kwa sababu wenzako wakifanya jambo zuri unafurahi. Kule kwetu tuna Mto mkubwa sana wa Momba, tuliomba Wizara na kweli wamepeleka wataalam wameanza kazi ya kutafiti umwagiliaji. Kwa hiyo, tunashauri miradi halafu vile vile suala la usindikaji wa mazao. Mimi natoa ushauri kwamba ingekuwa vizuri tuamue kabisa na tuweke mipango kuna suala la sera na suala la mipango na programu za utekelezaji.

**WABUNGE FULANI:** Sawa!!

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mimi nasema bado Mikoa yetu, Mikoa mingi bado ni utawala tunaita *Ceremonial Leadership* kila mtu amelala anafikiri mwenyewe atakachofanya. Sasa lazima nchi iwe na mipango ambayo wahusika watawajibika. Nasema kama ni kulima tuweke malengo. Mkuu wangu wa Mkoa ana malengo alijua hili. Sasa tunataka kulima alizeti, tunataka kulima michikichi. Vyote hivi vinatakiwa viwe na mipango na malengo.

Mheshimiwa Spika, ni bahati mbaya, duniani kama jana ulipokuwa unamtambulisha yule, duniani kwa wenzetu unaposimama kusema mambo makubwa, useme wewe mwenye kama ni mfano. Maana huwezi kusema jambo na wewe siyo mfano. Nilipokuwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, tulifanya utafiti wa nchi nzima, tukagundua kwamba ardhi ya kulima michikichi ya Tanzania ina eneo kubwa kuliko Malaysia na Waziri Mkuu wa Malaysia mimi nimekwenda mara mbili kule na alipokuja mimi nilialikwa na sikuja kuhudhuria kikao.

Mheshimiwa Spika, akasema hatutoi mbegu ya michikichi ya Malaysia lakini kwa Tanzania tutatoa. Wakati ule mpaka mimi naondoka niliacha zaidi ya hekta 4,000 tumelima michikichi. Lakini ule mradi haukuendelea mpaka leo. Nilikuwa naagiza mbegu ya kupanda kutoka Ivory Coast na Costa Rica inakuja kwa ndege mpaka Dar es Salaam inakwenda Kigoma, mradi ule ulikwisha kufa na Wizara wana *research* nyingi tu juu ya michikichi imekaliwa. Sasa *seriousness* yetu hapo iko wapi. Leo Malaysia kwa michikichi peke yake wanapata na kuingiza bilioni 4 kwa mwaka, fedha za kigeni. Lakini sisi tumekalia ardhi tunaiangalia hivi hivi.

**WABUNGE FULANI:** Waeleze!!

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Soya kwa mfano, soya ni chakula duniani. Soya haina *cholesterol*, alizeti haina *cholesterol*. Haya ni mazao ambayo tungeyawekea mipango na tungefanikiwa tu. Baada ya hayo ningependa kumalizia kwa kusema mambo mawili ya kumalizia. La kwanza, ningeomba vile vile katika mpango huu tufikirie mambo mawili kwamba tunaposema teknolojia. Tuna *transfer of technology* tuna maana gani. Kwa sababu leo ukiuliza Wizara ya Sayansi na Teknolojia utaona wana vyo vya kawaida, kusomesha watu wa kuja kufanya kazi za utawala.

Mheshimiwa Spika, lakini mimi nasema *transfer of technology* ni kuamua, mnasema sisi tunataka tupeleke mainjina au ma-*scientist* au *researchers* kadhaa Ujerumani au Japan au wapi ili hawa wakirudi waje kuwa wagunduzi wenu. Sisi bado tunasomesha ile kawaida tu na vile vile tunapozungumza ku-*transfer* kuhamisha teknolojia ambayo inafanana na mazingira yetu lazima tuulize hawa wanaokuja kuwekeza na kujenga viwanda baadaye wakiondoka itakuwaje. Kwa hiyo, hiyo ningependa niseme.

Mheshimiwa Spika, la mwisho nieleze vile vile kwamba wenzetu wanapotoa takwimu wawe consistence kwa mfano kwenye hii Taarifa ya Hali ya Uchumi, taarifa zinagongana, kwanza mazao hayakuongezeka yameshuka. Mazao ya nchi yetu ya kuleta faida kwa mfano kahawa, pamba yameshuka, hayakuongezeka. Maana yake ni kwamba hatujakwenda mbele. Lakini vile vile kwenye takwimu hizi kwa mfano utaona korosho wametoa takwimu mbili, kwenye korosho yenyewe inaonyesha 92 lakini upande huu mwingine ndani ya kitabu hicho hicho inaonyesha tena korosho 95, kitabu hicho hicho, kwenye *summary* ni 92 kwenye korosho yenyewe 98. Nyingine 78, kwenye kitabu hicho hicho inaonyesha 79.

Mimi naona tatizo, kwa hiyo, nashauri wataalam wetu mjitahidi kuwa waangalifu mnapotoa takwimu. Baada ya hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, asante sana na kwa kweli napenda niunge mkono kabla sijaenda mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Bwana Spika, kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Nzega na mimi mwenyewe ningeanza kutoa salam za rambirambi kwa kifo cha Mbunge mwenzetu aliyetutoka hivi karibuni Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mbunge wa Kilombero. Mwenyezi Mungu ailaze mahali pema roho yake peponi.

Lakini la pili, napenda kuwapongeza sana wagombea wetu wa Urais kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Mheshimiwa Aman Abeid Karume kwa upande wa Zanzibar na Mgombea Mwenza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein. Naamini Mwenyezi Mungu atawajalia na kwa kampeni tuliyonayo naamini CCM itashinda bila tatizo lolote. *(Makofi)*

La tatu Mheshimiwa Spika, napenda kuwatakia kheri Wabunge wote wa Chama Cha Mapinduzi katika mchakato ulioko mbele yetu hasa mwezi wa nane, kwa kawaida ya Bunge huwa linaondoka nusu wanakuja nusu. Mimi naamini mwaka huu itakuwa tofauti wataondoka robo watakuja robo tatu. Mungu atawajalia.

Baada ya hapo Mheshimiwa Spika, la nne nipende kwa kweli kuwapongeza Mawaziri wote wawili, Waziri wa Mipango pamoja na Waziri wa Fedha. Lakini vile vile kwa sababu wao hawafanyi kazi peke yao, napenda kuwapongeza watumishi wote wa Serikali, Makatibu Wakuu wote, Wakurugenzi, Makamishna wa Wizara zote mbili kwa kazi kubwa ambayo wameifanya. Sisi tulioingia tangu mwaka 1995 tofauti tunaiona. Wenzetu walioingia juzi mwaka 2000 na hasa wapinzani hawawezi kuona tofauti ya mabadiliko yaliyopo kwenye bajeti hii na vile ambavyo tulivyotoka miaka 10 iliyopita.

Lakini mimi ningependa kuwakumbusha tu kwamba mwaka 1996 na leo ni tofauti iliyo wazi, mambo yanaonekana, labda tu kwa sababu wenzetu wamechanjia ubishi basi hawawezi kusema zaidi ya kubisha na kukataa lakini Mwenyezi Mungu anawaona na anaandika na hawawezi kushinda hasilani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia mwaka 2001 Bajeti yetu ilikuwa shilingi trilioni 2.2, mwaka 2002 ilikuwa trilioni 2.7. Mwaka 2005 tunazungumza trilioni 4.1. Sasa anayesema anaongeza mapato zaidi ya Chama Cha Mapinduzi ataongeza kupitia wapi? *(Makofi)*

Naomba ndugu zangu katika hili na napenda nitoe mwito kwa Watanzania wote mambo ambayo Chama Cha Mapinduzi kimefanya kwa upande wa elimu hatukuwa na MEM, hatukuwa MMES. Leo tuna *terminology* hizo. Kwa upande wa barabara sisi upande wa kule kwetu hatukuwa na barabara kabisa ya lami. Lakini leo tunaona kuna barabara na inajengwa, upande wa Maji, upande wa Afya na Kilimo na sasa tunaanza MKUKUTA kitu ambacho kitawakomboa Watanzania wengi. Kwa hiyo, kila ambavyo

kuna mafanikio lazima matatizo yapo. Lakini mwenye kutatua matatizo ni yule ambaye ameanzisha na anajua na ana dira na ana mwelekeo mzuri. Kwa hiyo, natoa mwito kwa Watanzania wote waendeleo kuichagua CCM hata katika uchaguzi ujao wa 2005. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, leo nitakuwa na maneno machache sana na nilikuwa na ushauri katika kuboresha Bajeti hii ambayo kwa kweli ni nzuri, kwanza Bajeti hii imeonyesha kuna ukuaji wa uchumi ambao umefikia asilimia 6.7 na katika hili nilikuwa napenda kutoa ushauri tu kwamba ukuaji wa uchumi huu uandamane na ufanane na ukuaji wa uchumi hasa kwa mwananchi wa kawaida.

Ninapozungumza mwananchi wa kawaida hapo unamgusa mkulima, kwa sababu lazima tumwezeshe mwananchi wa kawaida kukuza uchumi, kukuza pato lake na hata ile nguvu ya manunuzi *purchasing power* awe nayo aweze kufaidi matunda katika uchumi ambao Serikali imekuza na katika hili vile vile nilikuwa napenda kushauri kwamba ukuaji wa uchumi wa asilimia 6.7 uwende sambamba vile vile na uimara wa shilingi yetu.

Mheshimiwa Spika, shilingi yetu bado inazidi kuporomoka, ukiangalia tulianza na shilingi 570, sasa hivi iko 1000 na zaidi. Kwa hiyo, inazidi kuporomoka. Kwa hiyo, Serikali ione namna gani inadhibiti uporomokaji wa shilingi yetu ili tuweze kuwa tunakuwa haraka zaidi. Ningependa dhamira kubwa kwa sasa ilenge katika kuhakikisha na kuweka hatua za makusudi kwa ajili ya kuinua pato la mwananchi na hasa mkulima. Nilikuwa nashauri kwa sababu zaidi ya 80 ni wakulima tena ni wakulima na wafugaji.

Watanzaia walio wengi ni wakulima na wenzetu nchi zilizoendelea nchi za Ulaya zinatoa hata ruzuku kwa wakulima wao wanapokuwa wamelima wanapewa ruzuku. Nadhani sasa hivi ziwekwe hatua za makusudi za makusudi kabisa katika utoaji wa ruzuku, katika bajeti ya mwaka jana Serikali iliamua kutoa ruzuku ya mbolea na hii naipongeza, lakini nilikuwa nadhani iboreshwe zaidi ili mbolea iweze kuwafikia wengi kwa bei rahisi na kwa wakati muafaka.

Kwa hiyo, utoaji wa ruzuku hasa kwenye mbolea na dawa, ninapozungumzia dawa na hasa wafugaji, wengi wanafuga lakini hawawezi kumudu kuogesha mifugo yao. Kwa hiyo, mbolea na dawa, kwa sababu mkulima anapopata chakula akiba yake ya kwanza ni kununua ng'ombe, ndiyo akiba yake ya kwanza. Kwa hiyo, tuweke utaratibu wa makusudi kuhakikisha mbolea linawafikia kwa bei ya rahisi zaidi, lakini madawa vile vile yanakuwa kwa bei rahisi zaidi.

La pili, katika ushauri wangu nilikuwa nashauri suala la umwagiliaji maji. Tunazo *scheme* mbalimbali ambazo Serikali imeanzisha na hapa napenda kuwapongeza, wamefanya vizuri lakini bado hatuna malambo, kama hatuna malamb maana yake hizi *scheme* zote inapotokea ukame kidogo tu *scheme* zote haziwezi kufanya kazi kwa sababu hakuna maji ambayo yamevunwa kwa ajili ya kumwagilia na bado Watanzania wakulima walio wengi wanaangalia wingu. Tufike mahali ambapo sasa tusitegemee wingu hali ikikataa basi unajua kwamba tutamwagilia tutapata chakula cha kutosha kwa kuwa na malambo na *scheme* kubwa kubwa na ndogo kwa ajili ya umwagiliaji maji.



La tatu, nilikuwa napendekeza uharakishwe mpango wa kuanzisha Benki ya Maendeleo ambayo itawapa nafasi wakulima, itawapa nafasi sekta isiyo rasmi, wafanya biashara wadogo wadogo wapate mahali pa kukopa. Kwa sababu wafanya biashara wadogo wadogo, wakulima katika sekta hii ya benki zilizopo hawana nafasi kwa sababu hawaaminiki. Ni wajibu wa Serikali kuanzisha benki ya maendeleo itakayowalenga wakulima na wafanya biashara wadogo wadogo sekta isiyo rasmi kupata mahali ambako watapata mitaji yao na kujikopesha kwa ajili ya kuinua kipato chao.

Hili lingine nilikuwa nashauri vile vile tuweke mlengo wa kuondosha jembe la mkono. Miaka mingi tumekuwa na jembe la mkono, ni kizazi kimepita kirefu, kwa hiyo ziwekwe hatua za makusudi kama tunadhamiria kupigana vita na umaskini, kama tunataka kukusudia kuondosha umaskini lazima tukusudie kuondosha jembe la mkono kwa sababu jembe la mkono linatucheleweshwa na halina tija.

Kwa hiyo, nilikuwa napenda kushauri jembe la mkono tulipige vita kama ambavyo tunapiga vita na tuanzishe makusudi kabisa kuhakikisha familia zetu zinatimia majembe ya kukokotwa na mifugo na zile ambazo zitakuwa na uwezo ziweze kuwezesha kupata matrekta madogo madogo kwa ajili ya kilimo cha haraka. *(Makofi)*

Vile vile nilikuwa napendekeza soko la mazao liwe la uhakika na katika hilo soko la mazao kwa sababu liwe la uhakika napenda kuungana mkono kabisa na juhudi za Serikali za sasa kuhakikisha zinatengeneza miundombinu ya barabara kupeleka mazao ambapo yanalimwa lakini lazima tuweke mkazo hata kwa mazao ambayo siyo ya asilia. Mazao madogo madogo, *publica* vitu vya namna hiyo, viweze kupata masoko kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tutakwenda kupata mazao ya uhakika.

Pia naipongeza Serikali kwa kuanzisha mpango wa kuinua uchumi na kuondoa umaskini kwa kifupi MKUKUTA. Nilikuwa na ushauri ufuatao, kwa sababu tumedhamiria kuanzisha mkakati huu kuinua uchumi, nilikuwa naungana mkono kwamba kweli tumetenga asilimia 50 katika Bajeti ya mwaka 2005/2006 lakini nilikuwa nataka mkazo mkubwa uwekwe kwenye sekta ya Kilimo kwa sababu ukiweka kwenye Sekta ya Kilimo utaweza kupambana na umaskini na kuinua hali ya wakulima walio wengi na ndiyo wananchi walio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile hapo maeneo ya Sekta ndodo ndogo zingine kwa mfano sekta ya wachimbaji wadogo wadogo haa nao tukiwaingiza katika MKUKUTA tutaweza kuwapatia vifaa, mitaji na hasa kuwapa hisa katika makampuni yatakayokuja kufungua basi wapate hisa ili waweze kuwa wabia katika makampuni hayo. Vile vile tuwatafutie soko la uhakika sasa hivi huwezi kuona wapi wanauza dhahabu, wapi wanauza almasi zao na wapi wanauza tanzanite huo ulikuwa ni ushauri wangu wa pili.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa tatu nilikuwa napenda kushauri kwamba mgawanyo wa fedha katika Kanda ningependa uweze kulingana. Ukiangalia Kanda zetu

hizi zimegawanyika katika maeneo mbalimbali. Lakini sijui ni kitu gani ambayo Serikali inatumia kugawa fedha hizi na ni *criteria* gani ambayo inatumia kuzigawa.

Mheshimiwa Spika, Mikoa ya pembezoni ambayo haipati fedha za nje inasahaulika kabisa katika kupewa pesa za ndani nyingi. Ukiangalia katika kitabu cha Mipango ukurasa wa 15 Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2005/2006 kilichotolewa na Ofisi ya Rais, Mipango, Mikoa ya Tabora, Rukwa, Arusha na Kigoma yenyewe haina kabisa fedha za nje.

Lakini ukiangalia mikoa kama Shinyanga, Singida inafedha kidogo sana za nje. Kwa mfano mkoa Tabora unafedha shilingi milioni 946 ya ndani na wastani wa pale ni milioni moja na laki saba ya watu, kutoka 2002, Rukwa ina shilingi milioni 579 na kuna watu milioni 1.1, Kigoma ina shilingi milioni 577 na watu wako milioni 1.9. Ukilinganisha na Singida na Shinyanga ambao wamepata fedha za nje kidogo wana milioni 770, Singida milioni 773, lakini ukiangalia robo ya watazania wanapesa maeneo hayo.

Kwa kijiografia maeneo hayo yamekaa katika eneo, sasa inakuwaje eneo moja la namna hiyo ambalo halina wafadhili, halina watu ambao wamekwenda kulifadhili. Inakuwaje linanyimwa fedha za ndani nyingi, mimi ningependekeza tu kwa sababu hawa wafadhili hawapendi huko mikoa ya pembezoni, basi pesa hizi ni za mitaji mikoa iweze kupendelewa, lakini ningependekeza vile vile barabara zinazoelekea katika maeneo hayo ziweze kujengwa kwa mfano barabara kutoka Kigoma, Tabora kuja Manyoni, Barabara kutoka Nzega, Tabora kwenda Mbeya na Mpanda ziweze kujengwa ili kuweza kuibua uchumi ambao unaweza kutusaidia katika kuinua hali ya wananchi wenyewe, lakini vilevile kuinua hali ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, tunazungumza juu ya mazao, mazao yote makubwa yanatoka kule, zungumzia pamba karibu nusu pamba inatoka mkoa wa Shinyanga, zungumzia tumbaku inatoka mkoa wa Tabora, zungumzia mazao madogo madogo kama vitunguu na alizeti vinatoka Tabora na Singida, zungumzia dhahabu, zungumzia Almasi, zungumzia wapi, zungumzia chochote kuna mikoa mingine wanalima mpaka wapelekewe Katibu Tarafa, lakini mikoa hiyo wanajituma ni watu ambao wana uwezo.

Kwa hiyo, mimi ningedhani tukae tukawapa kipaumbele ili tuweze kupambana na umaskini kukuza uchumi lakini tuwawekee kipaumbele zaidi katika barabara na umeme, kwa mfano, maeneo kama ya Singida, Shinyanga na Tabora yote yana gridi ya Taifa lakini umeme haujafika kwenye vijiji mbalimbali, kwa sababu kwa mfano tatizo kubwa liko mkoa Kigoma, Kigoma hawana kabisa umeme na Mkoa wa Rukwa hawana kabisa umeme.

Sasa lakini mikoa mingi katika kuzalisha iko mstari wa mbele lakini mtu anapendekeza, nilikuwa naomba kwamba mikoa kwa kweli kwa sababu inafanya kazi vizuri na iko katika maeneo mazuri ya uzalishaji basi tuipe kipaumbele kiasi kwamba miundombinu hii ya barabara umeme na maji vitu vya namna hiyo kama umwagiliaji viweze kupewa ili iweze kushiriki sawasawa na mikoa mingine ambayo iko katika

maeneo mazuri ya wafadhili, na ndio maana kuna vivutio vingi ambavyo viko katika maeneo hayo, ukienda Kigoma sasa hivi kuna utalii, unaweza kufanya utalii, ukienda Rukwa Katavi unaweza kufanya utalii.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache naunga mkono. (*Makofi*)

**MHE. ABDILLAH O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu katika hoja iliyoko mbele yetu. Lakini kabla ya hapo nianze na kuwaombea waliotutangulia wenzetu kama Mheshimiwa Abu Towegale Kiwanga na Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria na wengine kwa Mwenyezi Mungu wetu ili awaondolee adhabu ya kaburi na moto wa jehnamu milele *Alhamdulillah. Amin.*

La pili, nimpongeze Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Mheshimiwa Abeid Amani Karume na Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kwa kuwa wao ndio watakao kuwa wanapeperusha bendera yetu ya Chama Cha Mapinduzi na *Inshallah* Mwenyezi Mungu anatuona tunavyofanya kazi sisi wana Chama Cha Mapinduzi na Serikali yetu kuboresha maisha ya Watanzania, ataendelea tena kutupa na kutupa *Inshallah* watashinda wagombea wetu hawa wakijumuika na mimi maana yake kuniacha mimi tena itakuwa matatizo kidogo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii ni nzuri mimi nimeelezwa Jimboni kule Bajeti kwamba ikiwa nzuri unga mkono, usitupigie simu tena, lakini ikiwa mbaya ikatae huko, sasa mimi kwa maoni yangu naiona, kwa hiyo, natekeleza lile la kuunga mkono, naunga mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ila wakanieleza niboreshe na nieleze Serikali haya yafuatayo, kwamba sisi wa Mtwara Vijijini tumecharuka na ujenzi wa shule za sekondari, kila Kata shule ya Sekondari moja. Kwa hiyo, niombe Serikali milioni 14 alizotupa kila shule hazitoshi milioni 14 kujenga shule, tulikuwa tunaomba hela za MMES ziongezwe milioni 60, milioni 70 na sio shule tatu, nne kuwa zimepewa, shule zote kila Kata tunajenga shule ya sekondari. Shule zingine zimefikia kozi tano, kozi kumi, kozi kumi na tano, kozi ishirini kuna nyingine wanasoma lakini hazijakamilika tulikuwa tunaomba ruzuku ziongezwe.

Mheshimiwa Spika, shule hizi tunatarajia vijana wetu watapata elimu ya kisasa ya sayansi na teknolojia, bila umeme lengo hili halitafanikiwa. Mandhali kuna umeme huu wa gesi ya *Mnazibay*, tulikuwa tunaomba Serikali ipeleke umeme kila Kata ili kulisha kwenye shule, shule hizi ili azma ya kuwasomesha vijana wetu sayansi na teknolojia ikamilike, kuna kompyuta, na mambo mengine mengi na umeme ni muhimu katika shule hii. Lakini lingine ni maji, shule hizi tunakusudia kuweka hosteli hasa za watoto wa kike ili kuwaondolea mazingira ya vishawishi mbalimbali waweze kumaliza masomo yao. Sasa huwezi kuwaweka vijana mia nne, mia tano pamoja bila maji.

Mheshimiwa Spika, kwa stahili tumekubaliana jana na Mheshimiwa Waziri wa Maji kwamba *Inshallah* Mwenyezi Mungu akinirudisha madarakani tena basi nichukue

*District Water Master Plan* niende nikakae nae ili tuone katika hili tunalifanyaje bila Kata kuwa na maji ya uhakika kwa sababu ya hili na matumizi mengine ya kawaida.

Lakini lingine wameniambia mawasiliano, vijana wengi watakuwa kwenye shule hizo kutakuwa na mawasiliano mbalimbali yanahitajika. Sisi tunamwomba Waziri wa Mawasiliano akituwekea minara miwili tu ya *Celtel* mmoja akiuweka Dinyimba, mwingine akiuweka Kitaya basi Jimbo lote la Mtwara Vijijini litakuwa simu zinapatikana bila matatizo, sasa hivi ni sehemu tu inapatikana. Ni minara miwili tu iliyokosekana, kwa hiyo, nimetumwa kwa stahili niombe Serikali wafanye hivyo Jimbo zima lile litakuwa na mtandao.

Mheshimiwa Spika, lakini suala lingine wamenieleza nieleze Serikali katika Bajeti hii ni kwamba kilimo ni uti wa mgongo, na kwamba zao linalochangia Pato la Taifa moja wapo ni korosho na zao hili lilichukua nafasi ya tatu kama sikosei. Kwa mfano, mwaka jana tumechangia pato la Taifa hili si chini ya shilingi bilioni 39.5

Mheshimiwa Spika, lakini cha kusikitisha ni kwamba hali ya barabara zinazosafirisha korosho hizo kutoka kwa wakulima mpaka bandarini au zinazounganisha wilaya inayozalisha Korosho na Wilaya nyingine ni mbaya sana. Kwa hiyo, wanajimbo wa Mtwara Vijijini wameniomba niombe Serikali kwamba waimarishe na kuboresha barabara ya Hiari, Ihimba, Njengwa na Nanyiamba. Barabara ya Madimba, Kitaya, Mnongodi mpaka Chikwaye, barabara ya Mpapula, Kitele, barabara ya Mguho, Muungano na Madimba hadi Mtimbati, hizi barabara ndiyo maarufu katika kusafirishia korosho sasa zikiwa mbaya inakuwa matatizo kidogo.

Kwa hiyo, nilikuwa naiomba Serikali ili waweze kuboresha miundombinu hii ili kutetea uzalishaji wa zao hili linaloleta Pato la Taifa.

Lakini lingine ni ruzuku, walikuwa wanaiomba Serikali kutoa ruzuku katika pembejeo za kilimo. Wanamashaka sana kwamba, eti *sulphur* haitapewa ruzuku, hilo linawasikitisha kidogo kwasababu wameizoea. Walikuwa wanaiomba msiiache ghafila, mpunguze kutoa ruzuku mwaka hadi mwaka, lakini wakati huo huo mkituzoesha kutumia dawa hiyo ya maji mpya hiyo na mtuonyeshe kwa mfano kama inafaa maana yake tunavyo amini sisi ile kwa mujibu wa maelezo ya wana jimbo inaunguza mikorosho kwa hivyo kwa kweli hawana raha Mtwara, baada ya kusikia *Sulphur* inayodakiwa ni dawa ya maji hawakatai ili kile waliokuwa wanaiomba Serikali wawahakikishie kwamba hii ya maji itakuwa bora na mzuri kama ya *Sulphur*. Sisi hatuna haja ya *Sulphur* wala maji tunachokuwa na haja nacho ni dawa itakayofanya mazao ya korosho yawe bora na korosho zizae kwa wingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wanaomba hilo lizingatiwe, lakini lingine ni bei za pembejeo zenyewe hizi, pembejeo bei ghali mno ukilinganisha na bei ya korosho. Hapa pia wamenituma niombe Serikali waboreshe ubanguaji wa korosho, viwanda vya kubangua korosho ama wawekezaji wa nje au na ndani Serikali itusaidie ili korosho zinazotoka nchini hapa kwenda nje ziwe zimebanguliwa ili bei hii iboreshwe waweze kupata nzuri kwenye kutapu 4000 kwa kilo, kulingana na gharama za uzalishaji.

Suala lingine lilikuwa la *corridor*, kuna tetesi kwamba barabara itokee kwenda *Mbambabay* itapita Mnazi Mmoja mpaka Masasi. Sasa wa Mtwara Vijijini wakiungana na Tandahimba na Newala wanalalamika sana wameniomba nieleze Serikali kwamba hamtawatendea haki kama barabara hii ya *Mtwara Corridor* haitapita Mangamba, Tandahimba, Newala kutokea Masasi, itakuwa Wilaya ya Tandahimba na Newala mmeiacha katika mpango huu kwa sababu Mkoa wa Mtwara ni Mtwara, Tandahimba, Newala na Masasi. Mkipitisha kule unaziacha Tandahimba na Newala na mji wangu mdogo wa Nanyamba, kwa hiyo walikuwa wanaomba barabara hii ipite Mtwara, Tandahimba, Newala, Masasi na wala si vibaya tukiwa na mbili na nyingine basi itaboreshwa ile ya Mpapura, Mnazi Mmoja kutokea Masasi, kwani kuwa na vitu viwili kuna tatizo? Mbona hata katika urais kuna Rais na mgombea mwenza wanakuwa wawili wanasaidiana, kwani barabara hizi zikiboreshwa zote kuna nini.

Kwa hiyo, wanaiomba Serikali kufanya hivyo vinginevyo hamtalitendea haki. Mwisho Manispaa, Manispaa ya Mtwara hii kwani imekwama wapi mbona muda unakwisha? Mabwana ninyi tafadhali, Manispaa ya Mtwara tumeelezwa Manispaa maana yake tumeona tukimaliza hapa wa saba basi. Sasa katika hili kule, tunaiomba Serikali kabla ya kipindi hiki cha awamu ya tatu kumalizika basi *inshallah* Manispaa iwe imepatikana na habari zake ziwe zimeeleweka. *Wasalaam, waaleykum salaam.*

**MHE. YUSSUF KOMBO JUMA:** Mheshimiwa Spika, asante kwanza nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia mawazo yangu katika hotuba mbili hizi za Mawaziri waliokwisha kusoma hotuba zao.

Kwanza sina budi nami nitoe pole kwa wale wenzetu waliokwisha tangulia mbele ya haki na pia niseme tu kwa kuwa hili ndilo Bunge la kufunga dimba kwa kipindi hiki, niwapongeze sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Kwamtikpura na ni washukuru kwa ushirikiano walionipa katika kipindi changu chote cha uongozi, nasema shukrani sana.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niende moja kwa moja kwenye yale niliyoyakusudia kuyazungumza. Kwanza niseme tu naunga mkono hoja zote mbili kwa kuwa zimekidhi haja ya Watanzania kwa wale ambao tulikuwa tunayataraji kwa muda mrefu. Lakini niseme pia hakuna kivuli kizuri kisicho na kasoro, kuna baadhi ya sehemu kwa mawazo yangu nahisi zina matatizo kidogo na naomba niyaeleze ili Mawaziri wahusika waweze kurekebisha au kuboresha kwa yale mawazo nitakayoyatoa.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya mipango ya Waziri wa Mipango, kuna ukurasa wa 45 na 46, katika sehemu hiyo kuna matukio ya utekelezaji wa baadhi ya matumizi ya fedha za Kitaifa. Hapa kuna sehemu inasema Mashirika ya Umma kubinafsishwa na mambo mengine kama haya, mimi nakubali kwanza hiyo sera kwa sababu kwenye chama changu naikubali na naiunga mkono. Lakini yale matatizo ambayo yamejitokeza katika zoezi zima la shughuli hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuna matatizo kidogo hapo katika sehemu hiyo kuna sehemu wanasema katika zoezi Watanzania wengi walipata fursa ya kuwa wawekezaji.

Mchanganuo wa umiliki wa Mashirika haya 313 yaliyobinafsishwa umeonyesha kuwa Mashirika 160 yamenunuliwa na Watanzania kwa asilimia 100 na 24 yamenunuliwa na wawekezaji wa nje kwa asilimia 100 na 128 yamenunuliwa kwa ubia na wawekezaji Wakitanzania na wa nje.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nakubaliana na hiyo hatua, lakini katika hatua ya kubinafsisha Mashirika haya, wale Watanzania waliokuwa wanafanya kazi katika Mashirika hayo, huwa wanapata mazingira magumu wakati wa kubadilisha kutoka sehemu ya kwanza aliyokuwa ameajiriwa na kwenda sehemu ya pili. Sasa mimi nahisi huwa hatuwatendei haki Watanzania wenzetu kwa usumbufu wanaoupata katika hatua hii.

Sasa naiomba Wizara husika inayoshughulikia mambo haya iweke sawa mambo ili Watanzania wasione hili suala la kubinafsishwa kuwa ni mzigo na usumbufu kwao.

Mheshimiwa Spika, niende katika sehemu nyingine katika kitabu cha hali ya uchumi wa Kitaifa katika mwaka 2004 ukurasa wa 45 na 46. Hapa kuna maelezo kidogo nitaomba niyasome ili niweze kueleleza, anasema mwaka 2004 maandalizi ya utekelezaji wa mkakati mpana wa utekelezaji wa kilimo Afrika yalianza. Mkazo umetekelezwa katika programu. Sasa hapa nilichokusudia kusema kuna mambo yaliyopewa kipaumbele katika kupata misaada kuna Benki ya Dunia, kuna Benki ya Afrika yametajwa hapa mambo yenyewe ni sekta ya nishati, uchukuzi, mawasiliano akasema pamoja na kujenga uwezo.

Mheshimiwa Spika, sasa hapa mimi nashauri Serikali, tunaposema mawasiliano, nishati na kujenga uwezo basi tuwe na vigezo vya kuona kwamba Watanzania wote wanahaki sawa kupata kutumia na kufaidi matunda ya nchi yao na hapa nimekusudia hasa kuelekeza mawazo yangu katika suala zima la mambo ya Muungano. Niko Bungeni karibu mwaka wa tano sasa tulikuwa tunazungumzia mambo mengi, lakini hasa tunapofika yale ya Muungano huwa kidogo napata matatizo.

Sasa naomba sana Serikali kwa yale mambo ya Muungano tunapopata misaada kama hii ya nje ambayo inashirikisha moja kwa moja Serikali ya Muungano kwa ujumla, basi tuone tunatenda haki, tunakaa pamoja na kufikiria nini tufanye kwa pamoja basi tuweze kukamilisha yale malengo tumeyazungumza, kwa mfano tunaposema uchukuzi na mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, Zanzibar sote tunaifahamu, mimi ninamini kama Tanzania itakaa kwa makini na kufikiriwa ni jambo dogo tu kwa sekta hii ya mawasiliano kwa Zanzibar ikashughuliwa kwa mara moja, na ikawa Zanzibar tatizo la mawasiliano limekwisha tutakawa tunashughulikia mambo mengine kwa upande wa Tanzania au upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano. Sasa hapa nilikuwa nazishauri hizi Wizara ambazo hii ndio Bajeti kubwa, ndani ndio itakayokuwa na mchanganuo wakuona hiki kipelekwe wapi na wapi tupeleke nini basi nashauri Serikali kuzingatia na kuona yale mambo tunayoshirikiana nayo basi tuyafanye kwa nia njema, kwa kuona kwamba sote ni ndugu na huu Muungano wetu ni wadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niende katika suala la bandari, kule Zanzibar tunayo Bandari, lakini bandari ile kwa sasa ni sawa na kusema nyumba labda iliyofiliwa na wakazi wote wa nyumba hiyo, haina baba, haina mama na watoto wote hamna. Kwa sababu unaweza ukaenda usikute harakati zozote kama kunakufahamu bandari inatakiwa iwe.

Sasa mimi nashauri Wizara hizi kwa sababu ili ni jambo ambalo tunasema la Muungano, tuone tunafanyaje ili kuiwezesha Zanzibar kupata harakati za kibandari. Kwa sababu sasa hivi pale hapana kinachoendelea, unaweza ukaa mwezi mzima ikaja meli moja ukishusha pale unapata matatizo mengi. Sasa hapa naiomba Serikali iweke mazingira ya kuona kwamba na Zanzibar ile bandari inafanya kazi kikamilifu na kuweza kuwasaidia wale wananchi ambao wanategemea zaidi kipato chao kutoka sekta hiyo ya bandari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa kwanza kidogo naomba niende suala la Ukimwi, katika hotuba hizi Serikali imesema imetenga mambo mengi tu yatashughulikia. Lakini katika ukurasa wa 56 wa kitabu cha Hali ya Uchumi. Pale pana *graph* linatisha kwa kweli, *graph* ile inaonyesha kwamba Dar es Salaam, Mbeya zinaongoza, halafu wakaendelea kusema kwamba wanawake au wasichana ndio wanaoongoza kuwa na UKIMWI katika Tanzania. Lakini pia wakasema mkazo mkubwa katika bajeti hii umewekwa kuongeza Bajeti katika sehemu za kazi kutoa fedha ili kuona kwamba katika sehemu za unapungua.

Sasa mimi nilikuwa nataka kusema tu kwamba UKIMWI hauko tu katika sehemu za kazi, kwa sababu waliokuwa na kazi ni watu kidogo wenye kuwa na mawazo mazuri na mambo mengine yanafuata katika msaada wa maisha. Wanaopata UKIMWI ni watu wale wasio na kazi sasa hapa mimi nadhani Serikali kidogo izingatie tena ione kwamba zile fedha zilizotengwa zinakwenda moja kwa moja kwa wale watu wenye maisha ya chini wasio na ajira, ili UKIMWI usiongezeke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa kidogo niende katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika kitabu chake cha hotuba katika ukurasa wa 35. Waziri wa Fedha amesema katika ukurasa huo kwamba, katika kupanga mgawo wa fedha, Bajeti ya mwaka 2005/2006 mambo yafuatayo yamezingatiwa. Hapa katika yaliyozingatiwa ni pamoja na ile *four point five* ya Zanzibar, sasa mimi nataka kuelewa kwamba hii 4.5 ya Zanzibar kutokana na misaada ya nje kwa ninavyofahamu hii ilikuwa ni ya kipindi cha mpito kwamba kuna kipindi Serikali zilika zikazungumza kuona kwamba kwa sasa basi tuanzia hapa. Lakini baadae tukae tuone tunafanyaje, sasa mimi nauliza tu kwamba huo muda bado haujafika kwa sababu hapa tumesema tu kwamba Serikali imekuwa inamapato makubwa zaidi, misaada ya nje imekuwa mingi zaidi lakini bado tunazungumzia 4.5 mpaka lini.

Mheshimiwa Spika, sasa na hili nalo naomba Waziri mhusika atakapokuja basi atueleze vizuri na si kwa kurusharusha kwa sababu inaonekana kwamba wakati mwingine baadhi ya viongozi wetu wametujibu huwa wanarusha tu kuona kwamba hutopata nafasi tena ya kumweleza, wewe utasema anakuja yeye anamaliza basi.

Kwa hiyo, naomba atakapokuja au atakapokuja kwa yale yote ambayo Waheshimiwa Wabunge wanataka ufafanuzi au kujua basi atueleze kwa utaratibu, na hekima iwemo ndani yake na sijaziba au kuona kwamba wao wako sisi tuko nyuma vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na mwisho niseme tu kuhusu *TASAF*, mimi nataka nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Tanzania anayemaliza muda kwa swali la *TASAF*.

**MBUNGE FULANI:** Suala.

**MHE. YUSSUF KOMBO JUMA:** Sawa, sasa hasa nasema nampongeza Rais William Benjambin Mkapu, kwa kutuahidi kwamba awamu ya pili ya *TASAF* kuja kama haijapita lakini pia kwa hili naomba sana itakapofika *TASAF* awamu ya pili pia ije kwa Mtipura, kwa sababu awamu ya kwanza tumefanya vizuri sana pale Kwamtipura na katika vigezo vya *TASAF* wanasema utakafanya vizuri awamu kwanza basi awamu ya pili haina matatizo. Kwa hiyo, mimi nasema tu Kwamtipura tumefanya vizuri, kwa hiyo naikaribisha awamu ya pili ya *TASAF* ili ije tufanye kazi kwa pamoja na kujenga nchi kama tulivyotarajia.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia nasema naunga mkono hoja mia kwa mia asante sana. *(Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie Bajeti ya Serikali. Nianze kwa kutoa pole kwa wenzetu waliopatwa na msiba na sisi Wabunge tukiwa tumempoteza mwenzetu, kipenzi wetu ambaye tulikuwa naye kwa muda mrefu kidogo.

Napenda nitoe pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Mheshimiwa Abeid Amani Karume na Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa waendeshe nchi hii kuanzia mwezi wa kumi mwaka huu. Wameshapita na wala wasiwe na wasiwasi.

Mheshimiwa Spika, nianze kutoa salaam kwa Mheshimiwa Waziri Basil Mramba na vile vile kumuuliza wananchi wa Iramba Mashariki na Watanzania wote wamenituma nimuulize bei ya bati na *cement* zitapungua lini? *(Makofi)*

Sasa hivi wananchi wetu wanajenga nyumba za kisasa, mwaka jana uliahidi wanasema bei bado mbaya sasa wanataka majibu kutoka kwako. Vile vile niseme wananchi wa Rombo na Iramba Mashariki wanaolima alizeti kwa wingi wanauliza kwa nini unawatesa, kwa nini bei haiongezeki, kwa nini unapunguza kodi kwa mafuta yanayoingia kutoka nje? Wanataka majibu ya hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunasikika kote nchini na tunaonekana kwenye luninga, wananchi wanakataa kwamba nchi yetu si maskini bali Serikali ndio inafanya waendeleo na umaskini kwa sababu inaruhusu maji yaende Baharini bila kuyatumia. Wanasema tungeweza kufanya umwagiliaji wa kutosha tusingekuwa na njaa na huu



umaskini ambao tunalazimishwa na Serikali usingekuwepo, tuna madini mengi lakini mpaka sasa msimamo wetu bado haupo vizuri ndio maana Serikali inadiriki kuandika Tanzania ni nchi maskini sana. Sisi sio maskini, maskini ni Somalia ambao kuna jangwa na nchi nyingine Ethiopia, lakini Tanzania si maskini na sasa tunaitaka Serikali itumie njia tusiendele kuitwa maskini na maliasili tunazo, hiyo naomba sana. *(Makofi)*

Kuna hili neno MKUKUTA, njia ya kuwaondolea wananchi wetu umaskini, tunalazimisha wananchi wetu wawe maskini kwa sababu wanalima, wanazalisha lakini bei hakuna. Tukiendelea hivi bila kuwapatia masoko mazuri wananchi wetu hawataridhika na hayo tunayoyafanya.

Kwa hiyo, tunaomba na sasa hivi ili kuondoa umaskini ni kugawa raslimali ya Taifa iende kote. Mkoa kama Singida unaozalisha alizeti kijengwe kiwanda cha alizeti kikubwa tukamue mafuta, tupeleke mafuta baadala ya kuuza alizeti. Tabora wana asali nyingi, karanga na kadhalika, huko kwenye kahawa, kule kwenye karanga, pamba vijengwe viwanda na visimamiwe sawa sawa. *(Makofi)*

Mimi sikatai wawezaji kuja lakini waje tuwasimamie na wasitunyonye. Sisi tuambulie kodi tu, tugawane hata wao wakichukua 65 basi sisi tubaki na hiyo 35 itakuwa nafuu kuliko sasa ambao tunapigizana kelele na mrahaba.

Mheshimiwa Spika, mimi nashukuru sana kukua kwa uchumi wetu lakini kukua kwa uchumi hakusaidii kama wananchi wetu wataendelea kupata shida. Kukua kwa uchumi ni lazima wananchi wetu watoke waende na maisha mazuri la sivyo tutakuwa hatufanyi kazi na tutakuja kuulizwa mbele ya haki.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi naipongeza Serikali inajenga nyumba kwa ajili ya watumishi wake, lakini bado mgawanyo wa ujenzi wa hizi nyumba haufai. Nyumba zinajengwa Dar es Salaam na Dodoma, je Shinyanga, Singida, Tabora, Mtwara na ambako nako nyumba ziliuzwa ni lini utaratibu huu utanza? *(Makofi)*

Tunaomba kila mwaka badala ya kujenga Dar es Salaam na Dodoma zitawanywe hizi fedha, mbona wakati wa kuuza nyumba ziliuzwa mahali pote kwa nini leo kujenga mnajenga mahali pamoja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije kwenye UKIMWI bado hatujafanya kazi, bado tunaendelea na warsha, bado mnaendelea kuwavalisha wananchi *t-shirt* zilizoandikwa UKIMWI. Sasa hivi inatakiwa tufanye kazi, dawa ziwafikie wagonjwa kule walipo na hawa wagonjwa wapewe chakula na mahitaji mengine wakati wa warsha umekwisha sasa twende kwenye utekelezaji.

Mimi naomba Mheshimiwa Waziri atakapojibu atuambie ni lini dawa zitatoka na zitagawanywaje ziene Tanzania nzima? Sasa hivi kule kunakokwenda dawa tena wagonjwa wanapewa sio *dose* kamili, halafu ni wagonjwa wachache wale mamilioni wanaendelea kufa. Sasa tusiwe na upendeleo, Watanzania wote tuko sawa na dawa zipelekwe kila mahali.

Mheshimiwa Spika, naomba nije kwa wastaafu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kweli imekuwa aibu kwa Tanzania, wenzetu wote walishawalipa, sisi tunaendelea ni aibu sana. Tanzania tunasifiwa kwa mambo mengi lakini kwa hili ni aje? Kila mwaka, kila mwezi wahusika waandamane kwanza wengi walishakufa na waliobaki ni wazee sana na bado mnataka kuwalipa kwa thamani ya dola ya mwaka 1977 haipendezi. Sisi tunaomba hili suala liishe na liishe haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa sababu imeahidi hapa mimi nina imani itatekeleza haraka iwezekanavyo. Nije kwa watendaji wa vijiji, hawa watu ndio wanaokaa na wananchi, hawa watu ndio wanaowasaidia wananchi sasa imepita muda mrefu hawalipwi fedha zao. Mimi kwa hapa sina ya kuzunguka naomba kuanzia mwezi huu wa saba Serikali ianze kulipa na wote walipwe wanaohusika. *(Makofi)*

Nije *PPF*, *PPF* imesifiwa sana imefanya kazi nzuri sana, faida ya mtu kufanya kazi ananyang'anywa madaraka aliyonayo. Yule kiongozi aliyeko pale sasa hivi anakaimu, kazi hii nzuri yote aliyoifanya, ni aibu kwa Serikali yetu kama huyu mtu kafanya vizuri kwa nini asiendele na kazi hiyo? Yanatolewa matangazo ya kazi kimya kimya, sasa sisi kama Wabunge tunamwomba huyu bwana aongezewe muda. Mbona wengine wanastaafu wanaongezewa muda? Huyu kafanya kazi nzuri Bunge linamsifu, wananchi wanamsifu na hata Serikali leo wanataka kumnyang'anya madaraka, Mheshimiwa Basil Mramba, liangalie hilo. *(Makofi)*

La mwisho nije Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, kuna mambo ya aibu na mabaya yanayofanyika huko. Kuna watu wamekuwa wanafanya kazi kwenye Ofisi hii kwa miaka mingi na sifa wanazo wanachukuliwa watu nje kuja kushika nafasi yao na wale ambao wamepata ajira, *appointment* ya Rais, wanaambiwa sasa hivi baada ya muda mtaondoka, wameambiwa wanakaimu hivyo vyeo walivyonavyo kwa muda. Hawa watu wako nchi nzima na ndio wanaokusaidia Mheshimiwa Basil Mramba, kukagua mahesabu na ndio wanaosaidi kufichua maovu yanayofanyika hapa nchini, leo mnasema hawafai mnataka kuajiri wengine tena kwa upendeleo. Tunaomba mliangalie upya hata kama nia yenu ilikuwa nzuri lakini sio kwa hapo, hebu kaeni mkae mfikirie na muajiri upya.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa na haya tu naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuchangia hoja hii. Kwanza na mimi niwapongeze sana hasa Serikali kwa ujumla kwa Bajeti ambayo ni endelevu iliyokuja hapa, lakini kwanza nimpongeze sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Benjamin William Mkapa kwa kuongoza Baraza lake vizuri na kutufikisha hapa tulipo. Amekuwa anatuletea sifa kubwa huko kwenye Tume ya Mambo ya Utandawazi kama Mwenyekiti mwenzwa, amekuwa kwenye Tume ya Afrika ambayo ripoti yake imezinduliwa jana.

Kwa hiyo, tunampongeza kwa kweli kwa kuwa ametuwekea sifa kubwa sana hapa. Lakini nimpongeze vile vile Mheshimiwa Basil Mramba, kwa Bajeti nzuri na Makatibu Wakuu wote na watendaji wake wote, pamoja na rafiki yangu Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda kwa mwelekeo mzuri wa uchumi ambao kwa kweli unakuwa tunaenda mbele, matatizo hayawezi kuisha hata kama tungepata nini lakini bado binadamu tutakuwa na matatizo lakini Bajeti inakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe shukrani sana kwa *TRA*, kule Tunduma nilikuwa nikipiga kelele sana hapa kwamba pamoja na makusanyo makubwa sana pale Tunduma vijumba vile vilikuwa vibaya sana ukilinganisha na zile za wenzetu, zile za forodha pamoja na wahamiaji yale majengo yalikuwa mabaya sana, yalikuwa yanatia aibu kwa sababu Zambia walikuwa na nyumba nzuri. Sasa nataka nitoe taarifa kwamba wamejenga jengo zuri sana na hata Wazambia sasa wanafika mahali wanashangaa na nasikia na hili la Uhamiaji nalo wanaliondoa napenda niwashukuru sana kwa niaba ya wananchi wa Tunduma. (*Makofi*)

Napenda niwapongeze kwenye Bajeti hii kumetajwa ambayo Mheshimiwa mwenzangu amesema sasa hivi kwamba watalipwa wale wafanyakazi wa zamani waliokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na kuwarudisha kwenye daftari la pensheni wale wastaafu waliochukua hela yako kwa mkupuo.

Sasa mimi nafikiri jambo jema ni kumalizana na jambo hili moja kwa moja zitafutwe hela, walipwe tuachane na jambo hili, kurudia rudia kila siku inaonekana kama tukija hapa tunaanza kujifurahisha kuwaambia watu waweze kuwa na mategemeo na matumaini ambayo hayapo. Mimi nadhani Mheshimiwa Basil Mramba, utafute tu hela watu hawa wote wa aina hizi walipwe halafu na wale ambao waliingia kwenye pensheni wajue ni kiasi gani, halafu tumalizane na jambo hilo na bado mambo yatazidi kwenda kuwa mazuri zaidi tunaomba sana, na sisi tunasumbuliwa kule naona Wabunge hapa kila nikizungumza wanapiga makofi kwa sababu sisi tunasumbuliwa, wanakuja sasa imekuwaje hapa, tumeambiwa watapata lini? Sasa wanaandamana hata kuandamana. Mimi nafikiri jambo hili la ku-clear kama walivyofanya watu wengine, fumba macho, tafuta hela, ondoa basi mambo yanaishia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nashangaa kwa sababu mimi naona Bajeti ni nzuri, yale ambayo tunaweka tunaongezea tu. Sasa ninapoangalia unasoma kwenye gazeti au unaangalie kwenye *TV* unakuta mtu ameng'ang'ana, tena mtu mnayemtegemea kabisa angeweza kuwaelimisha watu vizuri anasema hii ni Bajeti ya kisiasa. Sasa Bajeti ya kisiasa maana yake nini? Mimi sielewi Bajeti ya kisiasa na Bajeti ya kawaida, sielewi labda mimi sijasoma sawasawa Bajeti ya kisiasa maana yake nini? Haitoi huduma kwa wananchi? Inapelekwa labda hela kwenye chama tawala au inakuwa namna gani.

Mimi nafikiri hakuna Bajeti ya siasa, hii ni Bajeti ya nchi na inachukiza sana inapoonekana kiongozi tena mchumi ambaye angeweza kuongoza, asipotoshe watu awaeleze watu kweli ni kiongozi mzima, mchumi kabisa mshauri wa zamani wa mambo ya uchumi kwa Rais anasimama kwenye *TV* anasema hii Bajeti ni ya kisiasa. Kisiasa

maana yake nini? Si Bajeti tumeweka huduma humo, tumeweka hiki tunafanya hiki ndio maana ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nafikiri Mheshimiwa tusipotoshe wananchi, Bajeti ni nzuri labda tuwe tunaongezea tu kwamba labda hapa wangepanya hivi ingekuwa hivi na ndio maana rafiki yangu Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, alipokuwa anasoma hapa nashukuru na wewe ulitoa *comment* kwamba hii ni sera na labda sera anaweka sera yao na ikaonekana kama ni Bajeti ya namana yake. Kwa hiyo, tuliendelea kushangaa hapa lakini tunasema hii ni Bajeti ya Serikali inagusa wananchi, kwa hiyo, hilo niweke namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu nadhani wenzangu wamelizungumza lakini kuna hili neno huu msamiati mpya umekuja na ni mzuri mtaji mfu kwamba tuna mitaji ambayo inaonekana imekufa lakini mtaji, mojawapo ni binadamu kama binadamu atakuwa anaamka asubuhi anakaa tu anacheza bao hafanyi shughuli nyingine yoyote ya kuzalisha huo ni mtaji mfu yaani mwingine anazurula tu toka asubuhi anapiga piga chenga tu hashughuliki na uzalishaji wa aina yoyote ile huo ni mtaji mfu. Lakini atakula kwa hiyo, atakula jasho la watu wengine hata kama tungeondoa ile Sheria ya nguvu kazi mimi nadhani labda tufikirie upya, lazima mtu afanye kazi.

Kwa hiyo, huo mtaji mfu wa binadamu ufufuliwe halafu mtaji mfu huo wa binadamu utumike vizuri, kwa mfano, sasa wale ambao ni wazalishaji ambao wangeweza kumiliki mashamba mkubwa kwa sababu nchi yetu ina maeneo makubwa ya kulima ni vijana. Lakini mimi sidhani kama vijana zile biashara wanazofanya mijini za kubeba maduka mgongoni au kuuza tu maji ambavyo ungesanya kwa pamoja aliyonayo ni mtaji wa shilingi 5,000 tu. Sidhani kama ule mtaji unaweza ukamkomboa, ule haumkomboi lazima ufanywe utaratibu au sera kamili jinsi gani tutawatumia vijana ambao ni nguvu kazi waweze kuzalisha kwenye mashamba, kwenye ufugaji kwenye shughuli zingine. Mzee Julius Nyerere alikuwa anasema hiki kitoto ni *anti-people*, kilimo ni *anti-people* yaani binadamu kilimo ni *anti-people* yaani binadamu ni kitu kibaya kwa binadamu isipokuwa na kilimo. Vijana wangeweza kuelimishwa wapate *guidances* na *counseling* waweze kutumia nguvu wanazozurula kutoka kutoka Manzese mpaka kuzunguka mji mzima.

Mheshimiwa Spika, mpaka siku nyingine unanunua kwa kumuhurumia kwa sababu na sisi wenyewe tuna watoto kama hao, ukiona anazurula hata kama kitu chenyewe unacho, mimi kwa mfano nimenunua viatu vingi kumbe vingi vimejaa kule nasema kumbe nilinunua ingawa viatu vingi tu, huku nawaonea huruma nanunua halafu unarundika wala huvivai. Kwa kuona huruma wale vijana wanatumia nguvu zao nyingi sana kwa kuzalisha kitu kidogo sana, kwa nini kama nchi hatuwezi kuwa na sera nzuri ya kutoa elimu ili vijana waweze wenyewe kuokoka watokane na kuzurula waanze kufanya kazi za kuzalisha za kuwasaidia baadaye, ule mtaji wanaoufanya ule hauwezi kuwasaidia chochote katika maisha yao hawawezi wakajikomboa. Hata ukiwauliza je, unadhani utajikomboa kwa kwa kuuza hizi *biscuit* kila siku? Anasema hainikomboi napata mkate wa kila siku. Sasa yule ni kijana hawezi kupata mkate tu wa kila siku anatakiwa apate mkate wa kila siku, lakini na baadaye kwa sababu ataoa atakuwa na watoto sasa huo ndio

mtaji bado ni mdogo. Mtaji mwingine ni huu mtaji wa raslimali Mheshimiwa wangu amesema hapa Mheshimiwa Mgana Msindai, raslimali.

Mheshimiwa Spika, kila watu wamepewa, Mungu amewajalia kila watu, tazama kule jangwani hakuna miti, hakuna nini lakini Mungu aliweka mafuta. Mungu kila mahali ameweka kitu, hawezi kuacha viumbe wake wafe hivi hivi ni jangwa tupu wote ambao wamekwenda jangwani wanajua. Ni jangwa kwa maana hakuna nyasi hakuna kitu chochote, lakini ameweka mafuta na wale watu wanaishi kwa mafuta. Lakini mafuta yale wanahakikisha kwamba yanawaletea fedha na maisha bora yanakuza uchumi wao kule. Vile vile sehemu nyingine kama Kongo wamepewe madini mengi tu, chungu nzima pale lakini sijui wanayatumia namna gani, sasa ule kwao ni mtaji mfu.

Mheshimiwa Spika, sisi hapa tuna madini mengi lakini sasa mimi nadhani labda tunakuwa na huruma sana. Kwa sababu mimi sidhani kama tunapata sana kutokana na madini, maana ukiangalia kwenye tovuti ukiangalia ile hesabu maana hivi hivi huwezi kudang'anya mtu kila kitu kiko kwenye utandawazi kule unakwenda tu unatafuta huko kwenye vifaa vya sasa hivi hivyo unapata almasi ilikuwa kiasi fulani, halafu unasema mbona sisi tumeambiwa tumezata kiasi hiki. Huwezi kificha mtu sasa ni utandawazi na sasa Sayansi Teknolojia imekuwa.

Kwa hiyo, mimi naona hatujapata sawa sawa madini na huruma hii ya kutoa kodi haya tunaondoa kodi sana, jamani huo ndiyo mtaji Mungu ametupa. Kwa hiyo, lazima utumie u-*capitalize*, lazima ung'ang'anie na mtaji ambao Mungu amekupa. Tung'ang'anie vile vile kwa mfano, kuna *geography* tu nzuri tu, kuna maliasili, kuna uvuvi tu, kuna mambo mengi, kwa nini tusi-*capitalize* katika hivi tulivyonyo hata hizi wanazokuja kuwekeza hivi, madudu makubwa makubwa. Tusiwe na huruma sana maana yake huo ndiyo mtaji wetu, mimi nilikuwa naomba sana tuweze kutumia mtaji mfu, binadamu wafanye kazi, raslimali zifanye kazi, jiografia yetu izalishe. Tutaongeza zaidi itakuwa sio 6.7 itakwenda zaidi ya hapo hilo nilitaka nilizungumzie kwa namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ingawa niliuliza swali hapa juzi kwamba lakini wazee kwa nini hamfikirii Wilaya ya Mbozi kuigawanya, sasa ni wakati wangu wa kuzungumza maana yake kwenye Bajeti ijayo waweze kuiweka. Wilaya ya Mbozi yenye watu 500,000 si sawasawa na Wilaya zenye watu 80,000 kuna Wilaya zilianza zina watu 45,000 ninazo siwezi kutaja kwa sababu wenzangu hawatapenda hapa.

Mheshimiwa Spika, ziko Wilaya katika nchi hii zina watu 80,000 sio laki, kuna Wilaya ina watu 42,000 sasa unamwelezaji mwananchi wa Mbozi mwenye watu 500,000 na jiografia imekaa vibaya, huku kuna bonde, huku kuna milima kiasi kwamba hata ukitaka ukitaka kuzungukia kwenye Jimbo lako unashindwa. Lazima kwanye mlima ng'ambo hapa kilometa 10 tu kutoka ulipo hapa, lakini ukitaka kuja huko kama uko bondeni kule itabaidi uende mpaka mjini Mbozi kilometa 80 ukazunguke tena mpaka huku kilometa 100 na kitu, unazunguka tu.

Mheshimiwa Spika, wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu walipita kwenye Jimbo langu, akina Mheshimiwa Haroub Said Masoud, hawa wote hawa

walishangaa Tarafa yangu moja ni kilometa 104 kutoka Tunduma mpaka ninapokutakana na Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, na bahati nzuri Mheshimiwa Basil Mramba wewe mwenyewe ulikuwa Mkuu wa Mkoa, ninachokisema ni kweli, ni kweli tupu. Sasa ulikuwa Mkuu wa Mkoa na ukapewa na Kijiji na unaitwa Mnyamwanga kama kabila langu. Pale Mnyamwanga mwenzangu namwita siku zote hapa anafahamu, huwezi kufanya hivyo kwa Wilaya nyingine ina watu 42,000 sana sana 80,000 unawapendelea kwa nini, Wanyamwanga si watu au Wanyiha si watu? Kwa nini *just very improportional 42,000* au 80,000 kwa 500,000, jamani, haiwezekani. Huwezi kueleza, unaonekana wewe una tabia ya kupendelea upande fulani, unaweza kuwa na nia njema tu, lakini kwa nini unagawa Wilaya ya watu 42,000 au 45,000 au 80,000 na mwenye watu 500,000 unasema hakuna hela, *how do you manage* hata Mkuu wa Wilaya mwenyewe tunamwonea huruma. Halafu unashindwa, mara uende bondeni, mara wapi.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa mfano Jimbo langu hiyo mliyoona Mheshimiwa Haroub Said Masoud, hiyo ilikuwa ni Tarafa moja tu, hamkuona Tarafa nyingine mbili, mimi nikitaka kuzunguka kwenye Jimbo langu ndugu zangu ni lazima nichukuwe sanduku mbili za nguo. Sanduku moja ni ya kuweka zile nguo chafu, nyinge ya kubadilisha na siku zote ili uweze kumaliza hata mwezi mmoja vijiji vyote, unatakiwa upige mkutano mitatu kwa siku na kwa siku 30 utakuwa umefanya vijiji 90, *but the villages are more than that*. Hilo ni Jimbo siyo Wilaya sasa unaelezaje, mwingine watu 42,000 mwingine 500,000 kwa Wilaya ya Mbozi, si tunatoka kule Kusini hakuna fedha za kugawa, kwa kugawa Mkoa mwingine juzi juzi wamepata Wilaya mbili mpya.

Wilaya nyingine wakizitaja mimi nasema hivi kuna Wilaya tena ya namna hii katika nchi hii, maana nyingine zikitajwa nasema hivi nayo ni Wilaya, yaani unashangaa. Sasa Mheshimiwa Basil Mramba wewe ulishakuwa kule na ulishakuwa Mnyamwanga mwenzetu, *ubuha Mnyiha* mwenzetu kule, kwa nini mnakosa hela kwa Mbozi tu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mtaeleza nini kwa watu wako, zipo Wilaya hapa tunazifahamu, lakini ni Wilaya, tuna Tarafa sita kubwa na vijiji vyetu ni vikubwa ni vijiji tu waliotembea kule wanajua. Mimi nina unga mkono hii hoja, lakini kwa maana najua kwamba bila shaka Bajeti ijayo Wilaya hii itagawanywa na Majimbo yatagawanywa, lazima *they are should be fairness* katika *contribution* ya mapato ya nchi. Hayawezi yakawa yanayumbia upande mmoja tu jamani. Tunajua jitihada ni kubwa na kazi nyingi hata hivyo kwa Wilaya ya Mbozi Serikali imeifanyia mambo mengi mema, tunashukuru sana Mheshimiwa Basil Mramba, mambo mengi mema mmeyafanya ni hili tu linatusumbua kwa ukubwa ule hamuwezi kuwahudumia watu vizuri .

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. OMAR S. KWAANG’:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nitumie nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye hoja iliyoko mbele yetu. Lakini kwanza kabla sijachangia niungane na wenzangu katika kutoa pole kwa wananchi wa Jimbo la Kilombelo kwa kufiwa na Mbunge Mheshimiwa Abu

Kiwanga, ambaye kwa kweli alikuwa mwenzetu na tunaomba Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, la pili naomba nitumie nafasi hii kwa kweli kuwapongeza wote walioteuliwa na Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya kupeperusha bendera ya Chama cha Mapinduzi wakati wa Uchaguzi Mkuu. Naomba nianze na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kama Mgombea Urais kupitia Chama cha Mapinduzi na Mgombea Mwenza, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, ambaye vile vile kwa sasa bado ni Makamu wa Rais na vile vile Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa kuteuliwa kugombea kiti cha Urais wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomaba nitumie nafasi hii kuwapongeza vile vile Waheshimiwa Mawaziri wawili, Waziri wa Mipango pamoja na Waziri wa Fedha kwa hotuba zao nzuri ambazo kwa kweli zimetupa dira ya kutekeleza Bajeti hii ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Serikali ambayo imewasilishwa ni mwanzo wa kuanza kutekeleza kitu kinachoitwa MKUKUTA, maana yake ni Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini. Sasa niseme yapo ya kupongeza katika kipindi amabacho kimepita na yapo ambayo kwa kweli tungependa kutoa maoni yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nianze kwa kuipongeza Serikali kwa ujumla wake kwamba ukuwaji wa Pato la Taifa umetufikisha mahali ambapo mwaka 2004 Pato la Taifa limekuwa kwa asilimia 6.7 na inaendelea vizuri kwa wastani wa karibu wa asilimia 5.8 na tunaipongeza Serikali vile vile kwamba sasa tuna akiba ya fedha za kigeni na akiba hii inakuwa kwa asilimia 12.7 na tunayo akiba inayoweza kutosheleza kwa miezi saba, na vile vile sasa tunakopesheka na tupo kwenye nafasi ya kusema tukope wapi. Kwa hiyo, ni jambo la kupongezwa kwa kweli kwamba tunakopesheka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile Bajeti hii imeinua hali kidogo ya wafanyakazi kwa kuongezea kidogo kile ambacho Serikali imeona kinaweza, kwa hiyo, vile vile ni hatua katika kuwapunguzia makali ya maisha. Vile vile nimeona kwamba ada za leseni za usafirishaji kwa baadhi ya magari zimefutwa na msamaha wa *VAT* umetolewa kwa magari yanayotumika kutoa huduma za afya zile *Mobile Health Clinics*.

Kwa hiyo, kwa kweli ni maeneo ya kupongezwa sana. Lakini vile vile tusingahau huduma za jamii hasa katika elimu tukianza elimu ya msingi imeanza kuboreka hasa kupitia mpango wa MEM na kwamba sasa tumeanza mpango wa MMES tuna hakika vile vile uboreshaji utafanyika vizuri na baadaye kuelekea kwenye elimu ya juu. Haya kwa kweli ni mafanikio ambayo Serikali hii inapaswa kujivunia na Wananchi wake wanapaswa kujivunia kwamba Serikali imefanya kazi ya kutosha, tunawapongeza wote.

Mheshimiwa Spika, kila anayesimama hapa kwa sehemu kubwa lazima atagusia kidogo habari hii ya MKUKUTA na hasa kwenye sekta hii ya kilimo. Uchumi wetu mwaka 2004 ulikuwa kwa 6% na tunatarajia kufika 10% na tunakubaliana wote kwamba pembejeo zote na dhana za kilimo zimesamehewa Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*), tunakubaliana kabisa lakini bado bei ya zana za kilimo ziko juu. Sasa maana ya msamaha

ni nini? Maana lazima tufike hapo tujue! Matrekta bei ni juu, majembe ya kukokotwa na ng'ombe bei ni juu, mbolea bei ni juu, dawa bei ni juu na zana za kilimo ghali. Kwa hiyo, ni lazima tujiulize ni nini hasa kinachofanyika hapo.

Mheshimiwa Spika, lakini tatizo zaidi ni vipuri vya zana za kilimo vinatozwa Kodi ya VAT. Sababu iliyotolewa jana na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula alipokuwa anajibu swali langu ni kwa sababu vile vipuri vinaingilia na baadhi ya vipuri vya magari. Sasa lazima tufike mahali tuchambue jambo hili kwa makini kwa sababu hicho ndicho kitu kinachoumiza wakulima. Matrekta mengi ni ya zamani, zana nyingi za kilimo ndio hizo ambazo zimetumika miaka mingi zaidi na kwa sababu hiyo vipuri vitahitajika sana. Kwa ajili hiyo mkulima hawezi kusogea hata kidogo kwa sababu kila akienda kununua *spare parts* kwa ajili ya kifaa au zana za kilimo anatozwa hiyo VAT. Kwa hiyo, eneo hili ni lazima Serikali ilifanyie kazi. Tukitaka kuinua kilimo, tusipapase, twende moja kwa moja kuwasaidia wananchi hawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suluhu ni nini? Suluhu ya kwanza ndio hiyo kuondoa VAT kwenye vipuri na zana za kilimo. Pili, tunapozungumzia habari ya ruzuku, mimi bado naona tunapapasa. Hii kusema tu kwa ujumla kwamba ruzuku inatolewa kwenye mbolea na nini mimi nilidhani twende zaidi ya hapo. Kwa mfano tuseme hivi mtu akinunua jembe la kukokotwa na ng'ombe (plau) kama bei yake ni shilingi 150,000 Serikali iseme wewe tutakupa ruzuku 50% kwa hiyo ainunue kwa shilingi 75,000 halafu aambiwe kwamba lengo tunataka utumie jembe hilo uinue kilimo chako kwa kiwango hiki, tufike hapo tumsimamie mkulima pale alipo. Kama yupo mkulima ananunua trekta labda ni shilingi 20,000,000 hadi shilingi 30,000,000, Serikali iseme ukiweza kununua trekta basi sisi tutakupa ruzuku kwa 50%. Kwa hiyo, ainunue ile trekta kwa mfano shilingi 15,000,000 halafu huyu mtu apewe malengo atalitumiaje trekta hilo na atakuza namna gani kilimo? Lakini bila kufika hapo na kwenye usimamizi kwa kweli tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu na kila siku tutasema kwamba ruzuku tumeitoa kwenye mbolea lakini matokeo hatuyaoni. Tufike hapo, tufike hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kutoa kwa mfano mikopo kwenye Mfuko wa Pembejeo, mimi nakubali lakini ni wangapi wanaweza kutimiza hayo masharti. Tunayaita masharti nafuu lakini watu hawawezi kununua hata hilo jembe la kukokotwa na ng'ombe. Sasa ukitaka kweli kufanya yawe masharti nafuu ndio hilo ninalosema ni lazima utoe ruzuku kwenye dhana za kilimo na kwa 50% hapo ndio tutavuka na tutapeleka kilimo kikue kwa 10%.

**MBUNGE FULANI:** Rudia hiyo *point*.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Spika, vile vile nizungumzie suala lingine ambapo ni mpango wa kutengeneza barabara. Tunajua kabisa mtandao wa barabara hapa nchini ni mkubwa karibu kilometa 85,000. Kuna barabara kuu, za Mikoa na za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Barabara kwa barabara kuu na za Mkoa 70% ya fedha za ule Mfuko ndio zinazokwenda huko halafu 30% ndizo zinazokwenda kwenye



Halmashauri za Wilaya. Lakini lazima hapa tujiulize mtandao mkubwa ni upi kama kweli tunataka kuinua kilimo? Kwa sababu tunaweza kuhamasisha wananchi wakazalisha sana lakini mazao yakaozea huko vijijini kwa sababu hayatakuwa na njia ya kupita. Nadhani huu mgao umepitwa na wakati. (*Makofi*)

**WABUNGE FULANI:** Ndio.

**MHE. OMAR S. KWAANGW’:** Huu mgao wa 30% ya Mfuko wa Barabara ziende kwenye Halmashauri za Wilaya na 70% ziende kwenye barabara kuu na Mkoa naona aina hii ya mgao imepitwa na wakati, tutafute namna nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nadhani vile viwango sasa vimepitwa na wakati hivi ambavyo tunachangia huu mfuko wa barabara kwa sababu barabara zinataka fedha na fedha lazima itafutwe sasa hatuwezi kukaa na kiwango hicho kwa muda mrefu sana tumekaa barabara haziwezi kusogea hata kidogo. Kwa hiyo, nadhani sasa kile kiwango kibadilishwe ili tufike mahali tuseme tukifikia hapa kweli tutatengeneza barabara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, utaratibu unaotumika kwa mfano mipango hii ya fedha zinazokwenda kwenye Halmashauri za Wilaya, kwa kweli hii mipango haifai kabisa. Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuendelea kutoa fedha kwa mitindo hii ni kupoteza raslimali na fedha.

**MBUNGE FULANI:** Haifai.

**MHE. OMAR S. KWAANGW’:** Kwa sababu gani? Halmashauri za Wilaya zinajadili mipango ya kutengeneza barabara halafu fedha zinapelekwa kule kulingana na ile mipango lakini fedha inayopelekwa kwa mfano ni shilingi 50,000,000 halafu kule Wilayani wanasema inatangazwa tenda barabara fulani shilingi 10,000,000 nyingine shilingi 5,000,000, nyingine shilingi 20,000,000, sasa tunagawana gawana hizo fedha kidogo barabara gani itatengenezwa na bado aitwe mkandarasa kwa mfano tangazo linatoka Babati mkandarasi anaitwa kutoka Dar es Salaam maana yake ni nini?

Mheshimiwa Spika, *mobilization* peke yake inamaliza hizo fedha kabla hata hajaanza kuleta hiyo greda, haina mantiki hata kidogo, ni lazima tubadilishe huu utaratibu wa namna ya kutengeneza barabara zilizoko vijijini. Kama ni kutumia *false account* tufanye hivyo lakini habari ya mkandarasi mpaka kule na wakandarasi hakuna au vinginevyo TAMISEMI nao basi wawe na *TANROAD* ya aina yao au iwe moja lakini vinginevyo tunapoteza fedha hakuna *impact* inayotokea katika kutengeneza barabara za vijijini. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Unafaa kuwa Magufuli.

**MHE. OMAR S. KWAANGW’:** Mheshimiwa Spika, ubora wa barabara vile vile ni jambo lingine. Sasa hivi tunaona barabara, hebu angalieni barabara za lami, toka hapa tu kilometa moja kama unaenda njia ya Dar es Salaam kwenye *round about* hapa na

wapi, barabara zimeumuka kama mikate, ubora gani huu? Nenda Dar es Salaam barabara zimeumuka kama mikate, tutaendelea na barabara za mikate mpaka lini Mheshimiwa Spika? Tunasimamiaje? Kama ni hao wahandisi washauri wasimamizi hawawezi kusimamia, fukuza sasa! Kwa nini unaacha barabara zinakaa zimeumuka kama mikate na wakati huo wale wanaochukua fedha wameshachukua, waliosimamia wameshaondoka, baada ya miaka mitano barabara ni mikate maana yake ni nini? Haina maana yoyote. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, naona muda umeshakimbia lakini niliseme kwa haraka. Mheshimiwa Rais aligawa Mkoa wa Arusha na akaunda Mkoa miwili, Mkoa wa Arusha na Manyara. Lakini barabara ambayo Rais aliihidi ambayo ndio ilikuwa inaunganisha Makao Makuu ya Mkoa yaani Babati na Wilaya za Kiteto na Simanjiro barabara ile inakwenda kwa kasi ambayo huwezi kuamini maana yake inaonyesha kwamba kulikuwa hata hakuna sababu basi ya kuunda huo Mkoa. Kilometa 17 hapa nimeona kwenye vitabu, kilometa 10 na mimi nimeangalia, Mheshimiwa Waziri wa Fedha ya kwako nimeiona, barabara zipi unatengeneza, Waziri wa Ujenzi nimeziona hapa, Naibu Waziri nimeziona hapa tukaangalie barabara ya kilometa 250 unaitengeneza kwa kusema kilometa 10, 10 ni miaka mingapi Makao Makuu ya Mkoa wa Manyara yataunganishwa na hizo Wilaya zake? Sasa hivi hakuna mambo ya utawala kule maana hata Mkuu wa Mkoa atakwenda vipi anakwenda kwa kupitia Pario, ni vitu vya ajabu.

**MBUNGE FULANI:** Sana.

**MHE. OMAR S. KWAANGW’:** Naomba Mheshimiwa Waziri wakati utakaposimama, ningependa kujua ni wewe uliyemnyima Waziri wa Fedha ili asitengeneze barabara inayounganisha Makao Makuu ya Mkoa wa Manyara kwenda kwenye Wilaya zake au ni nani au ni yeye Waziri wa Ujenzi ndio kwamba ameona haifai aweke hizo kilometa kumi tu, tunataka kufahamu hili. Maana lazima mambo haya tuyapime na kwa kuangalia uwiano, wapi tunatoa fedha na tunapeleka wapi na kwa sababu ipi. Zipo nyingine hapa zinakwenda mpaka vijijini, barabara za lami, barabara za nini, ile ni ya changarawe tu unawezaje kuweka kilometa kumi mahali ambapo Mkoa haunganishwi na kitu chochote ni kilometa 250 tena tunataka zijengwe tu kwa kiwango hicho cha changarawe, maana yake nini? Hii mipango inaainishwa vipi? Je, maana yake tuseme sasa mnatuonea, mnatupuuza au ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tungependa kufahamu hilo kabla sijasema naunga mkono, wiki hii bado tuna siku za kutosha kuwasiliana, wewe, mimi na Waziri wa Ujenzi tuone namna ya kuhakikisha kwamba fedha zinapatikana kwa ajili ya barabara hii, vinginevyo kwani mimi hapa peke yangu nikitamka kwamba siungi mkono Bajeti hii najua itapita lakini nimekuwa na mimi nimerejesta malalamiko ya Mkoa wangu. Kwa hiyo, hili ni jambo nalo la kuangalia san kwa undani huwezi kuunda Mkoa halafu huwezi kuuhudumia wala kuunganisha haina mantiki kabisa, hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, katika kuangalia Bajeti ya Serikali kwa ujumla wake, Serikali za Mitaa mnaipa shilingi bilioni 2 fedha za ndani, Serikali Kuu inachukua shilingi bilioni 358 uwiano uko wapi kama kweli tunataka kuimarisha Serikali za Mitaa? Hamna hata

kidogo. Fedha nyingi zinabaki kwenye Wizara na taasisi. Ni muda umefika kama tunataka kuimarisha Halmashauri za Wilaya tupeleke fedha kule fedha nyingi zinabaki huku maana yake nini. Nyingi ya fedha hizo zimepangwa kwenye sera na mipango, sera na mipango, sera na mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaweza kuangalia kwenye kitabu hiki cha Waziri sera na mipango imechukua kiasi kikubwa cha fedha badala ya kuelekeza fedha kule zinakotakiwa. Hii mipango ni lazima ibadilishwe. Matumizi ya Serikali ni makubwa. Tunakusanya mapato mengi zaidi lakini inaonekana na kasi ya kutumia nayo ni kubwa bila utaratibu, lazima tubadilishe jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hatua hii nitaunga mkono hoja nikiendelea kusubiri maelezo ya Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango na Ubinafishaji kuhusu barabara niliyoitaja.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kwa jinsi nilivyoona Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Bajeti hii ni nzuri lakini uzuri wa Bajeti hii ni kwamba mipango inayotuelekeza yote imepangwa mezani si mipango inayoonekana vijijini. Hili ndilo kosa na ndilo linatufanya tusiende kokote.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii ina tabia ya kusifia vitu ambavyo tunaona kwamba ni hatari, havitatusaidia, hili ni kosa. Tunasifu Wizara hii ya Madini juu ya uchimbaji madini. Napenda kusema kwamba hakuna idara inayotudhulumu wananchi kuliko hii ya madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi mimi niko hapa nimeletewa *fax* nyingi, watu wamepewa leseni wameingia vijijini kule Kamsamba hakuna hata barabara wanang'oa mawe na malori ya tani 30 hadi 70 kuwauliza wanasema sisi hatumjali mtu tunayemjua ni Waziri. Nimemwambia Waziri anasema nitachunguza sasa ni wiki mbili zinakwisha sina jibu. Hebu niambie, hivi hii Bajeti itatusaidia nini? Tunasifu watu ambao wanatudhulumu na wanaleta uchonganishi kwa watu vijijini! Sasa hili namngoja naye kwenye Bajeti yake, nakuomba Spika kwenye Bajeti yake unipe nafasi nimkumbushe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti hii nzuri, iliyopangwa kwa makini, haionyeshi usimamizi mzuri. Hivi tunazungumza juu ya mafuta, mafuta haya siku zote za nyuma tunazungumzia wakasema tubinafisishe bei itateremka yenyewe sasa tunakokwenda mnakuona? Leo sisi kule huwezi kulima kwa trekta kwa sababu heka moja sasa inaingia kwenye shilingi ishirini na kitu elfu, nani mkulima atakeyelimu? Nenda sehemu za Kapele, Ndarambo, Ilomba kwenye maeneo ya kulima na trekta, nani atalima kule? Hivi kweli tunataka kuzalisha au tunataka mzaha tu wa kuzungumza mezani? Halafu tunasema eti tunataka kuendeleza uchumi, tutaendelezaje uchumi katika hali hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunazungumzia juu ya nishati, nishati yenyewe huko vijijini nguzo zimesimama, mimi kule miaka kumi na zaidi sasa bado nyaya hazipo na tunajibiwa humu kila siku ooh tayari mambo, ngojeni, tutasubiri mpaka lini?

**MBUNGE FULANI:** Mpaka Yesu anarudi.

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Spika, na watu wenyewe wala hawaonekani kule. Unakwenda ofisini unaambiwa ooh katoka. Hivi kweli tutakwenda, tutafikia malengo haya wakati hatuna usimamizi wa kweli.

Mheshimiwa Spika, tunasema tutaleta mafanikio kwenye kilimo cha umwagiliaji mbona mvua nyingi zinanyesha, maji yote yanatiririka, kuna vijito vidogo ambavyo kwa kweli wananchi wangeelekezwa wangeweza kujenga na kuzuia vibwawa hata vidogo vidogo wakazalisha lakini hakuna anayewaza hilo watu wanafikiri kuchimba mabwawa ya magreda, greda hawalioni liliko.

Mheshimiwa Spika, watu wanasafiri kwenda kuona kwenye makampuni Ulaya magreda yalivyo, yote hii ni hujuma tu ya kutumia fedha bila utaratibu ili tubaki kuwa maskini. Lazima tuliangalie suala hili kwa makini na tuliepuke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia katika ubinafsishaji huu ni mzuri lakini ubinafsishaji huu lazima tuangalie. Kwa mfano *TAZARA* kutoka hapa mpaka kule mpakani Tunduma haiko kwa ajili ya Watanzania kwa sababu haisimami ikitoka huko mpaka Mbeya. Hivi *TAZARA* hii ni ya nani? Ilikuwa watu wanakuja wakihujumuhujumu wanakuja ooh, tuilinde, mtu alinde kwa faida ya nani? Lazima mambo mengine haya hata mkiibinafsisha huyo atakayeinunua huyo atakuja kulinda? Ni lazima masuala mengine haya tuwe tunaangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii *TRC*, reli hii inakwisha. Vyuma vinavyotumika kwenye mitarimbo pale vimechakaa ni vya wakati wa Mjerumani ndiye aliyevileta. Leo watu tumekaa tu kana kwamba hatuna watalaam, hatuna hata wanauchumi wanaoweza kuiendeleza? Wanasema wataiua au mtaikodisha. Hivi kweli atakayekodi si ataong'oa yale mabovu yale; watu wa kutoka huko Magharibi watasafiri na nini wakati barabara ya kupitia Singida haijaisha? Mnataka kutuletea mgogoro bure tu na fitina na watu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hata kuwaweka hata hawa wanaonung'unika kuwa eti wao wakichukua Serikali wataiweka vema, wataiweka vema wana nini hawa malofa kabisa, wataleta nini? Ni maneno ya ulaghai tu ya kuvuruga akili ya watu bure tu. Chama kimefanya mambo makubwa, Serikali imefanya mambo makubwa na wao wamefaidika na wananufaika, hii ni shukrani ya punda kuwa mateke. *(Makofi/Kicheko)*

Naomba wenzangu hawa wa Upinzani muwe mnaona tatizo ni nini lakini kukitokea kitu pengine cha kula kula hivi ndio wako mbele kupokea lakini sasa tutakwenda wapi katika kufanya nchi hii iwe ni nchi imara na yenye kuelewaka? *(Kicheko)*

Nawaomba wananchi wawaone hawa wanaotangaza kuwa watafanya kitu. Kama walivyosema wenzangu wengi hawa wanaosema watafanya kitu ndio hawa waliovuruga wakatengenezesha makaratasi, noti mpaka watoto wakawa wanaweka kwenye soksi leo ndio wanasema wataleta uchumi? Kwa nini walipokuwa na nafasi hiyo hawakufanya uchumi ufae kama sio ulaghai na kudanganya watu katika nchi hii bure? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba tuache udanganyifu na wananchi tuwaambie wasije wakalogwa na wadanganyifu wa namna hii wakafikiri watapata, kumbe wamepatikana. Huu ni mtego mkubwa na mwaka huu Mungu atusaidie maana liko balaa kubwa linaweza kutokea hapa. Lakini wana CCM tunasema Mheshimiwa Jakaya Kikwete ndio Rais wetu kuanzia mwezi Novemba, 2005 na Makamu wake atakuwa ni Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein. Anayebisha na abishe lakini hatumkatazi kusema. Huwezi ukamkataza nzi kurukia kwenye ugali kama umepoa lakini tunasema tunaruhusu na Rais wa Zanzibar tuna hakika atapita hata wakifanya lolote lile, atapita tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwananchi gani wa Zanzibar asiyeona kazi aliyofanya Mheshimiwa Amani Abeid Karume mpaka leo aje alaani yale mazuri aliyoyatenda apendelee ya hawa ambao hakuna walilolionyesha! Jana wanazungumza kwenye *TV* eti wao ngangari pale pale. Sasa ungangari huu tunaomba wenzetu wa kule Unguja waelewe na wawe tayari kuung'olea mbali ungangari huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa tunaloliona ni mbolea. Mimi Wilayani kwangu kule nenda hata kule Msangano watu wa Sweden walikuja wakapima wakasema kungekuwa na bomba kubwa wakatega kwenye maji ya maporomoko pale kule mbele wangechimba mifereji tu na kuipeleka kuzalisha kilimo kizuri kule. Lakini tangu ametoka huyu kabla ya Uhuru mpaka leo hakuna linalofanyika. Hivi hawa wataalam wetu hawana uwezo wa kuona hilo? Si ni kuchukua bomba tu, chukua hata haya yanayotumia maji hapa nenda jengea pale maji yakienda ng'ambo watu wanachimba mifereji wanaelekeza kwenye kilimo. Inawezekana kabisa ila watu wetu wamekaa basi ni kudai posho, nini, hatuendi! Unadai posho kwenye umaskini, hatuendi mahali.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine tuache urasimu. Mbolea ya ruzuku ipo lakini leo nenda vijijini hakuna, iko wapi mbolea? Kule kwetu mwezi unaokuja watu wanaanza kulima, mwezi wa tisa wanapanda, wa kumi inanyesha mvua mazao yanaota leo mbolea haieleweki iko wapi na watu tunasema tuzalishe.

Mheshimiwa Spika, hii ya kutangaza soko sijui leo mahindi gunia shilingi 18,000 wanayasema watu, haya mahindi wanayosema kule kwetu hivi sasa debe ni shilingi 1,000 hayo ni mahindi ya mwaka jana, Malawi wana njaa wameagiza chakula kutoka Afrika ya Kusini pale sisi ndio tunaopakana nao Serikali imeshindwa kuona na kukubaliana nao si wangechukua tu mahindi pale wakaingiza fedha za kigeni! Hivi nalo hili linahitaji kwenda shule ya ajabu? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, elimu uliyonayo kama haiwezi kusaidia watu ni upuuzi tu wala haina maana yoyote na huna haja ya kusema umesoma. Elimu ya vyeti sasa imekwisha elimu inayotakiwa ni ya utendaji kazi. Hilo tukubaliane. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa unakwenda kumweka mtu mbolea itoke huku Mkoani wapendekeze watu wao, wale watu ndio wasafirisha mbolea kwenda Mbeya, Mbeya nako wapendekeze watu walete kule Mbozi, huu ni urasimu tu hatutakwenda mahali hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, halafu mikopo tunayotoa hii kwa kweli ni sisi tunataka kujidhalilisha tu. Tunasema tukopeshe wafanyabiashara wadogo wadogo, wafanyabiashara wadogo wadogo ni kweli wanapata mikopo kutoka Benki ya *NMB* lakini biashara yao ni kuuza nyanya wang'ang'aniana nyaya kule, wanalangua, nao wanazileta wanapandisha bei, mlaji wa mwisho ndiye anayeumia. Wala hatuzalishi kuongeza chakula. Kwa nini tusimkopeshe huyu mzalishaji wa nyanya akanunua mbolea hata heka moja akapanda nyanya akafaidika, si itakuwa ni nafuu? Kwanza chakula kitapatikana kwa wingi na cha kutosha na bila matatizo. Leo tunaanza tena kukopesha wafanyabiashara hawa ambao hawana hata mashamba wala hawajui yanakotokea?

Mheshimiwa Spika, ukienda kila mji hata hapa Dodoma nenda huko pembeni pembeni wako watu na magunia wanapokea mazao kutoka kwa watu. Wanakusanya mchicha wanakuja kuuza hapa badala ya kuwakopesha wale walima mchicha angalau mbolea hata mfuko mmoja wamwagie wazalishe mchicha wa kutosha ili uwe na bei nafuu ili watu wote waweze kupata hiyo michicha lakini watu hawataki kuona hilo.

Mheshimiwa Spika, lingine sijui tuna tatizo gani au ni tatizo la ngozi au la maisha au nini sijui? Leo hii tunaamua mambo yetu mengine hayatusaidii sana. Leo tunasema kujenga miji kufanya nini, Mji Mkuu hapa hivi kweli tunalionga hili suala? Mbona ilipojengwa Nkhungu kule kulipelekwa barabara za lami kuonyesha lakini nenda Ipagala huko hata kupita kwa baiskeli ni tatizo lakini watu wanadaiwa fedha za *property tax*, hivi huu si wizi huu? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hivi Serikali imejiingiza hata kuibia watu maskini hakuna *service* yoyote, unakwenda kuwatoza maana yake nini? Hivi nani anayetoza hizi hela, hana msaada, hana *sewage system*, hana barabara watu wako kule Ma-sister na shule yao wanaweka changarawe kwenye barabara wenyewe, leo tuna Manispaa hapa sijui nini inafanya kazi gani, hilo si eneo lake? Watu sasa tubanane anayeonekana hawezi kuwajibika basi atupishe, aondoke hatuwezi kuendelea hivi na tunaomba Serikali ya Awamu ya Nne hii ifagie nyumba iwe safi ili tuweze kwenda mbele. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge ndio tumefikia mwisho wa kipindi cha asubuhi cha kikao cha leo. Mheshimiwa Naibu Spika, amesafiri kwa hiyo, kipindi cha mchana kitaongozwa na Mwenyekiti, Mheshimiwa Eliachim Simpassa. Sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

*(Saa 06.58 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa (Mhe. Eliachim J. Simpassa) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Kikao chetu kilichoanza asubuhi kinaendelea.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nikushukuru wewe pamoja na Mheshimiwa Spika kwa kunipanga wa kwanza kuzungumza mchana huu, kwanza nilikwisha toa rambirambi zangu na pia vilevile nilikwisha toa hongera kwa wale wenzetu ambao wamechaguliwa katika nafasi mbalimbali za kugombea hapo baadaye. Nijielekeze moja kwa moja katika uchangiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nipende kumpongeza sana Waziri wa Fedha kwa Bajeti nzuri, ni tabia yake ya kila mara kuangalia maeneo yenye kero na kuyachukulia hatua, nampongeza sana kwa miaka hii mitano ambayo amekuwa Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Waziri, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, kwa kweli kwa kufuatilia mwelekeo wa maendeleo ya nchi yetu ni kijana ambaye ana upeo mrefu wa kuona kwa upana na kuona tunakokwenda na kutoa maelekezo mazuri. Nampongeza sana.

Pia vilevile niwashukuru Manaibu Waziri wote wawili wa Wizara hii ya Fedha kwa kazi nzuri na niwashukuru na kuwapongeza sana wafanyakazi wote wa Wizara hizi mbili ambazo kwa kweli mimi naziita Wizara Dada na Mama, huwezi ukazigawa lazima zitembee pamoja na zipendane ndiyo maendeleo yatashabihiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nichukue nafasi hii hasa kwa upande wa kuishukuru na kuipa pongeza sana *TRA, TRA* wamefanya kazi nzuri ya kuondoa aibu ya utegemezi kwa kiasi fulani. Bajeti ya nchi hii mimi sasa niko katika Bunge hili nakaribia kumaliza miaka kumi. Mwaka 1995 tunaingia katika Bunge hili kwa wale wenzangu ambao tulikuwa nao ni mashahidi, ni ukweli kwamba Bajeti ya Serikali ilikuwa chini sana lakini leo tunazungumzia na wakati huo wafadhili walikuwa wanachangia asilimia 60 ya Bajeti hii, hivi leo Bajeti ya nchi hii inachangiwa kwa asilimia 41. Kwa hiyo, tumebadilisha mwelekeo, basi ndege hii badala ya kuanguka sasa inapaa sisi kama Wabunge ni kuwapa moyo wenzetu ambao wanatekeleza sera za Chama Cha Mapinduzi ambazo ndiyo sera sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sipendi sana kujisifu hasa kwa yale mafanikio ya Chama Cha Mapinduzi, lakini aliye na macho haambiwi tazama katika suala la mabadiliko ya uchumi wa nchi hii kwa mtu aliyekuwepo humu Bungeni na aliyekuwa na

nchi hii kwa kipindi chote cha Rais Benjamin Mkapa huhitaji kwa kweli kumwambia tazama. Sasa kama watu wa nje wanasifu sembuse sisi ambao tupo humu ndani.

Mimi nakumbuka mfano mzuri tulichokuwa tunalipwa *Jimbo allowance* ilikuwa shilingi 5,000/= tunaingia humu ndani wala si siri lakini leo unaweza pamoja na kwamba hakitoshi ukatembelea Jimbo lako vizuri na ukaangalia wapiga kura wako, ukazungumza nao kwa heshima, siyo kama ile ya mwanzo kwa hiyo, hakuna asiyeona kwamba maendeleo yapo na sisi wote tunakubali kwamba Bunge la leo siyo Bunge la mwaka 1995. Kwa kweli maendeleo mazuri na maendeleo makubwa na ninaipongeza Serikali kwa hilo. *(Makofi)*

Hatuhitaji kutaja maeneo kwa sababu yameshatajwa na wenzangu, mafanikio katika miundombinu unayaona ukianzia Dar es Salaam mpaka Mwanza kuelekea Bukoba kwa bahati nzuri mimi nimekwenda mpaka maeneo ya Ngara, huwezi ukaamini nchi inaonekana inaibuka, barabara zinajengwa, sasa kwa sababu wenzetu Wapinzani ni tabia na ndiyo mchezo wenyewe hata kikiwa kizuri hukisema ni kibaya basi hatuwashangai, ni haki yao waache waseme lakini tunasema bado tutaendelea kuiongoza nchi kwa sababu iko katika dira ya halali na ya haki katika suala la elimu huhitaji kuelezwa, katika afya huhitaji kuelezwa, katika kilimo yako mafanikio inawezekana hatuyaoni moja kwa moja lakini ukiangalia maelezo ya Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji ni kweli kwamba kuna kukua inawezekana kuna mazao mengine tumerudi nyuma lakini kuna kukua kwa kiasi fulani sasa kama alivyosema Waziri wa Fedha na kama wote walivyochangia kwamba huu ndiyo mwisho wa Serikali ya Awamu ya Tatu tunakwenda Awamu ya Nne wametoa mawazo yao na wametoa ushauri ambao Awamu ya Nne itaanza.

Mheshimiwa Spika, hakuna watu wazuri kama hawa ambao wanatoa mwelekeo na wanaeleza matatizo yaliyopo na wanakubali kwamba hawajafika mwisho ndiyo mwanzo wa kazi yenyewe na kweli huu ndiyo mwanzo wa kazi yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo ya muhtasari mimi niseme kwamba nitaanza kwanza kueleza yale ya kwangu na haya ninayozungumza si kwamba sikufurahishwa na Bajeti hii, naikubali asilimia mia moja na ninaipongeza ni nzuri, haya ninayoshauri ni ya kuboresha na ni kuboresha katika msingi kwamba hakuna kitu kinachoumbika kisicho na kasoro, chochote kinachoumbwa lazima kiwe na kasoro zile zisizidi uzuri, mimi naamini Bajeti hii nzuri kasoro zake ni ndogo ndogo na ni za ushauri.

Sasa nianze katika eneo ambalo linanihusu mimi mwenyewe katika Jimbo langu namuomba sasa Waziri wa Fedha, leo nimemwona mara mbili, tatu. Eneo la kutenda haki kwa ajili ya kukipanua Chuo cha Uongozi wa Mahakama ni eneo muhimu sana kama kuna eneo ambalo bado hatujafanya vizuri ni eneo la Utawala Bora hasa katika suala la utendaji wa haki, inawezekana kuna transparency kiasi fulani katika uongozi wa nchi lakini tukienda katika utendaji wa vyombo vya kutoa haki kwa kweli bado tuko nyuma. Bado tunahitaji mahakimu wa kutosha ili hukumu zitolewe mapema, haki itendeke mapema, lakini inaelekea mpaka leo hii Serikali haijaona umuhimu wa Chuo hiki, tumekubaliana kwamba ili tutende haki ni budi Mahakimu wazalishwe wengi, wasome wengi, wawe na upeo mzuri waelewe kutenda haki na kuzijua sheria vizuri lakini siyo



hali iliyopo na inaelekea hakuna mpango mzuri ambao kwa kweli utatuvusha katika hali tuliyo nayo kwenda katika hali ambayo ni nzuri.

Mimi naamini kwa sababu chuo hiki kimekwishaweka *Master Plan* yaani mpango kabambe, mimi naamini kutokana na mpango huo sasa Serikali inaacha madaraka ni vizuri ingejenga msingi kwa kutenda haki kwa wananchi wetu. Naomba na ninamsihi sana Waziri wa Fedha atamke tufanye nini katika kukisaidia chuo hiki ili kifanye vizuri na Mahakamu wawe wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo matatizo pia katika polisi, kweli tuna Chuo cha Polisi lakini bado haki kwa wananchi haijatangenda kila siku unasikia kuna rushwa pale, matrafi na nini matatizo haya yanakuwepo kwa sababu mbili muhimu.

Kwanza askari wenyewe hatujawaangalia vya kutosha ni kweli mishahara ipo tunawalipa lakini hebu tuwalipe vizuri ili mtu anapofukuzwa kazi aone uchungu, unajua kama mtu anahangaika kwa siku nzima mwisho wa mwezi anaondoka na kitu hakiridhishi hakitoshi basi kwa vyovyote hata kama ataomba hongo anaona hakuna sababu lakini akipewa kahongo kadogo alinganishe na kile anachokipata ataacha hongo Kwa sababu anajua akiharika kufukuzwa kazi basi itakuwa amewaangamiza watoto wake.

Mimi nashauri vyombo vyetu vya kutenda haki, Polisi na Mahakama waandaliwe mipango mizuri ya malipo na waweze kufanya vizuri ili waepukane na masuala ya rushwa na haki itendeke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nije sasa nichangie maeneo ambayo pengine naona ni vizuri nitoe mawazo yangu, Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji ameeleza hasa katika ukurasa wa 56, mimi Bajeti ya kaka yangu Mheshimiwa Basil Mramba, sina ugomvi nayo kabisa amejitahidi, amepunguza maeneo yale yenye kero yote na nafikiri ameyamaliza, Serikali ijayo itakuwa inatamba tu kuimarisha katika maeneo yale ambayo ni kupiga msasa mimi nasema hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nijielekeze sasa katika misingi ya uchumi ujao baada ya kuona kwamba sasa tunakwenda vizuri ukurasa wa 56 umetaja kwa kweli kukuza uchumi na kupunguza umaskini Tanzania MKUKUTA, ni *approach* ambayo ni ya kweli na ni muhimu huwezi ukazungumzia umaskini bila kukuza uchumi sasa ninaamini sasa gari hili limerudi barabarani na linajiseti katika mwenendo mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina wasiwasi kidogo katika eneo hili tumezungumzia MKUKUTA lakini ukiangali Bajeti kwa kweli hakuna direct relationship ya MKUKUTA yaani wa dhati kabisa unavyoona kwamba MKUKUTA katika eneo hili tuna uhakika mpaka kufikia mwaka fulani eneo la umaskini utapungua kwa kiasi hiki. Nasema hivi ukiangalia ukurasa wa 58 tumezungumzia *the Tanzania mini tiger plan*, mimi kwa bahati nzuri nimetembelea mara nyingi sana hizi nchi za Asia ambazo ndizo *Tiger Nations*, Thailand, Malaysia, Indonesia na hapa tumetaja kwamba tunataka *a mini tiger plan*. Lakini ukiangalia Bajeti yetu bado hatujajielekeza kama tunajiandaa kuingia

katika hiyo *plan*, kwa mfano tumezungumzia suala la masuala ya *ZES, SEZ, Special Economic Zones*.

Mimi naamini bandari kama ya Tanga ambayo inazungukwa na mikoa yenye uwezo mkubwa tukiamua kwa sasa hivi tukaanza kutenga hela kwa ajili ya *infrastructure* kutokana na mapato yetu ya ndani tunaweza kujenga msingi unaoeleweka, tumetaja humu lakini hakuna mpango unaoonekana hivi tumetenga kiasi gani hata angalau cha kuanza ukanda mmoja ambao uko tayari, maana ukizungumzia bandari ya Tanga pale tayari Katani ipo, Kahawa ipo, uchimbaji wa Madini Tanzanite upo.

Kwa hiyo, *Special Economic Zone* itakayowekwa pale na gharama yake ni ndogo kwani umeme upo, maji yapo ni kitu ambacho hakijapata *address* kimetamkwa lakini hakikuzingatiwa katika Bajeti sasa kama hatutafanya hivyo tutatamka maneno mazuri sana katika mambo ya kuiongoza nchi lakini tukifika mahali hatuna tulipoegamea kwa hiyo, kila mwaka tutatoa Bajeti ya matarajio lakini tutashindwa kuwa na Bajeti ya utekelezaji na utekelezaji katika nchi maskini kama ya kwetu lazima twende hatua kwa hatua, leo mafanikio makubwa tuliyoyapata kwa kuweka bilioni moja laki nane kwa ajili ya ujenzi wa barabara kila mtu anaamini tunafanya kazi kubwa kuanzia Mtwara tunaelekea Mwanza kwa hela zetu siyo kidogo ni kitu kikubwa. (*Makofi*)

Sasa kama tumeanza huko ni vizuri pia katika maeneo haya ambayo ni *plans* zilizowakomboza wenzetu, leo ukienda Malaysia, Malaysia imekomboka kwa ajili ya kulima michikichi na hizi *decorticators* ziko kule vijijini kwa sababu umeme upo kwa hiyo tukiamua kuchagua maeneo machache tukapeleka *resources* huko moja kwa moja tutajenga ajira kwa sababu jibu ambalo sasa hivi kama hatutajitoa itakuwa ni tatizo kubwa sana ni uwezo wetu wa kujenga ajira kwa vijana na uwezo wa kujenga kwa vijana siyo plan za lelemama ni mipango ambayo inakuja polepole inaibua na wao wanazama katika mipango hiyo polepole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi uka-*process* kuajiri vijana kwa miaka miwili ukamaliza lakini lazima uonyeshe lengo, leo tungetengeneza *special economic zone for that matter* hata hii *EPZ* hatujawekeza katika hii *EPZ* kusema ule ukweli mimi ni mfanyabiashara lakini ni kweli kwamba tumezungumza tu kwa maneno kwa miaka mitatu iliyopita tukizungumzia *EPZ* lakini hatujawekeza katika *EPZ* kwa sababu kwanza katika mambo haya lazima Serikali ikubali yenyewe kuwekeza ile miundombinu, mtu atakuja kuweka duka lake akikuta kuna kila kitu kipo Bandari ipo hata gharamika kwenda mbali, anaita malighafi anamaliza kuzalisha anapeleka nje na uchumi wan chi hauwezi kwenda na hatuwezi kupata maendeleo katika yote ya MKUKUTA kama hatutakuza uwezo wa kupata fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ndilo la mwisho ninalotaka kuchangia *EPZ* na *Special Economic Zones* hizo ndizo *pre-vocal* ya maendeleo kama hazikuzingatiwa hizo mimi nina uhakika maendeleo yetu ni *cosmetic* hivi leo tunasema tuna fedha nyingi za kigeni ni kweli, tunazo lakini *cosmetic* hizi ni fedha za misaada, hizi ni fedha ambazo kwa kweli siyo zetu tunaletewa lakini tutakapoweza kuzalisha sisi wenyewe kwa ku-*export* hapo ndiyo tunasema uchumi utakuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nashauri na napenda kupendekeza sana kwamba Bajeti hii ni nzuri lakini sasa haizingatii kuirusha nchi katika maeneo ya ku - *boost* uchumi kama vile hizo *Special Economic Zones* au *EPZ* ninaamini Bajeti ijayo itazingatia hayo hatua kwa hatua na nina uhakika tutaleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimalizie hapo kwa kuunga mkono hoja na kuisifu sana Serikali kwa kazi nzuri ya Serikali ya Mheshimiwa Benjamin Mkapa. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. MUSA A. LUPATU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi jioni ya leo ili niweze kuchangia hoja hizi mbili za Mawaziri wa Fedha na Waziri wa Mipango na Ubinafishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijatoa mchango wangu napenda nitoe pole kwa wananchi wa Jimbo la Kilombero kwa kufiwa na Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mbunge wao, nawaomba wavute subira na Mungu aiweke roho yake pema peponi. *Amin.*

Pili nichukue nafasi hii kuwapongeza wenzetu ambao wamechanguliwa na Chama Cha Mapinduzi kuipeperusha bendera ya Chama Cha Mapinduzi katika Uchaguzi Mkuu ujao, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Mheshimiwa Amani Abeid Karume na Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, nawapongeza sana kwa kuteuliwa na Chama ili kupepeza bendera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu napenda nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa kumpongeza Mheshimiwa Basil Mramba na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya kwa kipindi chote cha miaka mitano ambayo tumekuwa nao kama Mawaziri. Matayarisho ya Bajeti yao ni mazuri na kwa kweli inastahili sifa. Niwapongeze vile vile wasaidizi wao Manaibu Waziri wa Wizara ya Fedha, Makatibu Wakuu wa Wizara hizi zote mbili na wataalam waliowasaidia katika matayarisho ya mpango pamoja na bajeti ya mwaka huu, nawapongeza sana kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza kwa sababu wamepanga Serikali itumie trilioni 4.2 katika mwaka huu wa fedha na katika mgawanyo wake inadhihirisha dhahiri kwamba mgawanyo huu kwa kweli unalenga kwenye kuondoa umaskini, tumeona kabisa kwamba katika kutenga fedha za matumizi asilimia 50 ya Bajeti ya shilingi trilioni 4.2 yanaelekezwa kwenye vipaumbele ambavyo vimeainishwa katika Mpango wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini yaani MKUKUTA. Jambo hili linaonyesha dhahiri umahiri wa viongozi hawa wa kuipeleka nchi pale tunapotaka kwenda kuondoa umaskini, ninawapongeza sana kwa kazi hiyo. (*Makofi*)

Baada ya maelezo hayo naomba nichangie maeneo machache ambayo kwa kweli ni kudhihirisha tu kwamba wamefanya kazi nzuri na nataka nitamke rasmi kwamba naunga mkono Bajeti hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze na viashiria vya ukuaji wa uchumi, napenda niwapongeze kwamba Tanzania imepata mabadiliko kati ya miaka 1995 na mwaka 2005, katika Pato la Taifa tumeona dhahiri ongezeko la ukuaji wa Pato la Taifa kufikia asilimia 6.7 mwaka 2004 ukilinganisha na asilimia 5.7 ya mwaka 2003.

Ongezeko hili linaonekana kabisa kwamba tunakwenda vizuri na pato hili kwa kweli limeongezeka vya kutosha si kwa asilimia tu hata kwa namba inaonekana dhahiri kwamba ongezeko ni kubwa. Mwaka 1995 Serikali ilikuwa inakusanya shilingi bilioni 25 kwa mwezi lakini hadi kufikia sasa hivi tunavyozungumza Serikali inakusanya wastani wa shilingi bilioni 145 kwa mwezi, ongezeko hili ni karibu mara sita katika miaka kumi hii ni kazi kubwa na nzuri.

Pia nawapongeza kwa kuongeza mauzo ya bidhaa za nje kwa asilimia 32.6 haya ni mabadiliko mazuri, sasa nilikuwa najaribu kuangalia viashiria hivi vya uchumi na kuvilinganisha na wenzetu katika nchi zinazoendelea, nchi zilizoendelea pamoja na Afrika tukijilinganisha na Tanzania. Niliangalia nikaona kwamba kama walivyoeleza pato la dunia limeongezeka kutoka asilimia 4 mwaka 2003 hadi asilimia 5.1 mwaka 2004, pato la nchi zilizoendelea limeongezeka kutoka asilimia 2 hadi asilimia 3.4 katika miaka hiyo na Pato la nchi zinazoendelea limeongezeka kwa asilimia 6.4 hadi asilimia 7.2 na Pato la Afrika limeongezeka kutoka asilimia 4.6 hadi asilimia 5.1 mwaka 2003/2004 na Pato la Tanzania limeongezeka kutoka asilimia 5.7 hadi asilimia 6.7, sasa nini maana ya ongezeko hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama pato la nchi zilizoendelea inaonekana kwamba halikuongezeka kwa kasi kubwa lakini tukumbuke kwamba kasi ya wenzetu ya kuongezeka kwa uchumi inafikia karibu juu, karibu ya mwisho au kwenye *sealing* kwa hiyo, ni dhahiri kwamba ongezeko lake haliwezi kuwa la kasi kama lilivyo letu. Lakini kwa jumla kwa mapato halisi ongezeko lao ni kubwa kuliko ongezeko ambalo tumelipata sisi linaloonekana ni kubwa kwa hiyo nilitaka kutoa angalizo hapo kwamba tusije tukabweteka tukafikiria tumewapita Pato la Afrika na tumepita nchi zilizoendelea na tumepita pato la dunia kwa kuongezeka kwa kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni *rate* tu lakini takwimu halisi za kwetu ni ndogo kuliko za nchi zilizoendelea kwa hiyo, nadhani tu ni vizuri sasa tukafanya bidii kuhakikisha kwamba tunaongeza zaidi msukumo katika uzalishaji kwa bidhaa mbalimbali katika viwanda, kilimo kusudi pato letu liweze kukua kwa kiwango kikubwa zaidi na hatimaye tufikie asilimia 10 ya ongezeko kama tunavyotakiwa katika kuendeleza uchumi kwenye malengo ya kimataifa ya kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimetajwa hapa sababu za ongezeko la pato, zimetajwa kwamba sababu zilizoacha pato limeongezeka dunia nzima pamoja na sisi Tanzania ni kuimarika kwa uchumi katika dunia nzima na pili kwamba imekuwapo misamaha ya madeni kwa hiyo zimekuwepo fedha nyingi kidogo kwa nchi zinazoendelea katika kuzitumia badala ya kulipa madeni.

Lakini liko jambo muhimu sana kwa Tanzania ambalo nadhani sababu muhimu ya kuichambua hili ongezeko la uzalishaji katika Sekta ya Kilimo nadhani hili ndiyo jambo muhimu sana kwa watanzania kama tunavyojua pato la kilimo, kilimo kinachangia asilima 49 ya Pato la Taifa, kilimo kinaingiza asilimia 66 ya pato la fedha za kigeni na kilimo kinatoa ajira kwa Watanzania asilimia 70 kwa hiyo, ni dhahiri kwamba kilimo kina umuhimu mkubwa kabisa kuliko sekta yoyote hapa nchini. Kwa hiyo, nilitaka nizungumzie juu ya kilimo kwa umuhimu wake.

Napenda niipongeze Serikali nianze kwa kuipongeza tena kwa kutimiza lengo la kimataifa la kutaka kilimo kitengewe angalau asilimia 10 ya bajeti ya Serikali. Mwaka huu nimeona kwamba kilimo kimetengewa karibu asilimia 11 ya Bajeti ya Serikali, nawapongeza sana kwa kuongeza Bajeti hii ya kilimo. Lakini tuitazame imeongezeka kwa kiwango gani, matumizi ya kawaida yameongezeka kwa asilimia 56 kati ya mwaka huu na mwaka wa fedha unaofuata, miradi ya maendeleo imetengewa fedha asilimia 84 zaidi kuliko mwaka jana kwa hiyo ni ongezeko kubwa sana katika sekta hii ya kilimo ukichukua Wizara yenyewe ya Kilimo kwa hivyo Serikali inaonyesha Seriousness au umakini katika kutenga bajeti na kuangalia sekta za uchumi za kipaumbele katika kuondoa umaskini, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Lakini nilikuwa natazama takwimu halisi, ni kweli ongezeko ni kubwa asilimia 56 matumizi ya kawaida, asilimia 84 matumizi ya miradi ya maendeleo lakini takwimu halisi zinaonyesha kwamba matumizi ya kawaida yameongezeka kutoka shilingi bilioni 35 mwaka jana au mwaka huu unaokwisha hadi bilioni 56 mwaka unaofuata. Miradi ya maendeleo imeongezeka kutoka bilioni 64 hadi bilioni 118 sasa kasi ni kubwa ya ongezeko lakini takwimu bado zinaonyesha kwamba kiwango hiki hakitoshi kwa kufufua na kuendeleza kilimo kwa kasi ambayo tunatarajia kwa hiyo naiomba Serikali katika kupanga mipango ya miaka inayofuata iongeze kasi pamoja na kuongeza kiwango chenyewe cha fedha ambazo zinaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa nizungumze mambo machache yanayohusiana na uboreshaji wa kilimo. Kama nilivyosema kilimo ndiyo uti wa mgongo, kilimo ndiyo kinachojiri watu wengi na hivyo hatuna budi kukiimarisha zaidi.

Sasa nilikuwa napendekeza mambo machache yafuatayo; sasa hivi bei ya pembejeo za aina yote bado iko juu na wananchi hawawezi kuimudu kwa hiyo, nilikuwa napendekeza na kuiomba Serikali izidi kuongeza ruzuku katika zana za kilimo, mbolea na mbegu kusudi hizi ziweze kupatikana kwa bei nafuu, lakini natoa tahadhari kwamba tunaweza tukaweka ruzuku, tunaweza tukaondoa kodi lakini bei kwa mkulima ikabaki pale pale kwa sababu wafanyabiasha wanayotabia ya kupenda kupata faida zaidi kuliko kumwagalilia mlaji. Ndugu zangu wafanyabiasha naona wananitazama hili ni jambo la kweli hata mimi ninafanya biashara. *(Makofi)*

Kwa hiyo basi, ni vizuri Serikali ikaweka mkakati maalum kabisa kwamba inapopunguza kodi au inapotoa kodi, inapotoa ruzuku punguzo lile linakwenda moja kwa moja kwa mlengwa ama mkulima ambaye anahusika.

Pili, nawaomba kabisa Wizara inayohusika iweze kuongeza kiwango cha uzalishaji wa mbegu bora kwa sababu ni tatizo kubwa sana tulionalo juu ya mbegu kwani wakulima wetu bado wanatumia mbegu za kizamani tuna kama asilimia 10 au 11 ya mbegu tunazohitaji za kisasa, kwa hiyo, ni dhahiri kwamba bado kilimo chetu kitabaki nyuma kama Serikali hailioni hili na kuliwekea mkazo maalum.

Tatu, huduma za ugani, hapa ndiyo tuna tatizo kubwa, nimezungumza nadhani mfululizo kwenye Bajeti kwamba huduma za ugani hazilingani na matarajio ya wakulima mpango uliopo sasa ambao unatumika huwaweka Maafisa Ugani ama wa Kilimo ama wa Mifugo chini ya Wakurugenzi wa Wilaya bado una mushkeli, ni vizuri Serikali ikautazama upya kuangalia ni jinsi gani mpango huu au mfumo huu unaweza kuboreshwa ili huduma za ugani zimfikie mkulima kwa kiwango kikubwa. (*Makofi*)

Utafiti unaonyesha kwamba *extension contact* ama huduma ya mara kwa mara kwa mkulima inaongeza asilimia 6 ya uzalishaji wa mazao kwa hiyo *extension* ni jambo muhimu na ni lazima Serikali ilitazame upya ili mkulima aweze kukutana vya kutosha na kupata huduma kutoka kwa Maafisa Ugani.

Nne, uwepo uhusiano wa kutosha kati ya viwanda na kilimo ili uzalishaji wetu wa mazao uendeane na uzalishaji katika viwanda, ni vizuri tukaliangalia kwa mfano pamba.

Sasa hivi pamba nyingi inakwenda nje ikiwa ghafi, lakini zipo nchi ndogo kama Taiwan ambazo zinatumia pamba na zinatimia nguo kama sehemu kubwa ya uchumi wao. Kwa hiyo, sisi tungeweza tukaangalia viwanda vyetu vifanye nini ili viweze kulisha pamba yote tunayozalisha kusudi tuisafirishe pamba nje, lakini tuuze bidhaa ambazo zimetengenezwa kama nguo ama nyuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nawaomba kabisa tuweke mazingira mazuri ya ukopeshaji. Hivi sasa tumeambiwa zipo fedha nyingi sana Benki lakini hazipatikani kwa wakopaji kwa sababu hawana dhamana. Kwa hiyo, naomba tuweke hali nzuri ya ukopaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**MHE. SULEIMAN A. SADIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote na mimi naomba nianze kwa kutoa pole kwa msiba uliotokea wa ndugu yetu Mheshimiwa Kiwanga. Kwa niaba ya wananchi wa Mvomero na mimi mwenyewe tulipokea msiba ule kwa masikitiko makubwa na tunamwomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kusema naunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, naomba niungane na wenzangu kwa kutoa pongezi nyingi sana kwa Chama cha Mapinduzi kwa kumaliza n'ngwe ya kwanza kwa uteuzi wa Mgombea wa Urais na Makamu wake. Nawapongeza sana Mheshimiwa

Jakaya Mrisho Kikwete, Dr. Shein pamoja na Mheshimiwa Rais Amani Karume. Kwa kweli uteuzi wao umekuwa ni faraja kwa Chama, lakini pia ni faraja kwa Watanzania wote hususan kipindi hiki cha uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nami nichangie mawili matatu katika bajeti hii. Lakini mwanzo kabisa, naomba nianze kuwapongeza Mheshimiwa Mramba na Mheshimiwa Kigoda kwa hotuba zao nzuri walizoanzia kwenye Kamati yetu ya Fedha na Uchumi na hatimaye wakatuletea hapa Bungeni. Kwa kweli ni bajeti ambayo haina mzigo wowote kwa wananchi wetu katika Taifa letu, ni bajeti ambayo ni ya kisayansi na ni bajeti ambayo imekwenda na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya nyuma, tulizoea bajeti zenye mambo mengi sana ya kuongezaongeza viwango vya kodi mbalimbali, lakini sasa naona Tanzania tumeanza ku-*take off* vizuri sana na kwa bajeti hii inaonekana huko tunakokwenda ni kuzuri kweli kweli. Mimi nawapongeza wote walioshiriki kuandaa hotuba hizi nzuri za bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa kwanza kabisa, naiomba Serikali iangalie suala zima la mapato na matumizi. Miaka ya nyuma tulikuwa tunaangalia zaidi suala hili. Sasa hivi mapato yetu yameboreka sana, lakini kila mtu hata mimi na wengine kadri tunavyopata mapato mengi ndiyo tunavyotumia zaidi. Sasa hivi katika bajeti hii inaonekana matumizi ya kawaida ni makubwa kuliko matumizi ya maendeleo. Suala hili ni vyema likafanyiwa kazi vizuri sana na wataalam wetu na tukaboresha sana eneo hili kwa sababu bado tuna matatizo mengi na tunahitaji bajeti kubwa ya maendeleo sio bajeti ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi yetu ya kawaida yamepanda mno ukilinganisha na miaka ya nyuma. Waziri huyu ni Waziri wa Fedha miaka mingi sasa, akirudia bajeti zake huko nyuma atakuta matumizi hayakuwa makubwa kama sasa. Sasa hivi matumizi yamepanda mara dufu. Naiomba sana Serikali kwa miaka ya mbele tuliangalie suala hili kwa makini na wataalam wana kazi kubwa sana katika eneo hili ya kuhakikisha kwamba matumizi makubwa yawe ni matumizi ya maendeleo sio matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea na *TRA*, kwa kweli *TRA* imefanya kazi kubwa sana na tunawaomba waendeleo na kazi hiyo na tunahitaji mabadiliko makubwa ya uchumi, lakini bado mchango mkubwa wa *TRA* unahitajika katika sekta hiyo. Nimpongeze sana Kamishna Jenerali Bwana Kitilya na timu yake yote na Makamishna wake wote. *TRA* wanafanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, yapo maeneo ambayo nawaomba wenzangu hawa wa *TRA* wayaangalie, kwani yanaweza kuongeza mapato. Eneo la kwanza ambalo linaweza kuongeza mapato ni eneo hili la mafuta. Upande wa mafuta wamejitahidi sana, wamefunga *flow metre* pale Bandari ya Dar es Salaam, lakini kuna vifaa wanasema vimepungua, *flow metre* ile haija-*take off* sawasawa. Lakini wapo wengine wanatumia sana Bandari ya Tanga, Kanda ya Ziwa na Bandari ya Mtwara.

Namwomba Mheshimiwa Mramba aweke kwenye bajeti yake au ikiwezekana watafute fungu maalum kuhakikisha *flow metre* zinafungwa katika Bandari zilizosalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti hii inaonekana kuna suala limefanyiwa kazi sana, nalo ni suala la mafuta ya ndege, *JET AI*. Hapa mimi kwa upande wangu naona ni mtihani mkubwa kwa Bwana Kitilya, Lauwo na wengine. Haya mafuta ya ndege ndiyo yale yale yanayogeuzwa kutumika kuwa mafuta ya taa.

**WABUNGE FULANI:** Enhee!!

**MHE. SULEIMAN A. SADIQ:** Ndio. Sasa unapoondoa kabisa ushuru wa bidhaa katika eneo hili, lazima uwe mwangalifu na uangalifu wako uwe makini kweli kweli, tujue mahitaji yetu ya mafuta ya ndege kwa mwaka ni kiasi gani, lakini pia tujue mahitaji ya mafuta ya taa kwa mwaka ni kiasi gani. Hapa wachache wanaweza kutumia mwanya huu ambao Serikali ina nia njema kabisa katika eneo hili la kuondoa ushuru wa bidhaa, lakini matokeo yake likatokea tatizo kubwa ambalo litakosesha *TRA* mapato.

Namwomba Kamishna Jenerali na wataalam wote wa *TRA* waliopo hapa baada ya baraka zote katika eneo hili, sasa wakajiweke sawa kwa sababu wapo wachache wanaweza kutumia mafuta haya kwa sababu hayana ushuru wakayaleta kwa wingi na yakauzwa kama mafuta ya taa. Yakiuzwa hivyo, Serikali itakosa mapato sana sio kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie upande wa *TRA* ambapo ningependa tena wenzetu hawa walitupie macho eneo la *VAT*. *VAT* wamejitahidi sana na Kamishna aliyepo sasa hivi amejitahidi sana, lakini bado wanahitajika wawe na mkakati mpya utakaoboresha mapato katika eneo hili. Mkakati huu unatakiwa uanzie Bandarini, mizigo inapoingia, mizigo inapotoka kuelekea godown, mizigo inapokwenda dukani, inaposafirishwa hadi inapomfikia mlaji, kuwe na utaratibu wa kufuatilia. Sasa hivi unapofika dukani, unapouliza *TV* bei gani, unaambiwa laki nne pamoja na *VAT*, bila *VAT* unaambiwa laki tatu na nusu. Sasa ujue hapa kwenye *VAT* kuna tatizo. Kama lipo lazima *TRA* sasa tuelekeze macho yetu katika *VAT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *VAT* katika nchi nyingi za Ulaya imefanikiwa sana na imefanikiwa kwa kiasi kikubwa, lakini kwa Tanzania bado. Mimi naishauri sana *TRA* tubadilike na ikiwezekana tusione aibu, tutafute watu wanaojua mahesabu. Sio siri, katika dunia ya leo Taifa ambalo linapiga hatua kubwa kwenye mahesabu ni Taifa la India. Wahasibu wengi katika Mashirika mbalimbali ni Wahindi. Wahindi wamepiga hatua kubwa kwenye mahesabu. Inapobidi kutaka msaada wa India, basi tutake msaada katika eneo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nieleweke kwamba Taifa la India limepiga hatua kubwa sana katika mahesabu. Hata wenzetu Wazungu katika Mashirika yao utakuta kuna Mhasibu mmoja au wawili ni Wahindi na Wahindi wanajua kweli kweli mahesabu. Sisemi Wahindi hawa, lakini nasema Wahindi. Mheshimiwa Lowassa anafurahi kwa sababu anaelewa vizuri mambo haya. (*Kicheko*)



Mheshimiwa Mwenyekiti, inapofika mahali tunataka msaada, basi tutake msaada kwa nia njema kwa faida ya nchi yetu au Taifa letu. Hapa upande wa *VAT* bado tunapoteza mapato mengi. *TRA* wamefanya kazi kubwa, wamefanya kazi nzuri sana na bado tunahitaji wafanye kazi nzuri katika Serikali ya Awamu ya Nne ili iwe ni Serikali inayokuja na kasi mpya kweli kweli. Tunazungumza haya kwa sababu tunaitakia mema nchi yetu. Kwa hiyo, ni vyema tukaboresha yote haya. Waswahili wanasema kujifunza hakuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa Mheshimiwa Mramba alione, leo asubuhi kuna swali liliulizwa la sukari. Majibu ya Serikali yalikuwa ni mazuri, ya ukweli, kila aliyesimama alijitahidi kueleza hali halisi. Viwanda vya Sukari vimeanza uzalishaji kikiwemo Kiwanda cha Mtibwa, Kilombero na vingine. Lakini kabla havijaanza uzalishaji kulikuwa na tatizo la sukari kati ya mwezi wa Tatu na wa Tano. Vikatolewa vibali kupitia Bodi ya Sukari. Sasa hivi vibali vile vingi muda wake umeisha tarehe 31 Mei, ndiyo tarehe ya mwisho kuingiza sukari nchini. Lakini wapo watu wana vibali, sukari hawajaleta, wengine wanaandaa kuleta sukari.

Sasa hivi ikija sukari ya nje na viwanda vya ndani vimeanza uzalishaji, tutaleta mgongano na wakulima wetu watahinda kulipwa kwa wakati. Kwa hiyo, nashauri Serikali isitishie mara moja vile vibali ambavyo vimechelewa kufanyiwa kazi na wahusika ambao ni wafanyabiashara ili tusije kuleta mgongano wa sukari nyingi ya nje wakati sukari ya ndani inazalishwa kipindi hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye Wilaya ya Mvomero. Wilaya ya Mvomero ni Wilaya mpya, lakini namwomba sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tuliomba ianzishwe Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, hatujapewa mpaka leo. Mwanasheria amesema suala hili litafanyiwa kazi kisheria. Tunaomba Halmashauri yetu ya Mvomero ianze mwaka mpya wa Serikali tarehe 1 Julai. Tumepata Wilaya, tumejiandaa, tupo tayari kufanya kazi kubwa na nzito tuliyokabidhiwa na wananchi. Naomba Serikali sasa itoe baraka tupewe hiyo Halmashauri. Mvomero kama Mvomero ni Jimbo la Uchaguzi, hatujabadilisha mipaka ya Kata wala Tarafa, ni Wilaya yenye watu zaidi ya laki mbili na elfu sitini na tano. Ni Wilaya mpya yenye mikakati mikubwa ya kiuchumi, tunaomba Serikali iangalie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Korogwe kupitia Turiani kuja Mziha-Magole ni barabara ambayo imetolewa kauli na Serikali na ipo katika mpango wa kuwekwa lami na mwaka huu wanasema tayari mipango ya awali inaanza. Tunaomba hiyo mipango ianze na ikiwezekana mkandarasi atangazwe ili kazi za ujenzi ziweze kuonekana katika macho ya wananchi. Barabara hii itafungua milango ya uchumi ya Bandari ya Tanga na Mikoa ya Kati na Kanda ya Ziwa. Barabara hii itaunganisha barabara ya Korogwe-Dumila kuelekea Dodoma na Mikoa ya Kanda ya Ziwa. Ni barabara ambayo ilikuwa inapitika miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la ahadi ya Serikali kuweka lami barabara inayokwenda Chuo Kikuu cha Mzumbe, Morogoro. Ahadi hii tuliambiwa ingeanza

mwaka jana, lakini hadi leo haijaanza. Barabara ile ina urefu wa Kilomita mbili na nusu, inaanzia Sangasanga kwenda Chuo Kikuu Mzumbe. Naomba Serikali itoe tamko ujenzi wa barabara ile unaanza lini. Vyuho Vikuu vyote nchini mwetu vimewekwa lami, bado Chuo Kikuu cha Mzumbe. Chuo Kikuu cha Mzumbe kipo katika Wilaya mpya ya Mvomero na sasa hivi tumeshawatangazia kwamba Serikali ya Awamu ya Tatu inashughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa aliyoifanya hususan katika suala la barabara na pia kuna kauli ya kutengeneza barabara hizo, naomba wenzetu waiunge mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na suala la umeme. Zipo ahadi za Serikali kupeleka umeme Mgeta na Sumve kule Mwanza. Naomba ahadi hizo zitekelezwe na Serikali. Kazi zimeshaanza, naomba zimalizwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nimalizie kwa kusema naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ABDULLA S. LUTAVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu kwa hoja hizi mbili zilizowasilishwa hapa na Ndugu zetu hawa Mawaziri wa Fedha na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na Ndugu zangu walionitangulia kuzungumza ndani ya Bunge lako Tukufu, kutoa pole kwa kifo cha Ndugu yetu, Mbunge mwenzetu Ndugu Abu Kiwanga, kilichotokea hivi majuzi na nimtakie Marehemu huyu makazi mema Peponi na nimwombe Mwenyezi Mungu awape subira na uvumilivu wafiwa hawa kwenye Jimbo la Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba niungane tena na wenzangu kukipongeza Chama cha Mapinduzi kwa uamuzi wa busara kabisa wa kidemokrasia uliokamilika juzi tarehe 4/5 kule Chimwaga kwa kumteua Mheshimiwa Jakaya Kikwete kuwa ndiye Mgombea wa Urais kwa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Amani Abeid Amani Karume kuwa Mgombea wa Urais kwa kupitia Chama cha Mapinduzi kwa Zanzibar na Mheshimiwa Dr. Mohammed Shein kuwa Mgombea mwenza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naungana tena na wenzangu kuipongeza Serikali na kuzipongeza Wizara hizi mbili hasa Ndugu zetu Mawaziri hawa, Mheshimiwa Dr. Kigoda - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba - Waziri wa Fedha. Niwapongeze na Manaibu wao, Watendaji Wakuu wa Wizara hii na Maofisa wote ambao wameshiriki katika kuandaa mipango hii ambayo imewasilishwa hapa mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ingekuwa ni kutazama ubora tu wa jambo, tusingelazimika kusimama hapa tukasema. Kwa kifupi bajeti na mpango huu, ni vizuri kama tunasimama kusema ni kwa sababu tu pengine kuna mawili matatu tunatakiwa

tusaidie katika kuboresha. Waliosimama hapa ambao wamekaa muda mrefu ndani ya Bunge hili, wameturejesha nyuma wanasema huko walikotoka bajeti za Serikali zilikuwa haziwi namna hii na mimi wala sina sababu ya kurudi nyuma miaka mingi maana nimeingia hapa mwaka wa 2000. Kila mwaka nilivyoangalia bajeti hizi zilivyokuwa zinawasilishwa kila mwaka bajeti inakuwa bora na hii ya leo ni bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *plan* ya mwaka huu ni nzuri inaleta matumaini makubwa. Bajeti hii tunasema ni safi kwa maana inawalenga maskini. Inapofikia mahali unazungumza habari hata ya kuwafikiria wale wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki jambo ambalo lilikuwa karibu iwe fedheha katika nchi hii, kwa kweli ni hatua nzuri. Bajeti hii imeandaa angalau mpango wa kuanza kuinusuru nchi na fedheha hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi ambayo ni kero kwa wananchi yametazamwa na yamefanyiwa kazi. Hata hii iliyokuwa inazungumzwa sasa hivi na Ndugu yangu hapa, habari ya kutoa *VAT* kwenye *aviation fuel*, tumetoa *VAT* kwenye *spare za train*. Yote haya yanalenga kurahisisha maisha kwa mwananchi wa kawaida. Kiujumla tunasema uchumi wa nchi hii katika muda huu ambao Serikali hii imekuwa madarakani umekuwa ukipanda mwaka hadi mwaka. Leo tunazungumza pato la Taifa linapanda kwa asilimia sita mpaka saba, hii tumeanzia kwenye nne, tano, sita na hatushuki chini tunakwenda mbele. Hili ni jambo la kushangiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa makusanyo yanafika karibu Shilingi bilioni 146 kwa mwezi kutoka kwenye Shilingi bilioni 25 kwa mwezi mwaka 1995. Hii ni hatua kubwa na tunasema mapato ya ndani sasa yamefikia asilimia 13.8. Tumeongeza uwezo wetu sasa wa kutazama kama tunaweza kukidhi ununuzi wa mahitaji kutoka nchi za nje kufikia miezi minane. Hapo ni pazuri.

Lakini tunasimama hapa kusema kwa sababu ukweli unabaki kwamba ukuaji kwa kasi hii watu wengi wanasema hautoshi na ukuaji huu unasemwa kwamba hautoshi kwa sababu tunatazama jinsi unavyodhihirika, kwa maana ya kuona mwananchi mdogo ananufaika vipi na hali hii kama tunavyoieleza hapa kwenye vitabu. Kwa sababu bado wanyonge na maskini wa nchi hii wale wanaotajwa kwamba wanaishi chini ya dola moja kwa siku bado ni wengi na mkakati wote tuliouweka wa MKUKUTA na vitu vingine.

Ni kwa kutambua kwamba tuna tatizo hili, ndio maana mikakati hii yote inaletwa. Lakini tunasema kwamba lazima tujitahidi, kasi hii izidi kuongezeka ili ifike wakati ambapo tunapozungumza ukuaji wa uchumi, basi iwe tunazungumza sote pamoja na wale ambao wanatusubiri, waone matokeo ya ukuaji wa uchumi kwa maana ya kuwagusa wao na hawa tunaowazungumzia ni wale maskini kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunahitaji kasi gani, maana yake kila mwaka kasi inakua. Hapa kwenye mpango huu uliowasilishwa na Mheshimiwa Kigoda tumeambiwa kwamba tunahitaji angalau asilimia nane, lakini Waziri wa Fedha ameeleza kwamba inapofika mwaka wa 2008, basi ukuaji utakuwa umefikia asilimia 7.9. Sasa hapa hatupo mbali, ni juu yetu kuangalia kwa mwendo huu tukifika mwaka huo 2008, huu ukuaji

utakuwa tayari unatafsirika vizuri kwamba wananchi hawa wadogo kweli? Wanayaona manufaa ya wazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ninaloliona na mimi nataka nichangie kidogo hapa. Nimeangalia bajeti hii, chanzo chetu kikuu ni kodi za aina mbalimbali karibu asilimia tisini na mbili, hakuna kitu kingine. Kuna kitu kimeandikwa mapato mapya pale, lakini sijui ni kitu gani. Lakini nasema chanzo chetu kikuu ni kodi. Ukitazama ukurasa wa 31 wa bajeti hii, hii mikakati ya kuboresha na kupanua mapato yetu imeorodheshwa pale na yote inazunguka kwenye kodi tu. Mipango iliyopo ni pamoja na kuhamisha Makampuni ya Madini kutoka kwenye Idara waliyoitengea waiingize kwenye Idara ya Walipakodi Wakubwa. Bado tupo kwenye kodi tu.

Sasa mimi nauliza, haya madini tunatakiwa tuwe tunachukua kodi tu. Naomba kuinasihi Serikali, nimesema hili mwaka juzi na mwaka jana, naomba kuinasihi Serikali, ongezeko au ukuaji wa Sekta ya Madini katika nchi hii kwa kweli ni kubwa kuliko sekta nyingine yoyote, tupo kwenye 19% sasa hivi. Lakini habari ya kuambiwa kwamba mchango wa madini haya kwenye pato la Taifa ni asilimia mbili, tatu tu, kwa kweli mimi kidogo inanipa karaha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuinasihi Serikali kwamba isiwe kodi tu ndiyo tunayotegemea kwenye madini. Nainasihi Serikali tuwe na miliki kwenye madini haya. Ukiangalia hapa tunapozungumza, mapato ya ndani ya nchi hii ni mengi ukiyatazama. Tutazame vile vile kwamba nchi hii ina fedha zinazoingiza kutokana na kitu tunachoita *exports*. Tunasema, *exports* mwaka uliopita imeongezeka kwa asilimia 18.2, lakini hizi tunazoita *traditional exports* Wallah zimeongezeka kwa asilimia nane tu, yaani yale mengine yote yanatokana na hizi *non-traditional exports* na tunasema kwamba hizi *non-traditional exports* mchango mkubwa umetokana na dhahabu. Lakini hapa tunazungumza thamani ya *exports* ambazo zimetoka ndani ya nchi hii, sidhani kama vile hapa tunazungumzia mapato kwa nchi kwa maana ya kinachopatikana kutoka kwenye madini yale kwa hazina ya nchi hii kwa sababu kama tunazungumzia kodi tu ndio maana tunaishia kwenye asilimia tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama tungekuwa hivi, nataka kuuliza, tulipokuwa tunazungumza kwamba tulikuwa tunamiliki angalau asilimia hamsini ya almasi, si ilikuwa tunakuwa na almasi ya kwetu? Lakini asilimia hamsini inayosalia wanayokuwanayo wale Wawekezaji si tulikuwa tunawatoza kodi vile vile? Sasa inakuwaje tunapokuja kwenye suala hili la dhahabu na madini mengine haya ambayo Mikataba yake tumeingia hivi karibuni, kwa nini tutegemee kwamba itakuwa kodi tu na isiwe kwamba tunayomiliki kwenye madini yenyewe? Kwa sababu kama tungekuwa na miliki kwenye madini yenyewe nina hakika kabisa pato la Taifa lingeongezeka kwa kasi kubwa. Kama tungekuwa tuseme tunamiliki asilimia hamsini ya dhahabu yote inayotoka na leo tunazungumza karibu makontena matatu au manne ya dhahabu, dhahabu *pure* kabisa! Hizi ni fedha nyingi sana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba hapa tunapozungumza habari ya madini kungezeko, tunazungumza kwamba madini yameongezeka kwa sababu bei

zimepanda. Sasa na sisi tungekuwa tunamiliki, basi tungenufaika na upandaji wa bei, lakini kwenye habari ya *non-traditional* huku kilichopatikana kama ongezeko ni kidogo sana na hilo ongezeko halikutokana na kuongezeka na hizi *non-traditional exports*, kilichoongezeka hapa ni kwamba tumeongeza uzalishaji. Pamoja na unyonge wetu, imebidi tuongeze uzalishaji kupata angalau kidogo hizi bilioni 292. Hiki kitu kwa kweli inabidi tukifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema ni kwamba, kama tunataka kufanya maendeleo ya haraka, kama tunataka ukuaji wa uchumi uwe wa haraka haraka angalau kidogo kama tunavyotamani, kama leo tunalazimika kuongeza *production ya non-traditional exports*, hapa tunazungumzia korosho pamba na vitu vingine, basi kwa nini hatutazami kama tunaweza pia ku-*add value* kwa kuhakikisha kwamba angalau haya mazao kama korosho na vitu vingine, *agro-processing* tuipe uzito. Lakini kama hivi tunavyozungumza humu, nimeisoma lakini sioni kama kuna uzito tumeweka kwenye mambo ya *agro-processing*.

Hata hivi viwanda nakumbuka sana wakati Viwanda vya Korosho vile kumi wakati vinafanya kazi, kule kwetu kuna viwanda karibu vitano hali ilikuwa nzuri sana na sasa watu tumekuja kudhalilika sana kwa sababu viwanda vile havifanyi kazi.

Sasa nilikuwa nasema, tutazame maeneo ambayo kama unataka kukuza uchumi, basi ukuze uchumi, uchumi unakua kulingana na msingi wenyewe kama msingi ni mdogo hata ukikua kwa asilimia kumi bado *impact* yake ni ndogo. Kama uchumi kama ile *base* ni pana zaidi, basi *impact* ya ukuaji wa uchumi hata ingekuwa asilimia nne, maana yake uchumi wa Marekani ukikua kwa asilimia tatu, hicho kitu ni hatari. Sisi hata tukikua kwa asilimia ishirini, hatuwezi kuwafikia wale. Mimi nasema lazima Serikali iliangelie jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nataka kumalizia kwa kusema, viwanda hivi vilivyobinafsishwa, sisi tuweke mkakati wa kuhakikisha kwamba tunafuatilia, sio mtu anabinafsishiwa kiwanda cha *light source* halafu yeye anakwenda ku-*import* tena *bulb* badala ya kutengeneza hapa. Mtu anapewa kiwanda, lakini anafanya kitu kingine.

Mimi nafikiri tunapobinafsisha hatuondokani na maslahi na Serikali, haijitoi kwenye kuona kwamba lile jambo lililokuwa linaendelezwa pale liendelezwe, kama ni kutengeneza viatu, basi achukue atengeneze viatu. Sisi tusiwaachie wale wafanye wanavyotaka wao kwa sababu wanafanya uchumi wetu usiwe *stable*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumalizia kwa kusema tumefuta *VAT* kwa vitu kama *spare* za *TRC* na *TAZARA*. Tatizo tulilionalo hapa ni kwamba, sijui kama kuna mpango wa kuhakikisha kwamba tunapofuta *VAT*, kile kiwango cha punguzo kinachopatikana kinaweza kuwa *reflected* kwenye manufaa yanayowafikia watumiaji wa huduma zile. Jambo hili tunaweza kulipata, kama hatuna mpango mahsus, tunaweza kulipata kwenye *TRC* na *TAZARA* katika upangaji wa bei zake. Tunaweza kulipata sasa kama tunavyosema tunatoa punguzo la kodi hizi kwenye vitu kama pembejeo na vitu vingine.

Kinachojitokeza ni kwamba wale watu wanaotakiwa kufanya kazi ya kuingiza pembejeo hapa nchini wananufaika zaidi kwa kutengeneza faida zaidi kwa punguzo hili badala ya kuhakikisha kwamba punguzo hili linamfikia mlengwa ambaye ndiye mlaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatuweki mkakati kwenye jambo hili, pamoja na kwamba tumejitoa katika kufanya udhibiti, lakini hakuna shughuli ya biashara inayokwenda bila angalau udhibiti kidogo, ndiyo maana tumeanzisha hii *EWURA* na vitu vingine. Hata kwenye maeneo haya, kama tunajua kwamba haya ndiyo maeneo yanayomgusa kabisa mwananchi mdogo ambaye ndiye tunayepigana na umaskini wake leo, lazima tuweke utaratibu ambao utatuhakikishia kwamba angalau tunadhiti na kujua tunapompunguzia mfanyabiashara huyo, basi hii iwe *reflected* kwenye *price* ili yule ambaye anatakiwa kutumia huduma hii naye anufaike na hatua hii njema ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka nimalizie kwa kusema nimeona hapa tumepandisha bei moja kwa moja ya sigara na pombe. Mimi siyo mnywaji wala sivuti sigara, lakini nafadhaika kidogo, nimeona utaratibu huu au *approach* hii ya *direct taxation*, nilikuwa naona kama imepitwa na wakati. Hapa katikati tulikuwa tunaweza kufanya mambo yetu safi, huku wanywaji wa pombe wanaona bei imepanda, tu na wavuta sigara wanaona zimepanda tu siyo kwa kuzishambulia moja kwa moja kama hivi ilivyofanyika leo naona kama tumerudi nyuma kidogo. Hilo tu nilikuwa nataka niliseme mimi sikupendezwa nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa niyaseme haya na ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu Waheshimiwa Wabunge kutoa pole kwa wenzetu wa Jimbo la Kilombero kwa kufiwa na Mwakilishi wao na Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema Peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana wewe ukiwa Mwenyekiti na unifikishie salamu hizi kwa Mheshimiwa Spika na Waziri Mkuu na Waheshimiwa Wabunge wote walioko hapa ndani katika kunifariji nilipofiwa na mama yangu mzazi katika Bunge la mwezi Aprili. Nasema ahsanteni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza Wagombea wetu wa Chama cha Mapinduzi ambao ni Bendera inayong'aa. Tuna tegemeo kubwa sana atashinda kwa kishindo Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Wagombea wenzake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Mawaziri wetu wawili, Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji na Waziri wa Fedha, wametupa heshima kubwa. Tangu nimeingia hapa Bungeni miaka mitano hii ambayo tunaelekea ukingoni, wameweza kuwa Washauri wazuri wa Mheshimiwa Rais wetu na

hatimaye Tanzania tumekuwa na heshima kubwa katika kulipa madeni na ukusanyaji wa mapato yetu ya ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninapata wasiwasi sana watu wakibeba mafanikio ambayo tumeyapata kupitia kwenye Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi. Je, watakuja na miujiza gani? Hawaoni miundombinu kwa mfano, barabara, afya, maji, elimu jinsi ambavyo vimeboreshwa? Wao wamefumba macho, hawayaoni haya na wanapata kigugumizi kuipongeza Serikali yetu. Naomba hebu watueleze, basi watakuja na mikakati gani ya kuhakikisha kwamba utawala huu ulioshikwa na Mheshimiwa Rais mpendwa ambaye sasa hivi anamaliza muda wake basi, watapiku kwa namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumze kuhusu MKUKUTA na imekuja kwa wakati kwa sababu tulikuwa tunaboresha miundombinu na inaonekana. Sasa ni wakati wake tunaufufua uchumi na kupunguza umaskini baada ya kuboresha maeneo hayo barabara, afya, maji na Elimu. Lakini nitaomba tu wanisaidie, kila nikisoma bajeti zote mbili za Waheshimiwa Mawaziri sioni wapi tukiangalia kwamba tunapotaka kukuza uchumi tunaboreshaje viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwanja wa Ndege wa Mwanza ni eneo ambalo Jiji la Mwanza kuna madini, kuna samaki, lakini sioni wapi panasema kwamba ule Uwanja wa Ndege utapanuliwa namna gani ili kuhakikisha kwamba basi na wao wanachangia katika kukuza uchumi huu. Nitaomba Waheshimiwa Mawaziri wote wawili wanieleze tu wana mikakati gani kuhusu huo uwanja wa ndege, kwani unatia aibu kama tunavyojua kwamba vitu vingi vinatoka katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nimejaribu kuangalia mambo ambayo yamezingatiwa katika bajeti hii, sijaona mifuko hii ya akinamama na vijana limezungumzwa wapi. Lakini sijui kama imezingatiwa kwamba hata kile kiwango ambacho kilikuwa kinapitishiwa kwenye Wizara zile mbili wameongeza kiasi gani ili kuhakikisha akinamama wanapewa mikopo. Kama mnavyojua, akinamama wanajali wajibu wao na wanarudisha mikopo hiyo bila wasiwasi. Nitawaomba Waheshimiwa Mawaziri wote watusaidie. Kama hakuna mbinu nyingine, lakini kuna fungu limetengwa la rushwa. Kwa nini hilo fungu la rushwa lisipelekwe kwenye mikopo ya akinamama? Basi naomba na hilo liangaliwe vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapozungumzia MKUKUTA, unaangalia utaukuzaje uchumi na kupunguza umaskini. Ukiangalia, tumeamua kufungua mifuko ya umeme hadi Vijijini na akinamama wengi watakuwa na miradi yao midogo midogo ya kutumia huo umeme kwa kutengeneza *ice cream* au kuweka vitu vyao vya kuuza kwenye friji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kila tunapoelekea mbele, gharama ya umeme inazidi kupanda. Watamudu kweli hao hawa akinamama! Naomba hili waliangalie wenzetu na tuliwekee mkakati mzuri zaidi ili kweli kama tunasema tunamgusa raia wa hali ya chini ili aondokane na umaskini, basi ionekana kwamba umeme nao unaangaliwa upya na gharama zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kuzungumzia suala la jinsia. Katika hotuba ya Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu mpendwa ambaye anamaliza muda wake kwa kutekeleza ahadi yake aliyosema kwamba nitaondoka katika utawala huu nikihakikisha asilimia ya wanawake imepanda na kweli Bunge lako Tukufu hili limepitisha asilimia 30 ya kuhakikisha kwamba Wabunge Wanawake wanaongezeka ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalizungumza hili ili tusionekane kwamba wanawake tunadai sana, lakini wakati akisoma hotuba yake Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji ameonyesha kabisa jinsi Watendaji wanawake idadi yao ilivyo ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda wanakuwa na wasiwasi, lakini nina mfano halisi. Mwanamke unapompa madaraka anaonyesha uwezo wake kweli kabisa. Hili naomba nilisisitize na nina mfano halisi. Nimeingia ndani ya Bunge hili miaka mitano nimekuwa na mama mmoja mama Blandina Nyoni. Mama Blandina Nyoni ni mwanamke ambaye amekuwa na ushauri mzuri kwa Waziri wake na hatimaye mpaka sasa tunavyompongeza Waziri wake ni pamoja na yeye akiwa amechangia mle ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mama Blandina Nyoni, ameweza kuwa mshauri mkubwa sana kwa Waziri wa Fedha na ameweza kuleta mikakati ya kuhakikisha kwamba wizi wa fedha za Serikali unapungua kwa kuwabana wale ambao wana nia mbaya ya kuhakikisha kwamba fedha hizo zinatumiwa ovyo. Sasa ninakuja ninashangaa wakisema kwamba wanawake hatuwezi, lakini tunaweza! *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mnaweza.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza. Nikiangalia kwamba Wakuu wa Mikoa ni wanawake wawili tu katika Mikoa 26. Hivi wakikutana ndani ya Vikao vyao na ninajua wanawake tuna nafasi yetu. Jana wenyewe mmeona tulivyokuwa humu ndani vigelegele vilikuwa vinatoka kwa akinamama. Angekuwepo Mheshimiwa Ngoye ningemwuliza wao wawili wanapigaje vigelegele mle ndani.

**MBUNGE FULANI:** Hawawezi.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hawawezi kwa sababu wamemezwa na wanaume ambao ni 24 na wao ni wawili tu. Naomba hili suala, basi Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji aliangalie vizuri. Hebu watuwekee mikakati angalau basi waendeleo kutuongozeza hizo asilimia kwamba hata angalau wafikie kwenye utendaji asilimia 50 kwa 50, wafumbe macho tu ili waone na sisi kwamba huo uwezo tunao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mama Blandina Nyoni sifa nilizompa ni nzuri, lakini adui ni wengi kwake. Naomba sana Blandina Nyoni afanye kazi yake nzuri tu na



sisi tuko pamoja na yeye na tunamkabidhi kwa Mwenyezi Mungu, yeyote hawezi kumfanyia lolote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii tena kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kazi nzuri ya kuhakikisha kwamba *cash budget* imeweza kusimama imara na hii ni kutokana na uaminifu na ndugu zetu wa *TRA*. *TRA* ni Mamlaka ambayo imetupa heshima kubwa kila mwaka tukija hapa Bungeni kupewa taarifa ni kwamba tunakwenda juu, haturudi nyuma. Basi, ninaomba ndugu zangu wa *TRA* kupitia kwa Waziri wetu wa Fedha azidi kuwa nao karibu na wao, wavumilie tu kazi ni ngumu wanayoifanya, lakini tutawaombeni ili waweze kuendelea vizuri kuhakikisha kwamba Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi inaendelea kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, ningemwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha aimarishe sana Kitengo cha Ufuatiliaji wa Fedha anazopeleka huko. Mheshimiwa Waziri wa Fedha ana kazi kubwa sana kuzikusanya fedha na kuhakikisha kwamba zinafika kwa walengwa. Itakuwa maajabu Waziri wa Fedha anapopeleka kule watu wengine waweze kula hizo fedha hivi hivi. Lakini sasa nimwombe Waziri wa Fedha kama alivyofanya kufunga ule mtambo wa kuhakikisha wizi wa aina yoyote ile haufanyiki, basi tuone fedha anazotuma kule hususan amesema kwamba zinafika mpaka kwenye Mitaa anafuatilia matumizi yake ni halali ili tuone kwamba fedha zetu zinatumika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nimwombe Waziri wa Fedha aimarishe Vyuo vyetu vya Uhasibu. Ninasikitika sana kusikia aagize Wahasibu kutoka nchi za nje na wakati Waziri wa Fedha ana vyuo vyake, Arusha kuna Chuo na Dar es Salaam kuna Vyuo. Sasa nashangaa aagizaje wataalam kutoka nje na Watanzania wapo. Nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha aimarishe Vyuo na ahakikishe kwamba anatoa mafunzo kwa hao Wahasibu na wapate ajira hapa hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha asomeshe Wahasibu wengi ili basi wakidhi haja kwenye Halmashauri zetu za Wilaya kwa sababu Waziri wa Fedha anapeleka fedha nyingi kama hatuna wataalam huko tutakuwa tunatwanga maji kwenye kiu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tena kuongea kwenye suala la ubinafsishaji. Heshima kubwa tumepata na vijana wetu wamepata ajira. Lakini kinachosikitisha kuna watu ambao walichukua viwanda lakini havifanyi kazi. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji hili lifuatiliwe kwa makini. Hawa ni wabaya ambao wanaweza kurudisha uchumi wetu nyuma badala ya kuuendeleza mbele. Kwa nini wachukue maeneo? Natoa mfano wa *Moprocco* na ni eneo ambalo liko barabarani kabisa, kila mtu analiona na kiwanda kile hakifanyi kazi, basi tutafute mbinu nyingine ya kukiendeleza kama siyo *Moprocco* tena kwa sababu Dar es Salaam vimejengwa viwanda vingi, basi itafutwe njia nyingine ya kuendeleza yale majengo na yamekaa mahali pabaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine hatma ya *Embassy Hotel* ni jengo nzuri ambalo lipo katikati ya Jiji la Dar es Salaam na sasa hivi, hili jengo linachakaa. Serikali ina mpango gani basi hata kuwekeza kitu kingine kama hayawezekani mambo ya hoteli tena. Niiombe basi Serikali iangalie majengo mengineyo ambayo yako huko yanaweza kuendelezwa kwa namna nyingine, basi tuyafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi yangu ni hayo. Lakini mwisho niombe tutakiane kheri sana ndugu zangu, tunakwenda Uchaguzi ili wote turudi na Mungu atutasaidia tujikabidhi kwa Mwenyezi Mungu. Ninaunga mkono hotuba zote mbili asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipa nami nafasi hii ili niweze kuchangia hoja mbili zilizopo mbele yetu. Kama ilivyo kawaida, napenda niwape pole Ndugu zetu wa Jimbo la Kilombero kwa kumpoteza Mbunge wenzetu. Nawapa pole sana.

Pili, napenda Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge niwape shukrani kwa kuwa kipindi cha Bunge lililopita sikuhudhuria nilikuwa niko Bugando hospitali nanyi mlinitumia salaam, mlinipa pole na wengine walikuja kuniona. Nawashukuru sana kwa maombi yenu. Wananchi wangu kule napenda niwaambie kwamba sasa hivi niko sawasawa, niko kazini wasiwe na wasiwasi na wale wanaofanya mazoezi kule watulize bali nipo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze na kumpongeza ndugu yetu Jakaya Mriso Kikwete kwa kuteuliwa kushika bendera yetu ya *CCM* wakati wa mapambano yanayokuja na Ndugu zetu Mheshimiwa Aman Karume na Dr. Ali Mohamed Shein nawapongeza sana kwa nafasi hiyo. Lakini vilevile, niwape pongezi wale ambao walijitokeza kugombea nafasi hiyo. Kukamilisha demokrasia ni ujasiri mkubwa sana. Wengine tuliona maji marefu. Kwa hiyo, nawapa pongezi wenyewe kwa kujitokeza, walifanya kazi nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mada iliyo mbele yetu, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafishaji pamoja watumishi katika Wizara hizo. Kwa kweli wamefanya kazi nzuri sana, nawapongeza sana. Tangu nimeingia katika Bunge hili, kwa kweli wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana na hatua walizokuwa wanazifanya zimetufikisha mahali ambapo kila mmoja anafurahia kazi wanayoifanya. Hata Wapinzani wanavyozungumza kimoyomoyo wanakiri kwamba kwa kweli kazi imefanyika na ndiyo maana wanapata nguvu ya kuzungumza hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini napenda niangalie, sasa hivi *TRA* wanakusanya bilioni 160 kwa mwezi, wanafanya kazi nzuri sana. Nikijaribu kufikiria nadhani tunaweza tukapata zaidi kwa sababu bado kuna mianya michache wakiirekebisha tunaweza kukusanya bilioni 200 kwa mwezi. Hiyo inawezekana! Kwa sababu kama hizi fedha zinapatikana kwa jinsi wanavyokwenda, lakini unaona kwamba wanaweza wakakusanya zaidi ya hapo.

Tuchukue mfano wa pale *TRA* Ndugu *Commissioner General* amesifiwa sana hapa na kweli anafanya kazi nzuri sana na anajitahidi na ni mkali, namfahamu Ndugu Kitilya, ni mkali sana! Lakini ukienda kuna sehemu nyingine wanamchenga pale *long room*. *Long room* Ndugu Kitilya pale panamshinda. Pagumu pale!! Ukiagiza gari utamaliza wiki mbili, wiki tatu unazunguka, pale pamekuwa kero! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kama nia yetu ni kukusanya mapato, basi magari kama yanafika au mizigo inafika wafanye haraka vitu viondoke. Kwa sababu sasa hivi watu wameanza kutukimbia wanakwenda Mombasa. Mombasa ni siku mbili mzigo unaondoka, lakini pale Dar es Salaam kwa sababu ya *long room* na mizunguko ya pale utakuta gari imefika Jumatatu, Jumamosi na Jumapili wanapumzika, mtu anakuja ni wiki mbili anapigwa faini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nii mifano iko wazi, hata sasa hivi mimi kuna gari yangu ilifika Jumatatu, lakini nimepiga simu jana wananiambia labda niende mwenyewe. Sasa Mbunge, tena niache Bunge niende nikakae kule, kuna tatizo pale na watu wengi utakuta wanasota mpaka Mzungu anabadilika anakuwa *blue* hata kama ana fedha, ila ucheleweshaji ni tatizo siyo fedha anabadilika anakuwa *blue* anahangaika pale *long room*. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha aangalie, hapo pana tatizo pale. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, gari linavyochelewa Bandarini, ile Bandari yetu unakuta macho yametolewa, yameondolewa taabu tupu. Sasa pale tukirekebisha watu hawatatukimbia. Hii ni biashara na pale ni tatizo. Kama ni uongo sasa hivi uende ukaangalie pale au ubadilishe uvae ufanane na mimi wasikujue ni Waziri, pale utaona watu wanavyohangaika, lakini mtu anakuangalia usoni anakuzungusha, taabu sana pale! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ni kero, pamoja na kwamba Serikali imetoa *exemption*, lakini kuna hatua ambayo inakera unapewa *exemption* unalipa, unasubiri siku tatu, nne uandikiwe *cheque* nyingine. Kwa nini isiwe *process* ya ndani kwa ndani badala ya kuambiwa sasa *cheque* imeandikwa ndiyo uende ukalipie? Kwa sababu hii ni kupata fedha na sisi tunataka fedha ziingie. Kwa nini iwepo *process* hiyo nyingine? Sawa, labda ni ya ku-*counter check* kama kweli kalipa au namna gani, lakini kwa nini mtu asubiri kwa sababu ni fedha inatoka mfuko huu inaingia mfuko mwingine?

Mahali pengine Mheshimiwa Waziri wa Fedha tunaweza tukapata fedha nyingi kwenye madini wanavyokueleza, nadhani kuna haja ya kuwa makini sana. Hii biashara ya madini ni ngeni kwetu. Ni ngeni lakini isiendeleo kuwa ngeni miaka mitano sita, saba bado tunaiona ngeni. Sisi tunatoa leseni, ufuatiliaji hawa jamaa wanaendaje, *EIA* imefuatiliwa vipi? *EMP* imefuatiliwa vipi? Je, watu wetu sasa wanaingiaje humo kwenye biashara hiyo kwa sababu unakuta Kampuni zetu hazipewi msamaha zinapofanya kazi mle ndani, lakini Kampuni za kigeni zinapewa msamaha. Sasa MKUKUTA unafanikishaje hapo?

**MBUNGE FULANI:** Hapo sasa!

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna haja ya kuangalia sana suala la biashara ya madini. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha tukiri kwamba biashara hii TRA mwaka jana 2004 tunashukuru Serikali imeunda Tume. Tunaomba ile taarifa walioleta waliokwenda kwenye Tume, Tume ya Dr. Kipokora nilimwona kwenye viwanja hapa, hebu isomwe kwa makini na hiyo taarifa ifanyiwe kazi kwa haraka. Hawa watu wanachukua na bei inapanda, kesho itashuka. Hiyo taarifa ifanyiwe kazi haraka kusudi angalau tuambulie kitu. Makaburi yetu yatapigwa fimbo, wewe ulikuwa Mbunge, vitu vikachukuliwe! Tupo, tutachapwa fimbo sisi? Kwa sababu watauliza unaweka wapi fedha? *(Makofi/Kicheko)*

Halafu lingine ni matumizi yetu ya fedha. Tuangalie matumizi tunayopata wameeleza wenzangu. Lakini:- Je, matumizi tunavyopata fedha hii ni fedha ya kulamba tu au ni kufikiria kuweka vitega uchumi na maendeleo? Maana yake tunaweza tukapata fedha nyingi, lakini namna ya kuzitumia tunazitumiaje na tunaziweka wapi kwenye miundombinu sawa tumetengeneza barabara. Lakini:- je, hatuwezi kuweka nguvu zaidi huku? Labda nitaomba wanieleze kuna kitu gani. Nafikiri ni kitu kizuri lakini mimi sikielewi.

Ukiwa pale Ofisi ya Bunge Dar es Salaam ukiangalia kulia kama unaangalia Ikulu, kuna jengo kama hekalu linajengwa kwenda mbinguni kule, lile jengo refu najiuliza ndiyo Wizara ya Fedha au ndiyo Benki Kuu au ndiyo nini au ni kitega uchumi kwenye Benki au ni nini? Mimi sielewi lile jengo. Kwanza nilifikiri ni *University* au nini maana tuna *Universities* chache sisi. Maana yake sasa hivi tunatumia kompyuta kama ni fedha, ni kompyuta inaingia kwenye kitu kidogo, sasa je, tutapeleka mafaili kule au watumishi tutawapeleka kule au nini kinafanyika pale? Naomba maelezo ya kina, lile jengo ni la nini? Nitapenda nielewe lile jengo ni refu sana, watu kukaa mle na kwa kweli sijui tutaajiri watumishi wengine au *ma-safe* yatawekwa huko au ndiyo fedha za Benki zinawekwa huko, sielewi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikiangalia jengo lile naanza kuwaza barabara ya kutoka Dodoma kwenda Arusha, naanza kuwaza barabara ya kutoka hapa kwenda Tabora, naanza kufikiria maji kutoka Bukondo, Nyakagomba, Chigunga tangu mwaka 1976 mpaka kwenye wachimba madini kule Rwamgasa, Bukoli, Nyakagwe, hakuna, tumeshindwa! Lakini lile jengo linakwenda mbinguni. Je, kuna nini hapo? Sasa najiuliza:- Je, vipi? Nimembana Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo amenipa fedha kidogo, nafikiri zitatoha sehemu ndogo tu. Maji tangu mwaka 1976 jamani *priority* ya kuwasaidia wananchi wale wanakunywa maji machafu. Kwanza tulishaelezwa kwamba maji ya Mwanza chini ni madini, kwa hiyo hayafai. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la MKUKUTA nafikiri katika kuondoa umaskini tuangalie wachimbaji wadogo wa madini. Hawa wachimbaji wadogo ni wengi karibu milioni moja na wanazalisha, kwa nini tusiwape uwezo tuwapelekee umeme hawa wachimbaji wadogo? *(Makofi)*

Halafu wakulima tuangalie na wenyewe mwaka jana wakulima wa pamba walilipwa Shilingi 300 kwa kila kilo na leo wamepewa Shilingi 150, hivi tuwaambie nini Mheshimiwa Waziri kama MKUKUTA ndiyo *style* hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niipongeze Serikali kwa kuimarisha elimu. Inafanya vizuri. Tumepewa fedha za *MMES* lakini utaratibu wa fedha za *MMES* kupitia Hazina Ndogo ni kero. Mpaka sasa hivi fedha nyingine hazijafika mashuleni. Hebu tazama pale, ni tatizo!

**MBUNGE FULANI:** Ni kweli!

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanasafiri *kilometers and kilometers* kwenda Makao Makuu ya Mkoa kufuata Hazina Ndogo kwenda kutafuta fedha hizo badala yake fedha zinaishia kwenye nauli tu na wale watu wa Hazina Ndogo mnavyojua watu wa fedha wana macho ya namna gani, wanakutazama machoni wanazunguka mpaka uwateremshe, unajua mwenyewe uje upate fedha hizo ni shida!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kengele inanifukuzafukuza. Napenda nizungumze suala la madeni. Mheshimiwa Waziri wa Fedha amesema madeni yatalipwa. Lakini naomba nielewe kuna utaratibu gani ili tatizo hili la madeni ya watumishi hasa Walimu, kila siku kuunda Tume, kupeleka Wabunge, inaiondolea heshima Serikali! Hebu maliza hili tatizo Mheshimiwa Waziri. Watumishi wanadai fedha kwa muda wa miaka mitatu, minne, Walimu wa Sekondari ni shida, wanaandikiwa barua sasa hivi tunawashughulikia, unawapa matumaini. Ni sawasawa na mtu kumpelekea kijiko na uma halafu ukamnyima chakula, wanashindwa kusomesha watoto wao kwa sababu ya madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba hao wastaafu ambao Serikali iliahidi kuwapa fedha zao, tafadhali wasiendeleo kupata usumbufu. Wastaafu wamebakiza miaka michache, mnapowasumbua kwa kuwacheleweshea kuwalipa fedha zao ni kuwataka wafe tu. *We are buying time* ili wafe hao watu! Kwa nini tunavuta muda? Sasa hivi wako zaidi ya 50,000 lakini hapa waliosomwa ni karibu 7,000. Je, wengine hao namna gani? Kuna utaratibu gani? Tunaomba maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. JOHN L. MWAKIPESILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie katika hotuba hizi mbili ambazo zipo mbele yetu: Hotuba ya Waziri wa Fedha na hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kubwa sana kwa Mawaziri hao wawili kwa hotuba zao nzuri sana. Vilevile, napongeza Mashirika yote ambayo yako chini ya Wizara zao pamoja na Naibu Mawaziri na Makatibu Wakuu na wafanyakazi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba zote mbili zinaonyesha dhahiri mafanikio yaliyopatikana kati ya mwaka 1995 na mwaka huu 2005. Hotuba ya Waziri wa Mipango na Ubinafshaji pamoja na hotuba ya Waziri wa Fedha zinaonyesha dhahiri kwamba uchumi umekua kufikia asilimia 6.7 ambalo ni jambo nzuri kabisa kwa sababu mwaka 1995 uchumi ulikuwa unakua kwa asilimia tatu tu. Mfumko wa bei umepungua, mauzo ya nje ya bidhaa na huduma yanaongezeka na mapato ya ndani yameongezeka sana. Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri sana ambayo imeifanya kwa kukuza uchumi wa nchi yetu na kuuweka kuwa tulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kuipongeza Serikali kwa kuweza kulipa deni la ndani kwa Shilingi bilioni 144.3. Ukisoma ukurasa wa 13 Ibara ya 17 Waziri wa Fedha anatueleza kwamba madeni ya ndani yaliyohakikiwa yamelipwa Shilingi bilioni 12.3 kama fidia kwa wale waliokuwa wanadai Serikali, Shilingi bilioni 111 madeni ya wazabuni wafanyabiashara ambao wamefanya biashara na Serikali lakini Serikali ilikuwa haijawalipa.

Vile vile, Serikali imelipa limbikizo la mishahara Shilingi bilioni 21. Kwa kweli naipongeza sana Serikali. Naipongeza Serikali kwa sababu kutokuwalipa wananchi wako ambao wamekufanyia kazi kama Serikali, kutokuwalipa wazabuni ambao umefanya nao biashara ni sawa kabisa na kuwafilisi wafanyabiashara wako. Kama unawafilisi wafanyabiashara wako matokeo yake ni kwamba unadhoofisha uchumi wa nchi kwa sababu hawa wafanyabiashara wakifilisika ajira zinapungua na Serikali haipati kodi. Kwa hiyo, naishukuru sana Serikali. (*Makofi*)

Lakini bado naishauri Serikali kwamba hili suala la malimbikizo ya mishahara ni vizuri Serikali ifanye kila juhudi kulimaliza kwa sababu bado kuna matatizo makubwa hasa kwa Walimu, Askari Polisi na Wafanyakazi wa Idara nyingine ambao wanadai Serikali fedha nyingi. Ninaiomba sana Serikali hasa Wizara ya Fedha ihakikishe kwamba katika mwaka ujao, basi haya madeni ya ndani yalipwe ili malalamiko ya wananchi yapungue. Kulipa madeni ya ndani ni kujiletea heshima kwa Serikali, kwa sababu Serikali ambayo inadaiwa, maana yake inapunguza imani ya wananchi wake kwa Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wameshughulikiwa vizuri kwa kiasi, lakini kuna wafanyakazi wa Idara nyingine ambao *they are not organised*, hawajaji-organise vizuri na kuwa na vyombo vyao vya wafanyakazi vya kuwatetea, hasa Polisi, bado wanadai Serikali fedha nyingi na ningeiomba Serikali iwatazame hawa Askari. Pale Wilayani kwangu Kyela kuna Askari watatu ambao wamestaafu, lakini kwa maajabu kweli kweli baada ya kustaafu hawajalipwa pensheni zao, wameambiwa tu ondokeni kwenye nyumba za Polisi halafu msubiri pensheni kutoka Serikalini, mpaka leo hawajalipwa. Kama wamelipwa, basi wamelipwa juzi lakini wakati naondoka Kyela katikati ya mwezi uliopita walikuwa bado wanadai. Tatizo hilo sio Kyela tu, inaonyesha

kwamba ni tatizo la nchi nzima. Lakini Naipongeza Serikali kwamba imeliona hilo na imeanza kulipa madeni ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali vile vile kwa kukuza akiba ya fedha za kigeni. Tumeambiwa kwamba akiba ya fedha za kigeni ambazo tunazo hivi sasa inatosheleza kulipia manunuzi toka nchi za nje kwa miezi minane na siku kumi (8.3 months). Naipongeza sana Serikali. Lakini nikitafuta katika hotuba ya Waziri wa Fedha nilikuwa nataka kujua hii akiba ni kiasi gani, nimeshindwa kuipata. Ningependa kujua hiyo akiba ya fedha za kigeni kwa mwaka huu ni Shilingi ngapi? Mwaka jana tuliambiwa akiba ya fedha ya kigeni ilifikia Dola bilioni 1.6 ambayo ni nzuri sana na inawezekana sasa imeongezeka. Tungependa kujua mchanganuo wa hiyo akiba ya fedha za kigeni. Ninavyofahamu ni kwamba sehemu kubwa ya akiba hiyo ni misaada kutoka Serikali za nje, wafadhili. Akiba hiyo halitokani na jasho la uchumi wetu, ni akiba ambayo inachangiwa na wafadhili kutoka nje.

Hilo ni jambo zuri kuwa na akiba nzuri ya fedha za kigeni. Lakini kama akiba hiyo inatokana na ombaomba au inatokana na wafadhili, ni jambo la hatari kweli kweli. Endapo utagombana na wafadhili hao, basi uchumi wako utaporomoka utarudi nyuma. Tuna kazi moja kubwa ya kufanya na kazi hiyo ni kuongeza mauzo ya nje. Kuongeza tija ya uzalishaji katika viwanda vyetu na kuongeza uwekezaji katika miradi mipya. Lakini zaidi ni lazima tufanye mageuzi katika kilimo. Tukifanya mageuzi katika kilimo na kuwekeza fedha nyingi katika *agro-processing industries* tunaweza kabisa kuboresha uchumi wetu kwa kuuza bidhaa nchi za nje na kuongeza mauzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri wa Fedha ukurasa 39 ibara ya 44 Waziri ametoa kodi ya *VAT* katika vipuri vya treni, *TRC* na *TAZARA*. Naipongeza sana Serikali kwa sababu reli ndiyo muundombinu muhimu katika uchumi wa nchi yoyote ile. Lakini ningependa sana Serikali vile vile ifikirie kuondoa kodi ya *VAT* katika vipuri vya meli. Tunayo Makampuni mengi ya meli ambayo yanafanya kazi vizuri sana. Tunayo Kampuni ya *Marine Services Company* ambayo ni Kampuni tanzu ya *TRC*.

Hii Kampuni inafanya kazi katika maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Inasafirisha abiria na mizigo mingi katika maeneo hayo. Kampuni hiyo imeelemewa hivi sasa kwa sababu ya gharama kubwa ya vipuri. Kwa hiyo, kama Serikali inaondoa kodi ya *VAT* katika vipuri vya treni, hakuna mantiki yoyote kwa nini isiondoe kodi ya *VAT* katika vipuri vya meli. Ninaiomba sana Serikali ilione hilo na iondoe kodi hiyo ili haya Makampuni yaweze kuendeshwa vizuri na kwa faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, mimi sitazungumza mambo mengi. Naipongeza sana Serikali hasa Wizara ya Fedha kwa juhudi zake kubwa za kukusanya fedha, kukopa fedha nje na kuzileta hapa nchini kwa maendeleo ya uchumi wetu. Naipongeza Serikali hasa Wizara ya Fedha kwa *system* yake ya *cash budget*, imeleta nidhamu kubwa katika matumizi ya fedha hizo. Lakini ningependa kusema kwamba hizo fedha nyingi hivi sasa zinakwenda Wilayani, zinakwenda kwenye Halmashauri katika miradi mbalimbali ya *MMEM*, *MMES*, barabara, Shule na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nidhamu ambayo inaonekana katika Mawizara haonekani huko kwenye Halmashauri. Hizi fedha zikifika katika Halmashauri zinatafunwa kweli kweli. Barabara nyingi ambazo zinatengenezwa hazifanani na fedha ambazo zinapelekwa huko. Madaraja mengi ambayo yanajengwa hayafanani hata kidogo na fedha ambazo zinapelekwa huko. Sizungumzii Wilaya ya Kyela. Huko nyuma nimelalamika juu ya miradi fulani fulani. Nazungumzia uchumi wa Tanzania pamoja na bajeti hii ambayo imeletwa hapa ndani, ya bajeti kuna *hidden problem* na *hidden problem* hii ni wizi. Fedha nyingi haziendi kufanya kazi inayokusudiwa kuwainua wananchi wetu huko Vijijini. Ningeiomba Wizara ya Fedha ifanye kama ilivyofanya Wizara ya Ujenzi iwe na *Technical Audit Unit*, iwezeshe kufuatilia hizo fedha na kuona kama miradi hiyo inafanana na thamani ya fedha hizo zinastahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Naunga mkono hoja zote mbili. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kushiriki tena kwa mara ya tano kwa sababu ni bajeti ya tano napata bahati kushiriki kuichangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwanza kabla sijaanza kuchangia nataka niungane na wenzangu kutoa pole kwa Marehemu Abu Kiwanga, mwenzetu ambaye alikuwa ni Mbunge hapa hapa ambaye ameshafika mbele ya haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nikipongeze Chama cha Mapinduzi kwa kufanya Vikao vyake na kufikia hatma ya kupata Mgombea wake wa Urais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania ambaye ni Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Ningeikiomba Chama cha Mapinduzi kisijiingize katika malumbano yaliyokuwa hayana maana na Wapinzani tsubiri siku ikifika tumalize, tuchukue jukumu la wananchi watakalotukabidhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nataka nirudie kuwapongeza Mawaziri wa Wizara hizi mbili. Kwa kweli Serikali yetu ilikuwa inasema sera yake ni ya ukweli na uwazi. Hotuba hizi za bajeti mbili zimethibitisha hivyo. Nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Waziri wa Fedha pamoja na Watendaji wao wote. Kwa kweli wamelifikisha Taifa hapa kwa mafanikio makubwa sana, wanaopinga hawatakuwa na sababu zao lakini sisi lazima tujivunie tukiangalia hali halisi ya nchi inakotoka. Vile vile, nataka niseme kwamba naiunga mkono bajeti hii asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikichangia bajeti za Wizara hizi mbili nitagusia tu baadhi ya maeneo kama kuthibitisha kwamba ninaiunga mkono kwa asilimia mia kwa mia na vile vile kutoa maombi na mapendekezo yangu kwa Wizara hizi mbili kwa faida ya Serikali yetu na wananchi kwa jumla. Nataka niipongeze hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango. Kwa kweli alipotuambia kwamba uchumi umepanda kwa asilimia 6.7 ni mafanikio makubwa sana. Nimeona katika magazeti kwamba wenzetu Kenya uchumi wao umepanda kwa asilimia 4.3, imeonyesha ni mafanikio makubwa sana.



Pamoja na kwamba Kenya uchumi wao ni mkubwa lakini tukifikiria kwa muda ambao nchi yetu imeanza harakati hizi kimaendeleo ni mafanikio makubwa. Hatuna budi kuwapongeza sana wenzetu wa Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Watendaji wao wote kwa jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna moja ambalo kidogo limenishtua, bado katika taarifa zetu, Wizara ya Mipango inatambia kwamba deni la Taifa limezidi kuongezeka na sababu kubwa inasema inatokana na riba ya madeni ambayo hatujasamehewa. Hivi tunasubiri mpaka tusamehewe jamani?! Ni vizuri tukaendelea kulipa madeni haya tukaondokana na aibu.

Ni kweli kwamba Mataifa makubwa yana mpango wa kutafuta kusamehe madeni ya nchi maskini. Lakini ni vizuri tukajibana tukajikamua japo kwa asilimia fulani tunalipa madeni haya. Kwa hivyo, naitaka Serikali kwamba maeneo kama haya kwa siku za mbele zinazokuja tusiyaone ili kuleta heshima ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango ametueleza kwamba kuanzia mwaka 1995/2000 Sekta ya Kilimo imechangia asilimia 48.5 ya pato la Taifa. Kwa kweli ni pongezi kubwa sana. Hapa tutaona umuhimu gani wa kilimo kuweza kusaidia uchumi wa Taifa hili! Lakini vile vile, ikatambia kwamba asilimia 66 ya mapato ya fedha za kigeni inatokana na kilimo na pia kutoa ajira kwa asilimia 70 ya Watanzania wote. Ni maeneo matatu muhimu sana.

Ni vizuri kwa Taifa letu hili tukaliangalia eneo hili kwamba tumeingiza pato la Taifa asilimia 48.8. Kwa hiyo, inawezekana kama tutakwenda zaidi kwenye kilimo, wataalamu wetu wa kilimo wakaenda Vijijini kusaidia wananchi kuwapa taaluma na nyenzo zote tunaweza kufikia yale malengo ambayo yanaweza kukwamua Taifa letu katika uchumi duni kabisa. Kwa hiyo, nataka niombe Serikali kwamba ielekeze nguvu zake katika masuala ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka niligusie, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango, inasema kwamba Serikali itaendelea na ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma. Hili nataka nimwombe sana Mheshimiwa Waziri wa Mipango, pamoja na juhudi kubwa alizochukua kutembea baadhi ya sehemu ya nchi kulielezea kwa uwazi ambao wananchi walikuwa hawaelewi kwa mambo ambayo walikuwa wenzetu Wapinzani wakilizungumza kinyume na vile ilivyokuwa ikitakiwa. Kwanza nikupongeze sana. Lakini vile vile, suala la ubinafsishaji linaleta mgogoro tunaomba Serikali iliweke wazi sana ili kuondoa malumbano katika nchi yetu kuwayumbisha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizungumzia suala la ulinzi na usalama, ni pamoja na masuala yanayogusa wananchi. Suala la ubinafsishaji sasa hivi linawagusa sana wananchi, wanayumbishwa. Serikali inasema hivi, Wapinzani wanasema hivi, ni vizuri tukaliweka wazi zaidi ili kuwaondoa wananchi katika migogoro ambayo haina maana ili kulipeleka Taifa letu mbele katika maendeleo makubwa sana huko mbele ya safari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka nilizungumze ni kuhusu hii sera ya msimamo wa Serikali, inasema kwamba ni kudumisha ushirikiano mzuri wa kidiplomasia uliopo kati yetu na nchi karibu zote na Taasisi za Kimataifa na Mashirika mbalimbali kwa manufaa yetu sote. Ilikuwa ni kwa manufaa ya nchi zetu karibu zote. Naiomba Wizara ya Fedha, Wizara ya Mipango na Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kweli sasa hivi imefika muda tukawa wakweli kwa majirani zetu Kenya, Uganda, *DRC* na Burundi.

Nchi hizi zinaweza zikarudisha nyuma uchumi wa nchi yetu. Sasa hivi imejitokeza kwamba baadhi ya wenzetu hawa Waganda na Wakenya wanashiriki kufanya vitendo vya uhalifu katika nchi yetu ya Tanzania. Wanasababisha wizi katika Mabenki yetu. Ukisababisha wizi katika Mabenki unaweza kuua uchumi na wenzetu hawa wa *DRC* na Burundi wanafanya vitendo vya uhalifu katika mipaka yetu ya Tanzania kama Rukwa, Kigoma na maeneo mengine. Kwa hiyo, ni vizuri tukawa wawazi ili kuulinda uchumi wetu. Kwa hiyo, hili ningeliomba sana Serikali yetu kwa mafanikio makubwa liweze kulisimamia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye Wizara ya Fedha, nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Mramba kwa juhudi zake zilizoonekana na mimi nataka nikiri kwamba juzi aliposema katika wale wafungaji wa magoli kweli yeye ni mmoja na ni kweli kabisa. Ni bajeti yake ya tano nashiriki kuchangia. Tumeona juhudi zake, aliyekuwa hataki muache kama alivyo. Tekeleza wajibu wako, siku yako ikifika utaondoka, lakini utakuwa umeshatoa mchango wako wa Taifa la Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika changamoto zilizopo mbele yetu anasema Mheshimiwa Waziri kwamba nchi yetu bado ni maskini. Imekuwa wazi sana hotuba yako. Tunataka wenzetu waelewe hivyo. Waziri amekiri hili pamoja na hesabu yote ya fedha anazotoa kwa Taifa letu, pamoja na mikakati yote ya Serikali ambayo inalenga kupunguza umasikini, lakini amekiri kwamba nchi yetu ni maskini. Tunataka wenzetu waelewe hivyo! Sasa kutuletea siasa ambazo wanaweza kwenda kinyume na hili, wanaweza kuiyumbisha nchi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mramba nataka nikupongeze sana. Lakini vile vile ukasema idadi ya watu inaongezeka karibu asilimia tatu kwa mwaka. Tunalazimika kuongeza kasi kukua kwa uchumi wetu hadi kufikia asilimia 10 kwa mwaka. Hebu tuangalie malengo haya ambayo sisi tumeyapanga. Sasa wenzetu wanapokuja na bahati mbaya wao wanasababisha vurugu katika nchi. Bila aibu, Profesa Lipumba ni Profesa, mtu ambaye ni mchumi, hakuandikishwa tu; Maalim Seif Zanzibar anasema kama Zanzibar haikaliki. Hivi kweli kutakuwa na maendeleo katika nchi hii kwenye vurugu? Ni Profesa na ni mtaalamu katika masuala ya uchumi!!

Huku sisi tunasema kwamba idadi yetu inaongezeka ya watu kwa asilimia tatu kwa kila mwaka na tunahitaji kulazimika kuongeza kasi kukua kwa uchumi wetu hadi kufikia asilimia 10 kwa mwaka kutoka pale 6.7. Kwa hiyo, ni vizuri tukaelewana tukaondokana na jazba hizi ambazo hazina msingi, tukafikiria maslahi ya watu, maslahi ya Taifa. Twendeni katika uchaguzi, ukishindwa unga mkono tujenge Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, inasema kwamba bajeti yetu bado ni tegemezi. Tukiangalia kwamba uchumi mmetuambia kwamba pato la Taifa limeongezeka. Ili tuondokane na tegemezi lazima turudi kwenye kilimo kwa haraka sana. Tusitegemee mvua, twendeni kwenye vyanzo vyetu vya maji vilivyomo katika nchi hii. Tuache kusema, tuache siasa tufanye kazi. Mpeni fedha Mheshimiwa Keenja achukue wataalamu wake aende nao Vijijini kuwatumikia wananchi sio kukaa maofisini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri inasema “Katika mwaka wa 2005/2006, Serikali itaendelea kuimarisha nidhamu katika matumizi ya fedha za Umma. Tunakupongeza sana Mheshimiwa Waziri na kuhakikisha uwajibikaji. Hongera sana! Inasikitisha kuona katika nchi hii fedha zinapotea bure. Hata hizi za *MMEM*, nilisoma katika gazeti moja hivi karibuni kwamba kuna Shilingi milioni 40 zimepotea katika Halmashauri moja. Wananchi wanapoona fedha zao kama zinapotea, kwa kweli unaanza kuwarudisha nyuma.

Lakini hili lingine la kuhakikisha uwajibikaji mimi niombe Serikali ihakikishe kwamba wale wastaafu wote wa Serikali ambao wanastaafu iweze kuwalipa mafao yao mapema sana kwa njia yoyote ile itakayowezekana. Kazi moja kubwa ni kuwajibika, kuweza kuwapa huduma watu ambao wamelitumikia Taifa hili kwa mafanikio makubwa wakaweza kupata haki zao kwa muda mfupi bila usumbufu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri hili nataka nikuombe hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nataka nilizungumze hapa niombe Serikali ifanye utafiti kwa ile Mikoa na Halmashauri ambayo madaraja yao yameharibika kwa ajili ya mvua yaweze kuyafanyia matengenezo ili Wakuu wetu wa Mikoa waweze kutoa huduma kwa wananchi katika maeneo yale ambayo sasa hivi inaonekana kwamba hayafikiki. Kwa hiyo, Serikali ianze kufanya utafiti huo ili wananchi waweze kupata huduma kwa Viongozi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naiunga mkono Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kununua magari ya *VX* na *GX*. Nchi yetu ni kubwa sana, wananchi wanahitaji huduma kwa Viongozi wao. Hatuwezi kuitawala nchi kubwa kama hii kwa kusema wakubwa wetu watembe na *Vi-Scudo* na magari mengine. Ni vizuri tukaangalia umaskini wetu sio utufanye tuji-*broke* kwamba ni eneo fulani tujilazimishe wananchi wanahitaji maendeleo. Nchi inahitaji maendeleo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hotuba hizi asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naomba na mimi niungane na wenzangu katika kuwapongeza Watendaji wa Wizara hii ya Fedha. Lakini pongezi za pekee ziende kwa Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Alhaj Mufti Abdisalaam, Mheshimiwa Limbu na Mheshimiwa

Alhaj Abdallah Kigoda wao pamoja na Watendaji wao. Kwa kweli wamefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikuwa na nia sana ya kuchangia katika hotuba hii, lakini hapa wamekuja Viongozi wa Umoja wa Wastaafu Tanzania. Viongozi hao wamekuja kwa sababu ya matatizo. Ni jambo la aibu kuona wazee wetu ambao wametufikisha hapa tulipofika, inabidi watufuate mpaka huku kwa kutuona kwamba tumewasahau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuipa pongezi Serikali kwa kuongeza kiwango cha mafao ya pensheni na pia kuwarudisha wale waliochukua pensheni kwa mkupuo, lakini bado kiwango ni kidogo mno. Kiwango cha chini cha pensheni sasa hivi ni Sh.20,077/=. Sasa fedha hizi wanapata wale ambao wamestaafu kabla ya mwaka 1997 awe Balizi au alikuwa Mkurugenzi alikuwa nani atapata hizo hizo Sh.20,077/=. Yeye na Ofisa wake wa chini pengine Alikuwa Mhudumu wake, wote wanapata Sh.20,077/=. Hapa tuna Viongozi wetu Makatibu Wakuu, Mabalizi wamelitumikia Taifa hili na tumefika hapa tulipofika leo Kwa Sh.20,077/= hawawezi hata kulipa umeme, bili ya maji na vitu muhimu kabisa hawawezi kuvifikia. Kweli Taifa hili linataka kuwaona wastaafu wake wakiwa ombaomba au tunawaweka sehemu gani?

Wao wenyewe wapo hapa na wamesema kwamba wanaomba Serikali iwafikirie kwa sababu wanaona kuna *anomaly* kubwa sana. Leo Afisa yoyote yule ambaye atastaafu sasa hivi atapata fedha nzuri ataishi vizuri kuliko wao. Lakini nia kubwa ya pensheni ni maelewano ya kuwa mstaafu aishi maisha ambayo ni *reasonable* kwa maisha yake yote kulingana na wadhifa alioachia. Sasa tukiwaacha hawa katika lile kundi la Sh.20,077/= wa kweli ni kuwaonea.

Naomba Waziri wa Fedha nadhani pengine hili mlipitiwa kidogo mlitizame mwangalie waliostaafu kazi wakiwa na kiwango gani cha mshahara isiwe wote wanakwenda mkumbo mmoja na isionekane kama ni *favour* kurudishwa kwenye daftari, ni utaratibu tu ambao Serikali yetu imefikia na kuona wanapata taabu. Sh.20,077/= huwezi kununua hata dawa! Siku hizi ukiandikiwa *prescription* ya dawa, inafika hata shilingi 30,000/=. Kwa hiyo, kwa kweli tumewaweka katika hali mbaya na wanaweza kufa kwa sababu ya machungu tu ya maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwazungumzia wastaafu, sasa ningependa nizungumzie hili suala la kwamba sasa wale wastaafu, mafao ya wafanyakazi lililokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki sasa watalipwa mafao yao. Kwa kweli, hiyo nimeifurahia sana na wananchi wamefurahi sana. Leo nimepigwiwa simu mchana huu kutoka Dar es Salaam, naambiwa tumefurahi sana, lakini hii sio mara ya kwanza, tumeahidiwa katika bajeti kama hizi kwamba mafao yatalipwa. Lakini hofu kubwa walivyokuwanayo ni kwamba watalipwa kwa kiwango gani? Wale wafanyakazi wa waliokuwa Afrika Mashariki iliyokufa nadhani tokea mwaka 1977 hawajalipwa mpaka leo. Kwanza hiyo sio haki wengi wamekufa, wengi wako taabani kwa maisha, sasa watalipwa kwa kiwango gani? Wakati fulani nilikuwa Mkurugenzi *Air Tanzania* walikuja kulipwa mafao yao *calculation* yao iliambiwa walilipwa wale kwa dola ya mwaka 1977. Basi, iliambiwa

walipwe kutokana na *rate* ya mwaka 1977. Wale wafanyakazi wengine walizisusa hawakwenda kuzichukua.

Kwa hiyo, naishauri Serikali ihakikishe wanalipwa wafanyakazi waliokuwa wa Afrika Mashariki mafao yao kwa *rate* ya leo au ya kesho au ya siku ile ambayo wanapokea yale mafao yao, hapo itakuwa haki. Si haki! Umemcheleweshea mtu mafao miaka yote sasa uende ukamlipe kwa *rate* ya Shilingi saba kwa dola! Kwa kweli hiyo haiwezekani! Makosa sio yao, wamekuwa wakilalamika siku zote, tumeona walivyolalamika wazee wetu, wamekwenda mpaka Wizarani kwa bahati watu wa ajabu ajabu wakaanza kuwapiga! Wazee hawana jiwe wala hawana nini, *FFU* ikaleta fujo yote ile katika kutafuta haki zao. Ni kweli unapotafuta haki huwezi kuipata kwenye *silver plate*.

Lakini pale kwa kweli walionyesha kwamba wako *desperate* na wamekuja wamefanyiwa kama ilivyokuwa na imekuwa vizuri Waziri kwa busara yake na timu yake wameona wawalipe. Basi muwalipe ilivyokuwa haki au watagoma tena. Kwa hiyo, Serikali naamini Waziri ataishauri Serikali vizuri ili walipwe kwa kiwango ambacho wanastahili zile dola, maana yake *payment* yao ilikuwa *paid* kwa dola, walipwe kwa dola za sasa na sio kwa wakati ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia Wastaafu, napenda nizungumze tena kuhusu *speech* ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Katika *speech* ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, amesema unaanzishwa Mfuko Rasmi wa kutoa *Funds* kuhusu magonjwa ya kuambukiza hususani *UKIMWI*. Hilo ni jambo jema na tumelipokea vizuri. Lakini wasiwasi wangu ni utaoji wa fedha hizi. Ikumbukwe na ifahamike kwamba wenzetu wa *NGO's* (Mashirika yasiyo ya Kiserikali) wanafanya kazi kubwa sana. Ni *partners* wetu ambao wao ndiyo wako karibu na wagonjwa na wao ndiyo wako karibu na watoto yatima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa ndiyo wenye kufanya kazi yenyewe. Serikali haina uwezo wa kuwafikia Vijijini na sehemu nyingine. Sasa kuna tatizo ambalo limejitokeza, hizi *NGO's* zikiomba pesa leo inaweza kuchukua mwaka mpaka kuzipata. *Research* inafanywa, wanaandika *write up*, lakini unapochukuwa zaidi ya miezi sita kutoa hizo pesa maana yake wagonjwa wameshakufa kwa njaa, dawa hazijapatikana na matatizo mengi yanatokea kutokana na ucheleweshwaji.

Najua lazima kuwe na utaratibu, lakini urasimu umezidi wa kutoa fedha za *UKIMWI* kwa *NGO's*. Kwa hiyo, naomba Serikali ilishughurikie suala hili ili kusudi wagonjwa wa *UKIMWI* waweze kupata huduma zile ambazo tunatarajia wapate, kwa kuwa sasa hivi shughuli ya kuhamasishana imekwisha. Kila mtu anajua madhara ya *UKIMWI*, kila mtu anajua madhara ya *UKIMWI* na kila mtu anajua kuna gonjwa la *UKIMWI*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *T-Shirt* tumevaa sana, sasa utakuta sisi tunavaa *T-Shirt*, mgonjwa wa *UKIMWI* mwingine hana hata shati. Kwa hiyo, hizi pesa ziwe *directed* moja kwa moja kwa wagonjwa wa *UKIMWI* kupitia *NGO's* na iwe wale wenye

NGO's wapewe muda mfupi sana wa kuleta ripoti zao kurudisha *returns* zao jinsi walivyotumia zile pesa ili waathirika wengi zaidi wafaidike na hizi pesa ambazo zimepangiwa wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kuhusu kilimo na umaskini. Mimi sio mkulima, lakini naona jinsi neno la ukulima linavyoandikwa kila siku tangu nilipoingia Bungeni. Naona aibu kusema hata nimeingia mwaka gani! Tumezungumzia kilimo kila mwaka, kwa majina ya kila aina, lakini kwa kudharau na kutokutilia mkazo na kutokuwekea *priority* kilimo ndiyo maana mpaka leo tunajiita sisi maskini. Nchi yetu sio maskini. Mimi nakataa kabisa kusema kwamba Tanzania ni maskini, unapojitia unyonge wewe mwenyewe na kweli utakuwa mnyonge. Sisi sio maskini! Tuna kila kitu cha kutufanya tuwe tajiri! Tuna watu, tuna raslimali chungu mzima, mito mikubwa mikubwa iko Tanzania (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mito yote inakimbilia baharini, nani kasema bahari inahitaji maji ya mito? *After all* maji ya bahari yanazidi kuja juu kwa sababu kule barafu inayeyuka. Kwa hiyo, haihitaji kabisa maji ya mito yaende baharini, kwa nini tunaruhusu? Hapa lipo tatizo. Wataalamu wapo, tuna Chuo kizuri! Nakumbuka sijui mwaka wa ngapi sasa, hatuwaoni. Lakini kila mwaka tukija hapa tunazungumzia matrekta, tunazungumzia kilimo, lakini hakuna kinachofanyika. Sasa mwaka huu ndiyo hayo tumeambiwa tena, lakini mimi nahakikisha kabisa. Nina uhakika watu watalima mwaka huu tena kwa jembe la mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jembe la mkono ni umaskini, tunajiendekeza na jembe la mkono ambalo ni umaskini. Kama tunaweza kununua mashangingi aliyosema Mheshimiwa Mjaka, nadhani pia tunaweza kununua matrekta. Bei ya trekta sio kubwa, shangingi moja unaweza kupata matrekta hata matatu. Hivi kuna ubaya gani tukiwa na utaratibu mzuri wa kuwasaidia wakulima wetu wasiendelee kulima chakula chao na hicho hicho tutegemee sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa muda huu ambao najua umeni-*squeeze* tu. Nashukuru, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. DR. AMANI W.A. KABOUROU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nianze tu kwa kutoa pole kwa niaba ya Wapigakura wangu wa Kigoma Mjini na mimi mwenyewe kwa msiba wa Ndugu yetu Mheshimiwa Abu Kiwanga na namwomba Mwenyezi Mungu amweke mahali pema huko Peponi. Amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, vile vile niwapongeze Wagombea wote walioteuliwa na Vyama vya Siasa katika kinyang'aro cha Uchaguzi cha mwaka 2005, kwenye ngazi ya Urais. Kwa kweli ndiyo mfumo wa Vyama vingi unavyotaka na ninadhani sasa tumeanza kuuelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze haraka haraka tu, kwa kuunga mkono hoja iliyochangiwa na Wabunge wengi hapa, kuhusu suala la Wastaafu hao wa *East Africa*

ambao wametengewa Shilingi bilioni 50 naamini, walipwe. Kwa kweli naomba hili lisije kuwa hadithi kama ilivyokuwa mwaka juzi. Mimi mjomba wangu amestaafu kutoka Posta miaka mingi na nilimwona kabisa ana hamu kubwa ya kupata fedha hizo. Ni mzee sasa, lakini mimi nikamwambia mjomba bwana angalia watu hawa, badala yake tukawaona Wazee wanapigwa na *Field Force*, sasa sijui maana yake nini? Kwa kweli ni utamaduni hata usio wa Kiafrika tena. Mimi naomba tu safari hii wapewe pesa zao isije kuwa hadithi wanazihitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, labda nikubaliane vile vile na hoja na ninadhani mimi kama Mpinzani mwaka 1994 nilikuwa nikiongea kwamba, jamani Tanzania sio nchi maskini ina kila kitu. Mkasema waongo hao. Lakini mimi nashukuru sasa tunakubaliana kwamba kwa kweli sisi sio maskini. Sasa yale mawazo ya kimaskini hatuyataki na ninashukuru katika *Budget Speech* ya Mheshimiwa Mramba amesisistiza kabisa na ni heshima kubwa kuuchukua umaskini na mimi nakubali.

Maana yake mawazo ya mtu kuwa na suti mbili, kuonekena afatwe na *security*, kanywa bia nne, mambo ya *ki-communist*, yaani mtu huruhusiwi kuwa na nyumba, mtu anesema kuna hekalu kule Mbezi *Beach*, mimi sijaona hekalu pale naona nyumba za kawaida tu. Lakini mtu anasimama anasema majumba makubwa, sasa wewe ulitegemea watu wakae katika nyumba ya namna gani? *Ngondano!* Sisi tunataka watu wakae vizuri, tukatae umaskini, kwa sababu tuna uwezo. Sasa kama kuna mtu ana mawazo finyu atupishe, aende Uchina huko ambako labda watakubaliana na mawazo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, nisisitize kwamba, suala la ubinafsishaji, nashukuru kwamba *CCM* baadaye wameliona hili, tunajaribu kulitekeleza, najua kuna mapungufu ya hapa na pale. Kwa kweli siwezi kukubali kwamba asilimia tatu kwa madini yetu inatosha, hata mngeniambiaje! Nasema Mikataba ipitiwe upya na sisi tupewe kibanzu cha kuanzia, asilimia 25, 30 halafu tukatane kodi baadaye. Haiwezekani mtu aje achukuwe pesa Sh.100/= anakupa Sh.3/=, kwa sababu nilimjengea na ndugu yako wa kule Geita barabara ya udongo na nikawajengea na Zahanati, chumba kimoja hakina hata mashine! Hapana! Tuwe na kibanzu kabisa asilimia 25, 30 halafu mengine tunachangia na hawa watu. Kwa hiyo, mimi nasema ubinafsishaji ni sera nzuri, mimi ni muumini kabisa, lakini lazima tuwe na ufanisi katika kubinafsisha mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli sikubaliani na mtu anayesema tusibinafsishe, nadhani hiyo ni kurudi nyuma, kwa sababu hata hao tunajitia kusema ndiyo *development partners* wa Tanzania na kadhalika, wote wanatoka kwenye sera za ubinafsishaji. Mimi naona woga sana ninaposikia watu hapa wanang'ang'a nia Serikali inabinafsisha, Serikali inabinafsisha, Serikali itatoa wapi pesa za kufanya vitu vya nanma hii.? (*Makofi*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuwaruhusu wananchi wafanye kazi hizi. Unang'ang'ania Serikali tu, ikuletee kila kitu? Wanasema Ulaya, Amerika, ng'ombe anapewa hela nyingi kuliko mkulima wa hapa na wewe wape basi wakulima wako kama unazo. Wape! Tusijidanganye hapa, zinaletwa hadithi tunasikia sisi tunalima kisichotakiwa tunauza, wao wanatuuzia tusichokitaka! Mimi naona huku ni kutoelewa!

Hivi nani kasema kwamba Amerika nchi ile uchumi wake unategemea viwanda peke yake? Wale wanalima kuliko mtu yeyote! Dunia nzima mkipata njaa mnakula chakula kutoka Amerika.

Kwa hiyo kilimo ni sehemu kubwa sana kwa uchumi wa Amerika! *Very big!* Lakini ufanisi wa wenzetu ni kwamba wenzetu asilimia mbili wanalima na kulisha asilimia 98. Sisi huku tuko kwenye asilimia 90 wanalima na hawajilishi wenyewe na kuna tatizo la njaa, anasimama mtu anasema tupeleke na asilimia mia huko huko!!!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tusitengeneze mkakati mpya? Tumesikia hapa hadithi za *Asian tigers*, walilima, walifanya nini, wanajenga uchumi, uchumi gani? Nani hajui kwamba *Asian Tigers* wao walikuwa ndiyo *manufacturing agency* wa Amerika wakati wa vita na Vietnam, kwamba ndiko walikopata mitaji yao, mitaji isiyohesabika? Tunajisemea maneno ambayo hayawiani na ukweli kuhusu *Asian Tigers!*

Malaysia wamefanya vizuri. Zamani walikuwa wao ndiyo wanalima mpira kuliko nchi yoyote duniani. Walipoona mpira unashuka bei wakaja Kigoma wakachukuwa mbegu za michikichi mnaita huku, sisi tunaita migazi, wakaenda na Nigeria wakachukua mbegu za migazi wakapeleka kule, wakatengeneza *plantation* kubwa kabisa ya michikichi migazi, leo wanapata *four to six billion US Dollars* na bei ya mafuta ya mawese haijashuka. Ni aibu kwamba sisi tuliowapa mbegu, leo tunanunua Korie kutoka kwao, leo tunaweka vinasa wakwepa kodi pale Bandarini, kwa sababu wafanyabiashara wakubwa wa Tanzania sasa wananunua mawese kutoka Malaysia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wenzetu waliona wawe na *comparative advantage*. Niambieni hapa Tanzania *comparative advantage* yetu ni nini? Ni hii tu kugawana Bajeti! Mwaka jana ilikuwa *trillion 2.7* mwaka huu *trillion 4.5*, ni nini sasa kinachojengwa na mwaka kesho tutarudi tena hapa hapa? Tumeongeza matumizi ya kawaida, ni yapi sasa? Takrima! Ulikuwa unakuja Ofisini kwangu nakupa biskuti mbili mwaka jana, mwaka huu nakupa nne, ilikuwa chai ya rangi imekuwa na maziwa, ndiyo tutakwenda hivyo? Hela zimeongezeka! Kama ni kweli, basi ziongezeka kwenye uzalishaji, kwenye kuongeza tija! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba kidogo utegemezi umeondoka asilimia 48, sijui 42 iliyokuwa tumeshuka mpaka asilimia 40, tunashukuru. Lakini tunataka pesa zinazongezeka kimapato kwa mwaka zipelekwe kwenye uzalishaji. Mimi naona ajabu, tumekwenda kwenye Wizara ya Ujenzi tukaona tuna bilioni 344, mimi nikasema kwa nini isiwe *trillion* moja ya kujenga barabara mwaka huu?

Tulikuwa na *trillion 2.7*, leo tuna *trillion 4.5*, kwa nini *trillion* moja isijenge miundombinu? Kwa nini na zenyewe ziishie kuliwaliwa tu? Kwa hiyo, mimi nasema haya ni mambo ya kuangalia sana na sisi tupo hapa, tumekuja, tumeona, tumesema, tunashukuru kuna watu wanasikia na wanayafanyia kazi. Wazungu wanasema: "*They are lies then lies and statistics*", kwamba uongo wa mwisho kabisa ni *statistics (takwimu)* tuziangalie sana.



Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaambiwa kilimo kimechangia asilimia 49 ya pato la Taifa au 48.5 ya pato la Taifa. Mbona hatufafanuliwi hapa ni pato gani *GDP* au *GNP*? Kama tunakubaliana kwamba pato ndio tunalolizungumzia hapa ni asilimia 13.8 inayokusanywa na *TRA*, hatudanganyani hapo, hili ndilo pato la Taifa na kwanini tuwe kwenye asilimia 13.8? Zamani wakati wa *Roman Empire* kulikuwa na watu wanaitwa *Tax Farmers*. Hiyo kazi ya kukusanya kodi maeneo fulani kuchangia *Roman Empire* ikacharuka dunia, jenga Ujerumani, jenga Uingereza, jenga kila mahali na wangeweza wangevuka mpaka Amerika wakajenga. Pesa nyingi, uwezo mkubwa kwa sababu walikuwa na uwezo wa kukusanya. Sasa sisi tunang'ang'ania tu, asilimia 13.8 halafu linaitwa pato la Taifa! Hapana! Mimi ningependa ufafanuzi kwenye hili, ni *GDP* ni *GNP*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme baada ya hayo kwamba kwa kweli tuwe *serious*. Mimi nakubali, *efforts* zinaonekana, kweli ni dhahiri basi kwamba, kama zamani tulikuwa tunakusanya bilioni 25 na kumbe kuna uwezekano wa kukusanya bilioni 145 kwa sasa, ni dhahiri kabisa kwamba kulikuwa na upuuzi. Sasa tumeanza kuondokana na upuuzi huo, lazima tufurahie hilo. Lakini kuna mambo leo, tuchukue fani ya Madini. Ilizungumziwa kidogo katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango, akazungumza jinsi ambavyo ataboresha na nini.

Lakini mimi nasema leo kule kigoma yamegunduliwa madini yanayoitwa *colten* yanatengeneza simu za mkononi. Mimi sijaona hata mpango wa kusema na ndio madini ya moto haya, yanapatikana Kongo na Australia na simu za mkononi zimeongezeka duniani kuliko sijui hata jangwa. Hatuchimbi! Tutangoja mpaka yatakapokuwa hayana thamani tena tuje tuyauze kwa asilimia moja kwa sababu yatakuwa hayana kazi tena. Sikuona mimi, naona ajabu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema tujitahidi kuwa na kitu cha *comparative advantage*, tuwe na kitu cha kuonyesha basi, isiyokuwa bajeti hizi za kula kula tukaongezewa. Nilivyofika hapa zamani kulikuwa hata na mchezo kwamba wanasimama kabisa mfanyakazi anasema, mimi sijapandishwa cheo kwa miaka miwili bwana, sasa wewe ulitaka upandishwe cheo tu kwa sababu umekaa pale bwana. Yaani hutuambii ulichofanya tukupandishe cheo tu na anasimama *trade unionist* anamtetea, wanafanya maandamano hawajapandishwa vyeo. Tutakuwa na *too many chiefs and very few Indians* na nchi haiwezi kwenda hivyo, kila mtu ana cheo hakuna wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningependa nipendekeze hapa kumekuja wazo zuri. Kwa bahati, mimi natoka Kigoma ambako huko hakuna kitu mzee. Tumezungumza lami hapa na maendeleo na nini, hakuna lami yoyote iliyojengwa Kigoma na tumeambiwa tunajumuika, hakuna, barabara ya Kigoma, Tabora inazungumzwa kama nadharia. Reli inaitwa treni ya Waha, ina nyani sijui, panya, kunguni vitu gani wamo mle ndani, haina taa.

**MBUNGE FULANI: Manamba**

**MHE. DR. AMANI W.A. KABOUROU:** Sasa wengine wanasema Manamba, haya basi, mambo ya ukoloni hayo! Sasa msitugeuze sisi watumwa wenu!!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kimezungumzwa kitu kizuri kuondoa *VAT* kwenye vipuri vya *railways* na *marine services*, mimi naunga mkono hili. Lakini ningependekeza kiongezwe kitu kingine vile vile. Hawa *railways* ili waweze kutusaidia wanahitaji vile vile kuingizwa kwenye Mfuko wa Barabara ambao unatoa pesa zake kutoka kwenye makusanyo ya mafuta. Kama hatuwapi pesa kutoka Mfuko wa Barabara, basi tuwasamehe kodi ya mafuta vile vile ili pesa zile ziwasadie na sisi watuendeleze kihuduma na hii ni pamoja na Meli za Ziwa Tanganyika, Meli za Ziwa Victoria na Meli za Ziwa Nyasa kwa sababu wote wananunua mafuta ya *diesel*.

Lakini mgao unaishia kwenye kujenga barabara na kusaidia barabara, reli haina kitu na reli inakufa na ninasikia Novemba tutawakabidhi *South Africa* na wao watatengeneza mkakati wao wa kutumaliza kabisa na mizigo yote iende zake Durban na Dar es Salaam ibakie hivi hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa niseme kwamba daraja letu la Kigamboni, Mheshimiwa Magoba nadhani hili limekufika. Daraja letu la Kigamboni lijengwe isije kuwa hadithi wengine tunakaa kule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, mimi napenda tu niseme tu kwamba naiunga mkono Bajeti hii lakini kwa kuzingatia kwamba tunakwenda na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja hii ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Kwanza, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Manaibu wa Waziri, Makatibu Wakuu pamoja na Viongozi wote wa Wizara hii. Kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mimi nimeingia katika Bunge hili mwaka 1990, wakati huo tulikuwa tunakusanya fedha kidogo sana kwa mwezi. Lakini leo Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa *TRA* wanakusanya bilioni 145, fedha ambazo zimetusaidia kuboresha huduma za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kukusanya bilioni 145 sio kazi ndogo, ni kazi kubwa sana, ni juhudi ambazo wamefanya wenzetu Wizara hii ya Fedha. Kwa hiyo, ni lazima tuwapongeze sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani tulikuwa na usemi kwamba fedha si msingi wa maendeleo, lakini fedha ndiyo msingi wa maendeleo kwa sababu bila fedha huwezi kujenga daraja, bila fedha huwezi kununua dawa, bila fedha huwezi kutekeleza miradi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti sasa nichangie kidogo kuhusu sekta mbali mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Sekta hii ya Mawasiliano-barabara. Bado tunaikumbusha Serikali barabara ya kutoka Minjingu, Babati, Kondoa, Dodoma, Arusha.

Hii barabara ni muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu na uchumi wa nchi yetu. Sasa tunapenda tupate maelezo kwamba Serikali imefikia wapi? Lakini vile vile, tukumbushe kwamba barabara ndiyo uchumi, barabara ndiyo maendeleo. Tuna barabara za Mkoa, barabara za Wilaya na barabara za Vijijini.

Kama walivyozungumza, walivyochangia Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba tunategemea mazao toka Vijijini na ndiyo hasa yanasaidia kukuza uchumi wetu. Lakini barabara zetu zina hali mbaya sana. Bado tunaendelea kuishauri Serikali kwamba hii asilimia 30 ambayo wanapeleka kwenye Halmashauri za Wilaya ni kidogo sana. Kwa hiyo, tunashauri angalau asilimia 40 iwe inapelekwa kwenye Halmashauri. Wizara ya Ujenzi ibaki na asilimia 60, Halmashauri za Wilaya zipewe asilimia 40, hapo tutaweza kutengeneza barabara za Vijijini ili ziweze kusafirisha mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sekta ya Elimu, tuna Miradi ya *MMEM*. Serikali imefanya kazi nzuri sana. Sasa hivi hakuna hata Kijiji kimoja ambako hakuna darasa moja jipya. Wamejitahidi kujenga madarasa, tatizo letu kubwa ni upungufu wa Walimu. Sasa hivi tunajenga Shule za Sekondari kila Kata. Wilaya ya Mpwapwa mwaka huu tumefungua Shule nane za Sekondari na hivi sasa wanafunzi 760 wako madarasani wanasoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hizi ni juhudi za Serikali pamoja na wananchi, lakini tuna tatizo kuhusu Walimu. Ni tatizo kubwa na vifaa vya kufundishia na bado tuna tatizo vile vile na majengo ya Maabara katika Shule hizi. Kwa sababu wanafunzi lazima wanaposoma masomo ya Sayansi, wanasoma kinadharia na kivitendo vile vile. Kwa hiyo, tunaishauri Serikali ijenge majengo ya Maabara na kupeleka vifaa kwa ajili ya kujifunzia masomo ya Sayansi.

Vile vile, kuna Shule zetu kwa mfano Shule ya Sekondari ya Mpwapwa, tunaikombea usafiri. Gari ambalo liko pale ni bovu na Shule nyingine za Sekondari ambazo hazina usafiri, Serikali ijitahidi kuwapatia usafiri ili kurahisisha kusafirisha wanafunzi pamoja na Watumishi, Walimu wa maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Maji, naishukuru sana Serikali. Hivi sasa kuna Miradi mikubwa sana ya Maji pale Wilayani Mpwapwa. Benki ya Dunia imekwishatumia zaidi ya bilioni mbili kwa ajili ya Miradi ya maji Wilaya ya Mpwapwa. Hivi sasa zaidi ya asilimia 76 wananchi wa Wilaya ya Mpwapwa wanapata huduma ya majisafi.

Tumetekeleza sera ya kuchangia Mifuko ya Maji. Napenda niwapongeze wananchi wa Wilaya ya Mpwapwa kwa kuchangia Mifuko ya Maji zaidi ya milioni 17 na hii ndiyo sera yetu ya kuchangia Mifuko ya Maji. Lakini bado tunaendelea kushauri

kwamba maeneo yale ambayo kuna ukame, basi Serikali ijitahidi kuchimba mabwawa, malambo ili maji yaweze kutoa huduma kwa mifugo pamoja na binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije Sekta ya Mifugo. Kwanza tunawakaribisha sana kesho Mpwapwa, kuna sherehe kubwa ya kuadhimisha Miaka Mia Moja ya Kituo Cha Utafiti wa Mifugo Mpwapwa. Miaka Mia Moja. Kwa hiyo, tunawakaribisha sana kwa sherehe ya kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo inachangia pato la Taifa vile vile, lakini mifugo yetu inachangia pato la Taifa asilimia 18. Ni kidogo sana ukilinganisha na mifugo ambayo tunayo, mifugo karibu milioni 17.8, lakini mifugo mingi wanakufa kwa sababu ya kukosa huduma. Tuna Majosho zaidi ya 2,024 katika nchi hii lakini majosho yanayofanya kazi ni 476 tu. Kwa hiyo, mifugo yetu mingi wanashindwa kuogeshwa, hivyo wanakufa kwa sababu ya magonjwa ya Kupe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni zaidi ya asilimia 70 mpaka 80, mifugo wanaokufa kwa sababu ya magonjwa ya kupe. Ni aibu sana nchi ambayo ina wataalam Madaktari, ng'ombe wanakufa kwa sababu ya magonjwa ya Kupe. Kwa hiyo, wajitahidi wataalam wetu kuhakikisha kwamba, kwanza tufufue majosho, Halmashauri za Wilaya kusaidiana na Serikali Kuu tufufue majosho ili mifugo hii iweze kuogeshwa na vile vile kuichimbia malambo ya maji ili waweze kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie suala zima la mishahara ya Watendaji wa Vijiji. Tatizo hili limekuwa la muda mrefu sana, na Serikali ilitupa matumaini mwaka jana 2004 baada ya kukubali kwamba sasa watalipa mishahara ya Watendaji wa Vijiji. Wakati tunachambua bajeti ya *TAMISEMI*, tuliona fedha zimetengwa kwa ajili ya kuwalipa Watendaji hawa wa Vijiji. Katika Bajeti ya mwaka jana 2004/2005, Serikali ilitenga bilioni tano kwa ajili ya kuwalipa Watendaji hawa wa Vijiji na nashukuru kwamba wachache walilipwa, lakini idadi kubwa bado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtendaji wa Kijiji ni mtumishi kama Watumishi wengine. Anapokosa mishahara, inamletea shida sana. Ndiyo wanajiingiza kwenye mambo ya rushwa na mambo mengine. Lakini kwa uamuzi wa Serikali, uamuzi wa busara kwamba sasa watawalipa mishahara, naomba nisisitize kwamba mishahara hii ilipwe pamoja na malimbikizo.

Kuna Watendaji wengine wanadai miezi kumi, mwaka mmoja, hawajalipwa mishahara. Kwa sababu sote tunafahamu kwamba Halmashauri za Wilaya uwezo ni mdogo hasa baada ya vyanzo vingi vya mapato kuondolewa, kwa hiyo, hawana mapato ya kutosha ya kuwalipa wale Watendaji. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali, kwa mawazo ya busara, uamuzi wa busara, kwamba Watendaji hawa walipwe mishahara yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilizungumzia sana daraja moja la Godegode, mpaka nilisema kwamba Serikali za Mitaa na Serikali Kuu zote ni Serikali. Sasa, daraja hili la Godegode, nilikuwa nimeomba Serikali mwaka jana kwamba lijengwe lakini halijajengwa hadi sasa. Kwa sababu sasa hivi maji yakishajaa, mwaka

juzi watu wawili walikufa, walitumbukia na ni hatari kwa magari. Sasa naikumbusha Serikali tena, kama mnanitakia nia njema, basi mjenge daraja hilo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri wa Fedha, lakini, naomba sana haya mambo ya kutupiana mpira kwamba sasa ni Serikali za Mitaa, Serikali kuu, yote ni Serikali. Naomba sana daraja lile lijengwe. Ni daraja muhimu sana kwa sababu ndilo linalounganisha Jimbo la Mpwapwa na Jimbo la Kibakwe na ni maeneo ya barabara inayokwenda maeneo ya uzalishaji ya umwagiliaji Lumuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hiyo ni muhimu sana. Kwa hiyo, ninaomba sana, nimetumwa na wananchi wangu wa Vijiji vya Godegode, Kisisi, Mzogole na Mgoma pamoja na wananchi wa Pwaga, kwamba nieleze Serikali daraja lile ni muhimu, wajenge daraja. Nashukuru Mheshimiwa Waziri wa *TAMISEMI* alipita mwaka jana, nadhani alipita aliona. Sasa mimi ni Mbunge natetea wananchi wangu baadaye naambiwa kwamba usipokuja na jibu zuri na mwaka huu ni mwaka mgumu!! Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri usikilize kilio cha wananchi wa Kata ya Godegode, daraja lijengwe.

Tunaposema kwamba tunakusanya bilioni 145 kwa mwezi, daraja halijengwi hawaelewi Serikali. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri, nimewapongeza mnafanya kazi nzuri sana kwa kweli ya kukusanya mapato na haya mapato kwa sababu ukishakusanya ya kutosha mnalipa madeni ya ndani na madeni ya nje, kulipa madeni ya nje ndiyo yanaijengea heshima nchi yetu. Lakini naomba sana pamoja na kwamba kulipa madeni ya ndani na nje, hizo fedha zinazobaki zitengwe kwa ajili ya kujenga madaraja katika barabara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya machache, nikushukuru tena na niwatakie kila la kheri Wizara hii, wanafanya kazi nzuri, tuwaombe na kama Mungu akijalia warudi tena katika Wizara hii waweze kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Huyu kwa leo atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho. Nimepata shida sana leo kuita watu, kwa sababu watu waliokuwa wanatakiwa kuchangia hawakuwepo. Hivi hawa wanaochangia nimeruka nimekwenda kwa wale wa Jumatatu. Sasa na wenyewe nikaanza kubabaika babaika wengine wanasema tuko tayari na wengine hatuko tayari. Kwa hiyo sasa, hatuwezi kuendelea. Lakini tujitahidi, tukishakuwa kwenye orodha, tujitahidi kwa sababu kuna wengine wanachangia kwa muda mfupi sana, mtatuwezesha Waheshimiwa wengi kuchangia, kwa sababu wengine wanachangia muda mfupi. Sasa unapokuwa na nafasi kwa siku nyingine basi angalau uwe *around* hapa, utatusaidia sana.

Hivi sasa nimesharukia wale wa Jumatatu, lakini hata wenyewe nikawa nahangaika nao wanasema mpaka Jumatatu. Kwa hiyo, tujitahidi kuwepo karibu, tukishakuwa kwenye orodha hata kama uko namba 20 yawezekana mwingine akategea kidogo, mwingine hapa anaandika mimi nimejiondoa. Kwa hiyo, tukiwa karibu

tutaendelea kuchangia. Pamoja na hivyo, wale tuliowaruka sasa tumewaweka kwenye orodha bado, tutaendelea kuwapanga. Hilo la kwanza.

Pili, kuna tangazo la Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, anaomba Wajumbe wake wakutane kesho saa 4.00 asubuhi, Chumba Na.227. Halafu, tangazo lingine, Kamati ya Kilimo na Ardhi, mlishatangaziwa kwamba gari litaondoka saa 1.30 kuelekea Mpwapwa na kuna baadhi ya watu wameomba kuingia kule. Mimi nimewaruhusu wanaotaka kuingia kwenye gari lile pamoja na Mheshimiwa Lubeleje mwenyewe. Lakini, kadri ki-*mini-bus* kitakavyoruhusu viti ndivyo tutakavyochukua. Kwa hiyo, walio na *interest* ya kwenda Mpwapwa wangeweza kujiunga na kundi letu pale.

Hakuna matangazo mengine. Kwa hiyo, shughuli iliyobaki tunaliahirisha Bunge mpaka Siku ya Jumatatu, Saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.32 Usiku, Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu  
Tarehe 13, Juni, 2005 Saa Tatu Asubuhi)*